# UHAKIKI LINGANISHI WA SIFA ZA MASHUJAA: SAKAWA NA FUMO LIYONGO

**NA**

**JUDITH KEMUNTO**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.**

**OKTOBA 2015**

# IKIRARI

Hii ni kazi yangu binafsi na haijatolewa kwa shahada ya uzamili katika Chuo Kikuu chochote kile.

Sahihi ……………………………………………………… Tarehe ……………………..………

**JUDITH KEMUNTO**

(Mtahiniwa)

Kazi hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi:

Tasnifu hii imetolewa iwasilishwe kwa idhini yetu kama wasimamizi wa mtahiniwa:

Sahihi ……………………………………………………… Tarehe ……………………..………

**Prof. Wa Mutiso Kineene**

(Msimamizi)

Sahihi ………. ………………………………………..…… Tarehe ……………..…………….

**Dkt. Hanah Chaga Mwaliwa**

(Msimamizi)

# TABARUKU

Tasnifu hii namtabarukia mamangu mzazi Bi. Alice Kerubo aliyejitolea mhanga kunipa malezi mema. Mola akuruzuku kwa neema zake zisizo kikomo. Pia namtabarukia dadangu Irene Nyangweso, kwa kufanikisha masomo yangu. Mungu akujalie.

## SHUKRANI

Kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai, afya nzuri, uwezo na nguvu za kutimiza ndoto yangu. Ameniongoza katika bahari hii ya elimu, iliyojaa bughudha na kila nui ya kero na kunifikisha hatua hii. Aidha, namshukuru kwa neema zake za kila siku na kuniwezesha kufika kiwango hiki.

Ningependa kuwashukuru wasimamizi wangu, Prof. Kineene wa Mutiso na Dkt. Hannah Chaga Mwaliwa kwa kujitolea kusoma na kuniongoza katika tasnifu hii. Nawashukuru kwa moyo wangu wote kwa ushauri na mwelekeo walionipa kila nilipowahitaji. Isitoshe, walijitolea kunitafutia vitabu vya marejeleo ambavyo viliniwezesha kuiandika tasnifu hii. Mola awajalie zake baraka.

Vile vile, natoa shukrani za dhati kwa wahadhiri wote wa idara ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Nairobi. Hawa ni pamoja na Prof. John Habwe (mwenyekiti), Dkt. Iribe Mwangi (Mratibu), Dkt. Jefwa Mweri, Dkt. Ayub Mukhwana, Dkt. Evans Murage Mbuthia, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Amiri Swaleh, Bw. Basilio Mugania, Prof. Mwenda Mbatiah Prof. Kithaka wa Mberia (Idara ya Isimu), na wengine ambao sijawataja.

Shukrani maalum kwa mamangu mzazi, Bi. Alice Kerubo, kwa kuniwekea msingi bora wa masomo. Katika kunilea, kunifunza na kunielekeza pia kunipa motisha katika masomo yangu. Aidha amenifunza kunyenyekea na kuwaheshimu wote ninaotagusana nao.

Shukrani za pekee ninawatolea dada zangu Irene, Evelyn, Beatrice, Jackline, Pincess na kakangu Bob. Mungu awajalie maisha marefu na heri njema kwa msaada mlionipa.

Mwisho, ni kwa wanafunzi wenzangu kwa kunitia moyo na kushirikiana nami katika masomo yangu. Ninawashukuru kwa urafiki wenu wa miaka hii ambayo tumekuwa katika darasa moja na hasa kwa fursa mliyonipa kuwa mwakilishi wenu wa darasa. Kwa wote ninasema asanteni. Pamoja na hawa, wapo wengine wengi walionifaa kwa njia moja au nyingine lakini siwezi kuwataja kila mmoja hapa. Kwa jumla ninasema shukrani jazilan.

## YALIYOMO


**IKIRARI** ..... i

**TABARUKU** ..... ii

**SHUKRANI** ..... iii

**VIFUPISHO VYA MANENO** ..... viii

**IKISIRI** ..... ix

**UTANGULIZI** ..... 1

1.1. **USULI WA MADA** ..... 1

1.2. **TATIZO LA UTAFITI** ..... 4

1.3. **MASWALI YA UTAFITI** ..... 4

1.4. **MADHUMUNI YA UTAFITI** ..... 4

1.5. **NADHARIA TETE** ..... 5

1.6. **SABABU ZA KUCHAGUA MADA** ..... 5

1.7. **UPEO NA MIPAKA** ..... 6

1.8. **MSINGI WA KINADHARIA** ..... 6

1.9. **YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA** ..... 15

1.10. **MBINU ZA UTAFITI** ..... 21

**HISTORIA YA FUMO LIYONGO NA SAKAWA KWA KUFUNGAMANISHWA NA YA JAMII ZAO** ..... 22

2.0. **Utangulizi** ..... 22

2.1. **Vikale** ..... 22

**2.1.1.** **Aina za vikale** ..... 23

2.2. **Jagina wa Kijamii** ..... 27

2.3. **Aina za Majagina wa Kijamii** ..... 28

2.4. **Historia ya Waswahili** ..... 28

2.5. **Misukosuko ya Kivita iliyomzua Fumo Liyongo** ..... 31

2.5.1. **Historia ya Fumo Liyongo** ..... 34

2.6. **Historia ya Wakisii** ..... 39

2.7. **Mikakati iliyomzua Sakawa** ..... 44

2.7.1. **Historia ya Sakawa** ..... 45

2.8. **Hitimisho** ..... 50

**ULINGANISHI WA SIFA ZA KISHUJAA ZA FUMO LIYONGO NA SAKAWA** ......................... 51
3.0. **Utangulizi** ........ 51
3.1. **Muhtasari wa *Utenzi wa Fumo Liyongo*** ........ 51
3.2. **Muhtasari wa *Kivuli cha Sakawa*** ........ 54
3.3. **Sifa za Mashujaa** ........ 55
3.3.1. **Kuzuka kwa Mashujaa** ........ 55
3.3.2. **Ubashiri wa Kuzaliwa kwa Jagina** ........ 56
3.3.3. **Shujaa kwa Kawaida huwa Mwanamume** ........ 57
3.3.4. **Kuzaliwa na Ujana wa Jagina** ........ 58
3.3.5. **Shujaa Hutokana na Ukoo Bora/ Ukoo wa Kifalme** ........ 60
3.3.6. **Shujaa huwa na Maadui / Wapinzani** ........ 60
3.3.7. **Shujaa huwa Kipenzi cha Wanajamii** ........ 61
3.3.8. **Safari ya Shujaa** ........ 63
3.3.9. **Mashujaa huwa na Akili Pevu/ Uwezo wa Kung'amua au Kutabiri** ........ 67
3.3.10. **Maisha ya Mashujaa huwa ya Dhiki Tupu** ........ 68
3.3.11. **Maisha na Matendo ya Mashujaa huwa ya Kimiujiza** ........ 69
3.3.12. **Mashujaa huwa na Kimo Kikubwa na Nguvu Nyingi** ........ 70
3.3.13. **Ndoa** ........ 71
3.3.14. **Shujaa Uhusishwa na zaidi ya Jamii Moja** ........ 72
3.3.15. **Usaliti wa Jagina** ........ 73
3.3.16. **Wasaliti wa Majagina Hawaishi kwa Muda Mrefu/ Hutaabika** ........ 75
3.3.17. **Kifo cha Jagina / Siri ya Kifo cha Jagina** ........ 76
3.3.18. **Utabiri wa Majagina Hutimia** ........ 77
3.3.19. **Jagina Huwa Gwiji katika Vita** ........ 78
3.3.20. **Shujaa "Hafi" na Hukumbukwa Milele** ........ 80
3.3.21. **Jina la Jagina** ........ 80
3.3.22. **Jagina huchukuliwa na Jamii kama Hidaya** ........ 82

3.4. **Hitimisho** ........ 83
**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO** ........ 85
4.0. **Utangulizi** ........ 85
4.1. **Muhtasari wa Utafiti** ........ 85
4.2. **Matokeo ya Utafiti** ........ 86
4.3. **Mapendekezo** ........ 88
4.4. **Hitimisho** ........ 88
**MAREJELEO** ........ 90

## VIFUPISHO VYA MANENO

| | | |
|---|---|---|
| BK | - | baada ya Kristo |
| khj | - | kama hapo juu |
| n.w | - | na wengine |
| n.k | - | na kadhalika |
| k.m | - | kwa mfano |
| k.v | - | kama vile |

# IKISIRI

Kuna tafiti kadhaa zilizowahi kufanywa kuhusu majagina wa Kiafirika. Hata hivyo hakuna utafiti linganishi uliowahi kufanywa kuwahusu Fumo Liyongo na Sakawa. Tasnifu hii inazilinganisha sifa zao jinsi zinavyojitokeza katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* (Kijumwa 1973) na *Kivuli cha Sakawa* (Matundura 2010) kwa kuzingatia nadharia ya uhakiki wa vikale. Historia yao pamoja na ya jamii wanamotoka mashujaa hawa zimechunguzwa ili kuweka msingi thabiti wa kuzichunguza sifa zao. Inadhihirika kwamba vikale hujitokeza katika vipindi na maeneo mbalimbali kwa kurejelea wakati na mazingira ambamo tungo hizi ziliandikwa. Isitoshe, vikale huwa havifungamanishwi na utanzu mmoja inavyobainika kutoka kazi hizi tulizozitumia katika utafiti huu. Kwa kuongozwa na ubia wa sifa za majagina utafiti umebainisha kwamba mashujaa hawa wana sifa kadha ambazo zinafanana kuliko zile zinazowatofautisha. Sifa zilizozingatiwa katika kuwalinganisha ni zile za kihistoria, kijamii na za kimaumbile.

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1.**USULI WA MADA**

Kila jamii huwa na mfumo wenye asasi anuwai ambazo hutegemeana, huingiliana na kukamilishana kwa manufaa ya wanajamii wote katika kutekeleza na kukidhi mahitaji yao kwa wakati fulani. Jamii, kwa mfano, huwa na asasi za elimu, ndoa, afya, sheria, ulinzi na uchumi kati ya nyinginezo. Ushujaa pia ni asasi ambayo haijaachwa nyuma kwenye jamii nyingi ulimwenguni. Mashujaa wamekuwepo ulimwenguni tangu zama za mababu zetu. Mashujaa hawa huenziwa na wanajamii na huchukuliwa kama hidaya kutoka kwa Mungu kwa wanajamii. Wanajamii huamini kuwa shujaa huwa ametumwa kwao wakati fulani kwa sababu ya lengo fulani mahususi, kama vile; kunusuru jamii kutokana na dhiki fulani au masaibu ambayo yameisibu jamii husika katika kipindi mahususi ili waishi maisha mema.

Kutokana na ukweli kwamba shujaa ni mtu mashuhuri sana katika jamii, ni muhimu kueleza shujaa ni nani hasa. Katika kueleza shujaa au jagina ni nani, tutarejelea maelezo ya wataalam mbalimbali ambao wameshughulikia masuala ya majagina. Katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* jagina ameelezewa kupitia kwa neno shujaa kuwa ni mtu mwenye moyo thabiti anayeweza kukabili mambo, hata kama ni ya hatari, ujasiri, nguli, jabali, abtali, ghazi au nyamaume, anayeweza kukabiliana na mambo hatari bila hofu (TATAKI 2013:509; Longhorn 2011:461). Kutokana na maelezo haya, tunaona kwamba shujaa ni mtu jasiri asiyekuwa na woga na aliye imara kwa jambo lolote lile wakati wowote.

Mutiso (1999:1) anadai kuwa shujaa ni kiumbe wa kweli ambaye amekuzwa na akajikuza mwenyewe hata akaonekana kiumbe wa ajabu. Kiumbe huyu huwa ni mashuhuri na husifika kwa ujasiri, nguvu na kwa kila jambo lionekanalo kubwa au la ajabu katika jamii husika. Mutiso,

anataja aina tatu za mashujaa.Kwanza, kiumbe wa kweli ambaye amekuzwa na jamii nayeye mwenyewe kujikuza. Pili, kiumbe wa kihurafa, ambaye ameumbwa na jamii yake na huwa na sifa ambazo si za kawaida, ghalibu awe Mungu au mtoto wa Mungu au yote mawili. Tatu ni mhusika mkuu katika utenzi, tamthiliya, riwaya, hadithi, ngano, sinema, kitendo au jambo. Anasisitiza kwamba mpaka kati ya aina hizi tatu ni mwembamba kwani mhusika mkuu anaweza kuwa mmojawapo wa aina mbili zingine za mashujaa.

Kwa kuzingatia usuli, kuna mashujaa wa kihistoria na wa kidini. Mifano ya majagina wa kihistoria ni kama vile Shaka Zulu wa Wazulu, Lianja wa Wamongo, Elijah Masinde wa Waluhya na Lwanda Magere wa Waluo. Yesu Kristo wa Wakristo na Mtume Muhammadi wa Waislamu ni mifano mizuri ya mashujaa wa kidini. Katika kazi za fasihi andishi, kuna mashujaa ambao ni wahusika wakuu katika utenzi, tamthilia, riwaya na kazi nyingine za kifasihi, kama anayoeleza Mutiso (1999:1). Kwa mfano, kuna Mfalme Edipode katika tamthilia ya *Mfalme Edipode* (1971) yake Sofokile.

Gichamba (2005:1)anasemashujaa huwa na tabia fulani za kipekee ambazo huwastaajabisha wanajamii ambao humwona kuwa kiumbe asiye wa kawaida na kwamba shujaa huendelea kuwepo katika hali zote za kijamii, hata baada ya kifo chake.Mwegemeo wa Gichamba ni jinsi wanajamii humchukulia shujaa mwenyewe kutokana na jinsi alivyosawiriwa.Aidha, tunaweza kusema kuwa katika migani, shujaa ni mpiganaji hodari ambaye mara nyingi ni mtoto wa kiume wa Mungu ama mfalme. Shujaa ni mhusika mkuu katika hadithi ambaye huwa na hulka zinazoenziwa na wengi.

Kwa hivyo, kutokana na maelezo haya, tunaweza kusema kwamba shujaa huwa ni mtu mwenye sifa za kipekee. Sifa hizi wakati mwingine hupigwa chuku ili kuwafanya wanajamii kumwona

shujaa kama kiumbe asiye wa kawaida. Aidha, shujaa huzuka kwa manufaa ya watu wake. Mashujaa hukumbukwa daima na husifiwa kwa kutungiwa nyimbo, ngano na tenzi na kwa hivyo hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kwa mfano kuna *Utenzi wa Fumo Liyongo* na wimbo unaomhusu Sakawa. Hivi ni kusema kwamba, mashujaa wamekuzwa kwa kupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa njia mbalimbali kama vile nyimbo na hadithi kama migani ambayo huwasawiri mashujaa kwa njia ya kipekee. Maendeleo katika maisha ya binadamu yameibua kuvumbuliwa kwa maandishi ambayo yamekuwa sehemu muhimu ya kuhifadhi habari za majagina wa ulimwengu. Kazi nyingi za majagina kutoka sehemu mbalimbali ulimwenguni zinaweza kupatikana kwa urahisi na hili limesababisha watafiti wengi kutafitia majagina. Katika nyingi ya tafiti hizi, tunapata kuwa baadhi ya sifa ni bia.

Mashujaa wote wanakisiwa kuwa na sifa nyingi zinazoshabihiana au zinazokaribiana kwa kiasi fulani. Sifa hizi ni kama vile  kuwa na maumbile ya kiajabu. Kama vile kuzaliwa na upungufu wa kiungo fulani cha mwili lakini wakawa na nguvu ajabu, kwa mfano, Sundiata wa Mandika. Vifo vyao kutokea kwa njia ya ajabu kama Fumo Liyongo na Sakawa, kuangamizwa kwa shujaa kutokana na kusalitiwa na jamaa zao au watu wa karibu sana nao kama Samsoni, kuangamizwa na watu wasiokuwa na uwezo kama wao, kukabiliwa na mgogoro mkubwa, kuzaliwa kwa ajabu kama Yesu Kristo, kuwa na msukosuko katika jamii kabla ya kuzaliwa kwa shujaa, kuleta mabadiliko katika jamii yake, kuwa na uwezo wa kutabiri mambo na nyinginezo.

Ni katika misingi hii basi, tutawalinganisha mashujaa wawili, Fumo Liyongo wa Waswahili, kama anavyosawiriwa katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* (Kijumwa1973) na Sakawa wa Abagusii anavyosawiriwa katika *Kivuli cha Sakawa* (Matundura2010).

## 1.2.**TATIZO LA UTAFITI**

Kila jamii ina jagina wake ambaye huwa na sifa za kipekee zinazomtambulisha. Wataalamu kadhaa wamelishughulikia swala la majagina ambapo sifa bia za majagina kote ulimwenguni zimeorodheshwa katika viwango mbalimbali. Hawa ni pamoja na: Kunene (1971), Butler (1979), Mutiso (1985 na 1999), Gichamba (2005) na Achieng’ (2012). Hata hivyo, hakuna utafiti uliowahi kuwalinganisha Sakawa na Fumo Liyongo ili kubainisha iwapo wanadhihirisha ubia wowote.Hivyo basi katika utafiti wetu tumelenga kuziba mwanya huu wa kiakademia kwa kuzipambanua sifa za kishujaakwa misingi ya sifa bia za mashujaa kama zinavyojitokeza katika usimulizi wa *Kivuli cha Sakawa* na katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Katika kuchanganua sifa hizi, tumeangazia sifa zinazofanana katika kazi hizi mbili na vilevile sifa za kishujaa zinazotofautiana. Aidha, tumetoa ufafanuzi wa mazingira ya kijamii yaliyowazua kama ambavyo tumeeleza hapo juu.

## 1.3. **MASWALI YA UTAFITI**

i. Ni sifa zipi za kishujaa zinazojitokeza katika *Kivuli cha Sakawa* na *Utenzi wa Fumo Liyongo*?
ii. Je, ni sifa zipi zinazofanana na ni zipi zinazozotofautiana za majagina hawa wawili?
iii. Je, mazingira yaliyochangia kuzuka kwa majagina hawa wawili ni sawa ama mambo yaliyochangia kuzuka kwao katika jamii zao ni tofauti?

## 1.4. **MADHUMUNI YA UTAFITI**

Katika utafiti wetu tuna madhumuni yafuatayo:

i. Kuzipambanua sifa za kishujaa za Sakawa na Fumo Liyongo zinavyosawiriwa katika *Kivuli cha Sakawa* na *Utenzi wa Fumo Liyongo.*

ii. Kuchunguza sifa za mashujaa zinazofanana na zinazotofautiana.

iii. Kuelezea historia ya Fumo Liyongo na Sakawa kwa kuifungamanisha na ile ya jamii zao ili kuonyesha yale mambo yaliyochangia kuzuka kwao katika jamii zao.

## 1.5. **NADHARIA TETE**

Nadharia tete za utafiti wetu ni kama zifuatavyo:

i. Fumo Liyongo na Sakawa ni mifano ya mashujaa wa kihistoria wa Kiafrika.

ii. Sifa za mashujaa hawa wawili, kwa kiasi kikubwa, zinafanana na tofauti yao ni ndogo sana.

iii. Kuzuka kwa mashujaa hawa ni kutaka kutetea kabila lao dhidi ya adui na ndiko kuliwajenga kama mashujaa.

## 1.6. **SABABU ZA KUCHAGUA MADA**

Uhakiki wa tungo za fasihi simulizi za Kiswahili umeshughulikiwa na wataalamu kadha ambao hutumia nadharia za kimagharibi ikiwemo ile ya uhakiki wa vikale. Nadharia hii imeendelea kuimarika katika uhakiki wa kazi za fasihi. Kazi za fasihi ya Kiafrika zimekumbwa na tatizo la kutathiminiwa kwa misingi ya nadharia za kimagharibi. Kutokana na madai haya, mtafiti ameonelea kwamba kuna haja ya kutanua nadharia ya uhakiki wa vikale na kubainisha utendakazi wake katika tungo za fasihi simulizi za Kiswahili.

Wataalamu wengi hukubaliana kwamba majagina wa fasihi hufananakwa njia moja au nyingine, jambo ambalo huwafanya majagina kudhihirisha ubia (Mutiso 1999). Hii ina maana kwambaubia huu hudhihirika katika majagina wote. Ingawa kuna ubia wa majagina, majagina wa jamii nyinginezo kama vile Zulu na Luowamefanyiwa utafiti zaidi kwa kuwalinganisha na majagina wa Uswahilini, hasa Fumo Liyongo huku jamii nyingine kama vile Wakisiizikikosa

kushughulikiwa. Kutokana na hali hii, pana haja ya kuchunguza iwapo upo mfanano katika shujaa Fumo Liyongo na Sakawa ili kuziba pengo lililoibuliwa na tafiti za awali zilizoegemezwa kwa uchunguzi wa jamii nyinginezo.

Kutokana na historia, tunaelezwa kwamba jamii za Waswahili na Wakisii zina uhusiano wa karibu kwa kuwa wote ni Wabantu. Hii ina maana kwamba, katika kipindi fulani cha historia yao waliingiliana, wakatagusana na kubadilishana mawazo kwa mtindo mmoja. Ni katika muktadha huu wa kuingiliana mtafiti alionelea achunguze iwapo uhusiano unajitokeza kwenye visa vya majagina wa jamii hizi.

## 1.7. **UPEO NA MIPAKA.**

Suala la taasisi ya ushujaa ni pana, hivyo basi itamlazimu mtafiti kuchukua muda mrefu ili kuweza kulishughulikia suala nzima ipasavyo. Basi katika utafiti wetu tumezamia sifa za Fumo Liyongo zinavyojitokeza katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* na sifa za Sakawa kama anavyosawiriwa katika *Kivuli cha Sakawa*na kazi nyingine zinazomzungumzia Sakawa. Katika kufanya hivi, tumelinganisha sifa za mashujaa hawa kwa mujibu wa sifa bia na kuangalia zile zilizo tofauti kati yao.

## 1.8. **MSINGI WA KINADHARIA**

Katika utafiti huu, tumeongozwa na nadharia ya uhakiki wa vikale. Huu ni mkabala wa uhakiki unaozingatia ruwaza za kimsingi za visasili na za kitambiko ambazo hujirudiarudia katika visakale na taratibu nyingi katika tamaduni anuwai uliotokana na maelezo ya Carl G. Jung kuhusiana na akili-laza (Abrams 1999:12-14). Jung alitumia istilahi ya vikale kwenye taswira za asili za kumbukumbu zinazorudiwarudiwa kutokana na tajiriba katika maisha ya tangu mababu zetu wa kale kama utaratibu wa kushughulikia tatizo la sifa bia. Alisisitiza kuwa, taswira hizi

hurithiwa na kutiwa kwenye akili-laza jumuishi ya jamii ya watu na ambazo hudhihirika katika visasili, ndoto, mawazo ya binadamu mathalan, katika vipengele vyote katika maisha ya binadamu wote duniani na katika kazi za kifasihi. Katika uhakiki wa kifasihi, vikale hutumiwa katika ruwaza ya aina za wahusika au taswira ambazo zinafanana katika tungo mbalimbali za kifasihi na pia katika visasili na mitindo anuwai ya kijamii. Kufanana katika maswala haya anuwai huchukuliwa kuakisi seti ya ruwaza bia ambazo zimekuwepo tangu jadi. Nadharia ya uhakiki wa vikale kwa hivyo inaeleza kuwa binadamu wote ni sawa popote walipo. Tofauti ni ndogo za kufikirika ambazo husababishwa na tofauti za kihistoria na za kimazingira.

Jung aliamini kwamba busara na afya njema hujitokeza pale binadamu wanapatana vyema na vikale na ishara bia kwenye akili-laza jumuishi. Alihofia hali ya watu kutegemea mno sayansi na mantiki katika kuelewa na kufumbatia hali zao za kiasili na zisizo razini, jambo linaloweza kuwafanya kupoteza kitu fulani maishani mwao. Kulingana na Jung (1990), kuna sehemu ya pili ya akili ya mwanadamu iliyo chini ya ile ya kwanza. Sehemu hii anaiita akili-laza. Hapa ndipo huhifadhiwa vikale vyote. Yaliyomo kwenye vikale hivi ni dhihirisho la michakato ya jumla ya akili-laza ya wanajamii (tutaita hili akili-laza jumuishi kwenye uchunguzi huu) ambazo awali kabisa hujitokeza kama jazanda. Nadharia yenyewe iliibuka kutokana na kutumia dhana zilizojitokeza kwenye elimu visasili pamoja na uchanganuzi-nafsi katika uchunguzi wa tungo za kifasihi. Ilipata umaarufu ilipotumiwa kuchanganua kazi za Maud Bodkin na William Troy huku misingi ya mfumo ikichotwa kwa nadharia za Lord Raglan (Burton 1968).

Katika uhakiki wa kazi za kifasihi, kikale huwa “aina za sifa, ruwaza za usimulizi zinazojirudia, ruwaza za utendaji, dhamira, taswira na motifu ambazo huweza kutambulika kwenye tungo kadha za kifasihi, ambazo hujumuisha visasili, ndoto pamoja na miviga ya jamii (Jung 1996: 115). Kwa mujibu wa Mutiso (1999:2), vikale hurejelea ruwaza za aina moja au nyingine za

kimsingi, za kijumla au zilizo bia. Uhakiki wa vikale hujihusisha na jinsi ruwaza zinazojirudia za mila, utamaduni, taswira na imani huathiri kazi za kifasihi. Ishara fulani huwakilisha wazo lilelile, wakati na mahali popote. Watunzi huzingatia ishara hizi ili kufikia akili laza za hadhira. Hivi vikale ndivyo hutumiwa kama malighafi ya kuumba ulimwengu ambayo binadamu wanaweza kuyaepuka[1]. Vikale hutumiwa na jamii zote ulimwenguni kuunda ngano zake. Ruwaza zinazojitokeza kwenye vikale huwezakudhihirika katika jamii za watu mbalimbali ulimwenguni na ndizo humvutia msomaji ikiwa zitatumiwa vizuri katika kazi ya fasihi hasa kwenye visakale.

Kwa mujibu wa Plato, duniani kuna wazo ambalo ni kamilifu na la kudumu na linaweza tu kufahamika kupitia kwa akili wala si kupitia kwa hisia. Kile ambacho binadamu hukihisi au kukiona kwa kutumia viungo vyake vya mwili huwa ni nakala isiyokamilifu na yenye ukinzo ya kile kilichokikamilifu, ambacho anakiita “kikale”. Jung, kinyume na usomi wa saikolojia kwa wakati wake ulioegemea kwenye mawazo ya Locke, kwamba mtoto huzaliwa bila akili yoyote, alipanua maoni ya Freud kuhusu akili-laza, akidai kwamba sehemu hii ya ubongo kumefichamwa pia mawazo ya kale ambayo binadamu wa sasa huwa nayo yanayofanana na yale ya mababu zao. Jumla ya mawazo haya yaliyomo kwenye akili-laza za wanajamii ndiyo anayarejelea kama vikale. Jung anayachukulia mawazo haya kama vitamalaki, taswira dumifu, na vikale. Hivyo basi, ung’amuzi wa pamoja wa kijamii wa kujirudiarudia kwa taswira hizi ndizo vikale ambavyo huwa na maana ya masimbi ya tajiriba mbalimbali za aina moja. Jung anasema kwamba visasili huwa njia ambayo kwayo vikale hujibainisha na “kueleza” akili tambuzi na mara nyingi hujitokeza kwenye ndoto za binadamu. Katika hali hii, Jung aliona kwamba kuna uhusiano wa karibu kati ya ndoto, visasili na sanaa. Hii ni kwa sababu zote huwa kama njia ya kuwasilishia mawazo ya akilini. Njia hizi zote hupitia kwenye kikale na kufikia akili tambuzi.

Jung anasema kwamba yeyote aliye na ung'amuzi wa kiasili, anayezitambua ruwaza za vikale pamoja,ana kipawa cha kuzungumza kwa kutumia taswira za kiasili ambazo humwezesha kuwasilisha tajiriba za "ulimwengu wa ndani" kuelekea kwa "ulimwengu wa nje" kupitia kwa sanaa. Msanii hutegemea visasili ili kusimulia anayoyapitia kwa ufaafu zaidi (Zhugang 1997: 164).

Kulingana na Jung, binadamu wote huitikia kisa kwa namna iliyo sawa kwa sababu, kwenye akili-laza jumuishi kuna kumbukumbu za kale yao ambayo ina kitovu kimoja. Kumbukumbu hizi ndizo vikale. Mwelekeo wake wa uhakiki unaonekana kushabihiana na mawazo ya usomi wa awali katika nchi za magharibi. Uhalisia wa Kiplato, uliosisitiza urazini bila uthibitisho wowote wa kijarabati, ulisisitiza kuwepo kwa ulimwengu wenye vitu kamilifu visivyo na dosari yoyote ambao hudhibiti vitu vyote vilivyo duniani; uhalisia wa Kiaristoto kwa upande wake ulikataa kuwepo kwa ulimwengu unaodaiwa kuwepo na wanauhalisia wa Kiplato na kupendekeza kwamba dhana hiyo ilijitokeza kwenye vitu mahususi. Ingawa uhalisia wa Kiaristoto uliegemea pakubwa kwenye mbinu za kiurazini, misingi yake haikuegemea tajiriba hivyo basi kuweza kutegemewa zaidi.

Jung aliiasisi nadharia ya "akili-laza jumuishi[2]" kwa maana kwamba binadamu aliyestaarabika huhifadhi maarifa ya kiasili ya enzi za ushenzi, ingawa bila kutambua kwamba ameyahifadhi. Kazi za awali za uhakiki wa vikale zilikuwa na misingi yake kwenye mawazo ya Jung ya "akili-laza jumuishi" ambayo yalichukuliwa kuwa yalidhibiti kujitokeza kwa ruwaza fulani za kimsingi katika fasihi.Kwa mujibu wa Burton (1968), miongoni mwa wataalamu wa kwanza kutumia nadharia ya uhakiki wa vikale katika kuchunguza ruwaza zinazojirudia katika tungo za kishairi ni Maud Bodkin (1934). Wasomi wengine watajika ambao wametafitia nadharia hii ni pamoja na Robert Graves, Francis Fergusson, Philip Wheelwright, Leslie Fiedler, Northrop Frye, Maud

Bodkin na G. Wilson Knight.Nao James Frazer na Jessie Weston wametafitia visasili vya kale na kuonyesha kwamba tabia na utamaduni hufuata ruwaza sawa katika vizazi vyote na maeneo yote ulimwenguni. Utafiti wao umeikuza nadharia yenyewe hadi ikawa mojawapo ya nadharia muhimu za kuchunguzia fasihi.

Joseph Campbell aliiendeleza nadharia ya Jung ya "akili-laza jumuishi" kwa kuihusisha na visasili baada ya kuchunguza dini, sanaa na ngano za ulimwenguni. Campbell anabainisha kwamba kazi hizi huwa na vipengele fulani sawa ambavyo huunganisha zote. Anaamini kwamba visasili ni ithibati ya "ndoto" jumuishi ya binadamu na ni "wimbo wa kila mlimwengu" (Campbell 1970). Uchunguzi wa Campbell unasisitiza juhudi za wanadamu za kusaka maana na ukweli tangu kizazi hadi kizazi.

Mihimili muhimu katika nadharia hii ambayo imetufaa kwenye uchunguzi huu ni:

i. Msisitizo kwenye ubia wa ishara zenyewe hivyo kusisitiza kwamba binadamu wote huwa na fikira sawa.

ii. Vikale hudhibiti muundo na jukumu la tungo zinazohusika. Hii ina maana kwamba maana ya matini hukumbwa na imani za utamaduni na kisaikolojia. Vikale huwa ni miundo ya kimsingi isiyoweza kufahamika ambayo hujitokeza kupitia taswira, ishara na ruwaza mbalimbali.

iii. Ruwaza za vikale huipa hadhira motisha ya kushiriki kwenye imani, hofu na dukuduku za kipindi wanamoishi. Nduni hizi za kivikale huchangia kwenye uelewa wa matini pamoja na kufafanua kiwango cha matamanio na wasiwasi wa binadamu (Sugg 1992).

iv. Msisitizo huwa kwenye ishara na ruwaza dumifu zilizomo kwenye tungo. Ngano na ishara zote zina misingi yake kwenye vielelezo vya masimulizi ya tajiriba za awali za wanajamii. Lengo hasa ni upataji wa maana bia katika sanaa. Mhakiki hulenga kupata hizi aina za kale

ambazo inachukuliwa kwamba hazijaingiliwa na dosari zozote wala kupotoshwa kwa njia yoyote ile. Hili huwezekana kupitia kuchunguza hali chache zinazojitokeza na kujirudiarudia.

v. Hudhihirisha ubia kwa kuwa huumbwa akilini mwa binadamu pasi kutegemea wakati au mahali.

vi. Kikale hujirudia kila mara tangu mwanzo hadi mwisho wa ulimwengu kwa kuwasilisha jinsi binadamu huitikia hali anamojikuta lakini yeye mwenyewe hawezi kubadilisha hali hizo.

vii. Msisitizo kwenye ruwaza zinazojirudiarudia za mandhari, msuko na uhusika ambazo hutoa mwangaza kuhusu tajiriba za wanajamii.

Katika utafiti huu tumetumia mtazamo wa Jung kwa kuwalinganisha Sakawa na Fumo Liyongo kwa kuzingatia sifa zao na maisha waliyoyaishi wakipambana na wapinzani wao majahili. Haya yote ni katika kudhihirisha kuwa majagina ni viwakilishi vya kikale cha kijamii ambacho kimo kwenye akili-laza yao kuhusu wanavyoyafasiri maswala yanayowapitikia.

Hii ni nadharia inayohusishwa sanasana na uhakiki wa visasili. Waitifaki wa uhakiki wa vikale huchukulia visasili kama muundo wa kimsingi katika fasihi kwa kuwa vina matumizi ya kina ya jazanda pamoja na maana dhanifu ambayo huweza kujitokeza katika aina yoyote ile ya fasihi. (Bressler 2011).

Tunapoirejelea nadharia ya fasihi, ni wazi kwamba fasihi huwa na sifa bia. Sifa bia za fasihi huiwezesha kulinganishika. Kwa mujibu wa Wamitila (2002:1; 2008:45), fasihi mbalimbali duniani huingiliana. Mwingiliano huu unatokana na ukweli kwamba binadamu ndio chanzo cha fasihi. Hii inatokana na sababu kwamba fasihi ina msingi wake katika jamii, nayo jamii imeundwa na binadamu. Ukweli huu, kwa mujibu wa Wamitila, ni kuwa fasihi za jamii tofauti ulimwenguni hazina budi kuingiliana, kama ilivyo miingiliano kati ya binadamu wenyewe.

Fasihi kama mali ya jamii hutumia lugha kama malighafi yake. Lugha ya binadamu huwa na sifa zinazofanana. Maudhui katika kazi za fasihi hutokana na mambo yanayoihusu jamii ya binadamu. Binadamu wote duniani husheheni sifa zinazofanana. Aidha, fasihi hulenga kutimiza wajibu fulani katika jamii kama vile kuonya, kukashifu, kuburudisha kuadilisha, na hata kuzindua. Fani ni kipengele muhimu katika kazi yoyote ya fasihi. Fasihi za jamii mbalimbali ulimwenguni huwa na fani zinazokaribiana kutokana na ukweli kwamba masuala mengi ya maisha ya binadamu yanafanana. Binadamu wanavyofanana, basi hata mashujaa hufanana.

Katika utafiti wetu, tumejikita katika masuala yanayomhusu binadamu. Tumemrejelea binadamu na tabia zake ulimwenguni, ili kuwalinganisha mashujaa wawili kutoka jamii mbili tofauti zinazoishi katika maeneo tofauti ulimwenguni. Kisaikolojia, binadamu wameweza kutafitiwa ili kubaini jinsi sifa bia za binadamu zinavyoshabihiana ulimwenguni kote. Utafiti wetu hata hivyo umeegemea zaidi upande wa anthropolojia linganishi ili kujibu madai ya wanaanthropolojia katika swali, 'kwa nini ruwaza za visasili na matambiko hujitokeza katika visakale na taratibu nyingi za watu mbalimbali ulimwenguni?' Ili kupata jibu la swali hili, ilibidi tuchukue mtazamo wa kijumla kuhusiana na uelewa wa tabia na mienendo ya binadamu ulimwenguni.

Binadamu wote ulimwenguni ni sawa kwani tunapoangazia masuala ambayo yanamjenga binadamu, tunaona kwamba jamii zote za ulimwengu zinafanana kwa sababu ya vipengele na desturi zinazoandamana kama vile dini, uchumi, mapenzi, elimu, sheria, utu, mapishi na uhusiano wa watu wa matabaka mbalimbali na wenye umri tofauti. Vipengele hivi hujengana, kuingiliana na kukamilishana jambo ambalo husababisha kuwepo kwa jamii ambayo imekamilika katika pande zote. Kwa mfano, makazi huwa muhimu kwa kuisetiri jamii ya binadamu kutokana na hali mbaya ya anga na hatari nyingine mbalimbali ambazo binadamuhuenda akakumbana nazo, pamoja na kuhifadhi mali yao. Makazi pia huwa ishara ya

umilikaji na umoja katika jamii ya binadamu – nyumba fulani itahusishwa na jamii ambayo huishi humo. Mapishi kwa upande mwingine huhusu jinsi jamii ya binadamu huandaa mlo wao kabla ya kuliwa. Mifano hii inaonyesha jinsijamii ya binadamu ilivyo ulimwenguni kote. Tofauti iliyoko ni jinsi jamii tofauti hutumia mikabala tofauti katika utekelezaji wa mambo yale ya kimsingi kutegemea matamanio, mazingira na mambo mengineyo.

Njogu na Wafula (2007:81-82) wakiwarejelea Jung (1972), Cuddon (1997) na Wamitila (2001) wanaeleza vile Jung alifanya utafiti juu ya usingizi na ndoto. Wanadai kuwa Jung alichukulia kikale kama ruwaza ya matukio anayopitia mwanadamu ambayo hujitokeza kama picha kongwe ijitokezayo mara kwa mara kutokana na tajriba ya binadamu maishani. Maulama hawa wanasisitiza kuwa mtu na utamaduni wake ni nakala ya wanadamu wengine waliokuwepo kabla yake miaka mingi iliyopita. Jung anadai kuwa mtu na utu ni wa kibinafsi ambao huathiriwa na jamii ya watu waliomzunguka. Mtu ni sharti atagusane na jamii yake ambayo humpa athari fulani. Mtu huathiriwa na sherehe mbalimbalianazofanyiwa na jamii yake. Kwa mfano, sherehe ya ndoa huathiri jinsi mtu aliyeoa au kuolewa atakavyotangamana na jamii. Jamii itatarajia mienendo fulani kutoka kwa wanandoa husika. Matarajio ya jamii yataathiri jinsi wanandoa wataingiliana na wanajamii wengine. Baadhi ya matarajio ya wanajamii yanatokana na visakale vinavyohusiana na masuala ya ndoa katika jamii husika.

Kuna masuala bia ambayo huwakumba watu wote mahali popote pale ulimwenguni. Anavyoeleza Gichamba (2005) akimrejelea Gennep (1960) masuala haya ni pamoja na; ujauzito na kuzaliwa kwa mtoto, ukembe, kushiriki kwa binadamu katika shughuli mbalimbali za jamii, jando, ndoa na hata kifo. Gennep anafafanua kuwa ingawa masuala haya hutekelezwa kwa njia tofauti tofauti katika jamii mbalimbali, uamilifu wao huwa sawa toka jadi za mababu zetu.

Kutokana na maelezo haya ya nadharia hii, hatuna budi kukubali kwamba jamii zote ulimwenguni huwa na mashujaa wao na mashujaa hawa huwa na sifa zinazofanana au zinazokaribia kuwa sawa. Akili laza ya mwanadamu humtweza shujaa licha ya ukweli kwamba shujaa huwa binadamu wa kawaida. Jamii humpa shujaa sifa ambazo ni za kipekee na huwa ni za kiuhalisiajabu, hivyo humweka shujaa katika kitengo ambacho si cha binadamu wa kawaida.

Kufanana kwa sifa za mashujaa duniani kote katika nadharia ya uhakiki wa vikale imekuwa nguzo muhimu sana katika uafiti wetu wa kulinganisha mashujaa hawa wawili kutoka jamii mbili zinazoishi katika majanibu tofauti, Fumo Liyongo na Sakawa.

Kwa kutumia nadharia hii, tumechunguza sifa, ruwaza na matendo ya mashujaa Sakawa na Fumo Liyongo. Kisha tumejaribu kuonyesha kwamba hizi ruwaza zinazojitokeza kwa wote wawili ni akisiko la yote yanayowapitikia binadamu maishani. Nadharia hii imetumiwa kupambanua kiulinganishi sifa za kishujaa za Sakawa na Fumo Liyongo kulingana na sifa bia za mashujaa. Nadharia hii ni muhimu kwetu kwa kuwa mihimili yake huwezesha kuchunguza mchango wa miundo inayojitokeza katika tungo mbalimbali na kulinganisha sifa za mashujaa ambao waliishi katika jamii tofauti na vipindi tofauti (Frye 1971 katika Halpé 2010; Bressler 2011). Kati ya mikabala mbalimbali ya nadharia hii iliyopo, mkabala wa Jung umetufaa zaidi kwa kuwa tunaamini kwamba ndio mkabala maarufu zaidi ambao umetajwa na wasomi wengi kwamba umedhihirisha athari kubwa katika uhakiki wa fasihi. Kwa mujibu wa Jung (1959), akili hukihusisha kikale fulani na ishara fulani ili kukihifadhi na kukiumbia maana. Pale kikale kinawasilishwa kwa akili, kinajitokeza kama picha fulani (uk. 81). Anayaendeleza haya mawazo kwenye chapisho lake la (1964) kwa kusema kwamba kila jambo halina maana mwanzoni hadi pale ambapo linadhihirika kujirudiarudia hivi kwamba binadamu anaanza kujenga picha fulani kulihusu hadi likapata nafasi akilini mwake (Jung 1964). Anavyosema Jung, ishara huja kwa

hiari wala hazibuniwi na binadamu. Kujirudia kwake humchochea binadamu kuziundia maana. Ishara hudokeza kuhusu kitu fulani ambacho hakijajulikana. Kahler (1961) anasema kwamba sanaa, ishara si tu uwakilishi bali pia hujumuisha yale ambayo bado hayajulikani, hayaonekani na hayajawahi kuelezwa[3].

## 1.9. **YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA**

Katika sehemu hii, tumerejelea kazi mbalimbali ambazo zinahusiana na mashujaa. Kuna zile za kinadharia ambazo zinaangazia masuala ya kijumla kuwahusu mashujaa. Kazi hizi zimekuwa za muhimu kwetu. Kuna zile ambazo zinazungumzia historia za jamii hizi ambapo Fumo Liyongo na Sakawa wametoka kwa mapana na marefu. Aidha kuna kazi mahususi ambazo zinawahusu mashujaa hawa. Kazi hizi zote zimekuwa muhimu kwetu.

Steere (1870) alikusanya na kuhifadhi katika maandishi *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar*. Huu ni mkusanyiko wa ngano za Waswahili. Ngano hizi zilipitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa njia ya utambaji. Kwenye mkusanyiko huu zipo ngano na masimulizi mbalimbali yanayomhusu Fumo Liyongo. Kazi hii imekuwa ya muhimu katika utafiti wetu hasa kuzipambanua sifa za shujaa Fumo Liyongo.

Harries (1962) ameeleza kuhusu ushairi wa Kiswahili. Ameeleza kuhusu mgogoro kati ya Liyongo na binamuye Daudi Mringwari, aila yake na pia ufafanuzi wa *Utendi wa Fumo Liyongo*. Maelezo haya ni muhimu kwetu kwani yametupa maelezo ya ziada mbali na yale yaliyo katika *Utendi wa Fumo Liyongo.*

Werner (1968) ametoa maelezo kuhusu mkusanyiko wa visasili na visakale vya baadhi ya Wabantu ambamo kuna madai kuwa Wabantu wote wana uhusiano wa karibu katika lugha, mila na desturi nyingi zinazofanana. Kufanana huku ndiko kumetuwezesha kuzitazama sifa za

majagina hawa wawili kiulinganishi. Pia ameirejelea hadithi ya Liyongo na kutoa maelezo kuhusu aila ya Fumo Liyongo na mgogoro uliokuwepo. Hadithi hii ni muhimu katika kuijua historia ya Liyongo katika utafiti wetu. Aidha, ameeleza kuwahusu mashujaa wengine wa Kibantu na kutoa picha za baadhi ya watu, shughuli zao na fenomena mbalimbali katika jamii ya Wabantu. Maelezo haya ni muhimu katika kuelewa utamaduni wa wanamotoka Fumo Liyongo na Sakawa.

Brooks (1970) katika tasnifu yake ameelezea historia ya Wakisii ambamo shujaa Sakawa ametoka. Kazi hii ni muhimu kwetu kwani imetusaidia katika historia ya jamii ya Wakisii na mazingira ambamo shujaa Sakawa alizuka pamoja na mtazamo wa wanajamii wenyewe kumhusu Sakawa.

Ochieng' (1971) amechunguza historia ya Wakisii kipindi cha kabla ya ukoloni. Isitoshe, kazi hii inashughulikia hali ya Kisii na Wakisii wakati alipoishi ama kuaminika kuishi Sakawa. Hii ni jamii ambayo anatoka Sakawa. Ameonyesha nafasi aliyopewa Sakawa katika jamii yake hasa kwenye vita. Hivyo basi, historia ya jamii yenyewe na msimamo wao kumhusu Sakawa ni muhimu kwetu.

Knappert (1979) ametoa maelezo kuhusu kipindi alichoishi Liyongo, historia ya Waswahili pamoja na maelezo mengine kumhusu Liyongo na tungo zake. Aidha mwandishi huyu pia amekusanya visasili na visakale ya Waswahili (1970). Kazi hii imekuwa muhimu katika utafiti wetu. Kazi hii imetusaidia kuelezea historia ya jamii ya Waswahili. Kutokana na uchunguzi wa Knappert tunafaidi kuelewa mikakati iliyomzua Fumo Liyongo.

Nurse na Spear (1985) wameeleza historia ya Waswahili pamoja na lugha ya Kiswahili baina ya karne ya saba na karne ya kumi na nne. Wameelezea masuala anuwai kuhusu historia ya

Kiswahili na Waswahili yakiwemo; asili ya Waswahili, asili ya lahaja mbalimbali, kuibuka kwa miji mbalimbali, kupanuka kwa jamii ya Waswahili, muindo ya kijamii na kiutawala katika miji mbalimbali, hali za kiuchumi na maingiliano baina ya Waswahili na watu wa jamii nyingine za Kiafrika. Kazi hii imekuwa muhimu katika kuelewa hali ilivyokuwa, kwani wengi hudai kuwa Liyongo aliishi katika kipindi hiki.

Mutiso (1985) ameshughulikia hurafa – linganishi kuwahusu majagina. Anairejelea *Kasida ya Hamziyya,* ili kuona vile inavyosema kuhusu Mtume Muhammadi, shujaa wa Waislamu. Analinganisha sifa za shujaa huyu na sifa za mashujaa wengine katika hurafa za jamii tofautitofauti ili kueleza hurafa na uyakinifu katika kasida hiyo. Kazi hii imekuwa muhimu kwetu, kwani imeorodhesha sifa bia za mashujaa ambazo ni msingi mzuri ambao umetufaa kuwaangazia Sakawa na Fumo Liyongo.

Mbele (1986) amerejelea utamaduni wa Liyongo na kuchunguza namna masuala mbalimbali kumhusu Fumo Liyongo yanavyosawiriwa na wasomi mbalimbali kama vile; Lyndon Harries, Jan Knappert, Edward Steere, Ali Jaddhmy, Sayyid Abdallah, Muhammad Kijumwa na Shihabuddin Chiraghdin. Mbele anayatazama makosa ambayo baadhi ya wasomi wanayafanya na hasa kutokana na kuyapapia maelezo ya wengine bila kuyatathmini kwanza. Anasisitiza umuhimu wa kusoma na kuyaelewa maoni ya maulama wengine na kwa hiyo kuwezesha kuwepo kwa hali ambayo itaondoa tashwishi zilizoko kuhusiana na utamaduni wa Fumo Liyongo. Mbali na maelezo haya, Mbele ametoa mtazamo wake kuhusu jina halisi la Liyongo. Anaonelea kuwa jina lenyewe linafaa kuwa Liyongo Fumo na si Fumo Liyongo na kwamba Fumo Liyongo alikuwa babake Liyongo Fumo. Naye pia hana uhakika katika madai haya kwani alitegemea kazi za awali ambapo ametoa ushahidi wake. Kazi hii imetusaidia katika kuuelewa

utamaduni na historia ya Liyongo. Isitoshe, majadala anaouibua kuhusu jinsi ya kutathmini maandishi kabla kuyakubali kwa jumla ni muhimu kwetu.

Mberia (1989) anamchukulia Fumo Liyongo kama shujaa wa masimulizi katika ngano za Waswahili. Katika makala haya, mwandishi amezibainisha sifa nne za Liyongo na kudai kuwa sifa hizi hupatikana katika masimulizi ya mataifa mengine duniani. Hizi ni pamoja na ushupavu, nguvu za kimwili, wepesi wa akili na stadi katika gungu na mwao. Anatoa ngano kumhusu Sundiata, ili kuonyesha visanga sawia na ngano ya Liyongo. Tofauti na makala haya, utafiti wetu utamwangalia Fumo Liyongo kama shujaa wa kihistoria bali sio shujaa wa ngano. Pia sifa za Liyongo kama shujaa ni zaidi ya nne kama ambavyo tumedhihirisha katika utafiti wetu. Sakawa kama shujaa hajatajwa popote katika makala haya. Madhumuni ya utafiti wetu ni kuzilinganisha sifa za kishujaa za Fumo Liyongo na Sakawa.

Mulokozi (1999) ameziharirі na kuzitolea maelezo tenzi tatu katika kitabu chake *Tenzi Tatu za Kale*.Tenzi hizi ni pamoja na; *Utendi wa Fumo Liyongo*, *Utenzi wa Al-Inkishafi* na *Utenzi wa Mwana Kupona*. Akirejelea Utenzi wa Fumo Liyongo, Mulokozi (khj) anaeleza sifa kuu tatu za shujaa wa utendi wa kiafrika ambazo ni: nguvu, uganga na mshikamano na kundi fulani au jumuiya fulani inayomuunga mkono. Kutokana na maelezo haya, Mulokozi amezifungia sifa nyingi nje za mashujaa wa kiafrika. Hata hivyo, kazi hii ni muhimu kwani imetusaidia katika kuelewa historia hasa wakati alipoishi Fumo Liyongo. Pia Utenzi huu una maelezo ya maneno ya kilahaja ambayo yametumika katika utenzi hivyo basi imetusaidia kuelewa zaidi *Utenzi wa Fumo Liyongo*, pamoja na kutupata mwangaza wa namna ya kuwalinganisha mashujaa mbalimbali.

Mutiso (1999) ameyalinganisha maisha na sifa za mashujaa wawili wa kidini, Buddha na Muhammadi, huku akirejelea sifa bia za mashujaa. Katika kuwasawiri mashujaa hawa, anataja kwa mpito tu mashujaa wengine duniani wakiwemo Fumo Liyongo na Sakawa. Kazi hii ni muhimu katika somo letu, kwa sababu anaeleza japo kwa kifupi hidaya ya jagina kwa jamii yake kama mojawapo ya sifa za mashujaa. Anasema kuwa Fumo Liyongo aliwaachia Waswahili gungu. Hajatueleza hidaya ambayo Sakawa aliwaachia Wakisii. Utafiti wetu umeangazia kwa kina sifa za mashujaa hawa wote wawili, Fumo Liyongo na Sakawa. Mkabala wake katika kuwalinganisha mashujaa umeufaidi uchunguzi wetu kwa kuwa tumewalinganisha Sakawa na Fumo Liyongo. Vile vile katika kazi hii, Mutiso ameshughulikia kwa kina ufafanuzi wa shujaa na kuelezea aina mbalimbali za mashujaa japo anasisitiza kuwa mpaka kati ya aina hizi mbalimbali za mashujaa ni mwembamba mno. Maelezo haya pia yamekuwa muhimu kwetu katika kufafanua shujaa ni nani.

Njogu na Chimera (1999:156-168) wametoa maelezo kuhusu majagina mbalimbali pamoja na sifa zao. Sifa wanazozitaja wataalamu hawa zimetufaa katika uchunguzi huu. Kazi hii imekuwa ya umuhimu kwetu katika kuzidondoa sifa za mashujaa Sakawa na Fumo Liyongo.

Miehe n.w (2004) walikusanya mashairi na nyimbo zilizodaiwa kutungwa na Liyongo kutoka kwa maktaba na hifadhi za nyaraka katika taasisi kadhaa ulimwenguni na kutoka kwa kazi awali zilizochapishwa. Kazi hii ilitokana na warsha zilizofanywa katika Chuo Kikuu cha Bayreuth Ujerumani miezi ya Juni / Julai 2003 na Machi / Aprili, 2004 ambazo zilikuwa na lengo la kuibuka na toleo ambalo lingekidhi mahitaji ya kiusomi kote ulimwenguni kutokana na mashairi na nyimbo zilizohusu Fumo Liyongo. Aidha walitoa maelezo kuhusiana na utamaduni wa Fumo Liyongo na fani zilizotumika katika mashairi hayo na nyimbo. Maelezo haya yamekuwa ya

muhimu kwetu katika kuelewa utamaduni wa Waswahili pamoja na kutupa mwangaza zaidi kumhusu shujaa Liyongo.

Gichamba (2005) amezilinganisha sifa za mashujaa Fumo Liyongo na Shaka Zulu kwa misingi ya sifa bia za mashujaa ulimwenguni pamoja na umuhimu wao kwa jamii zao. Kazi hii imetusaidia kumwelewa Fumo Liyongo kwa kina. Amemtaja Sakawa kama mfano wa mashujaa wa kihistoria wa jamii ya Wakisii. Utafiti wetu umejikita katika kiwango cha kufanana na kutofautiana kwa mashujaa Sakawa na Fumo Liyongo. Mkabala aliouchukua Gichamba katika ulinganishi wake umetufaa katika utafiti wetu. Licha ya Gichamba (2005) kueleza sifa za Fumo Liyongo, hakutueleza sifa za Sakawa pamoja na historia yake ikifungamanishwa na jamii yake. Hivyo basi, utafiti wetu umeziba pengo hili.

Muniu (2011) katika tasnifu yake *Ujagina wa Mwanamke katika Pango,* amezungumzia sifa za majagina katika faslu ya kwanza. Anasema kwamba jagina husalitiwa huku msaliti wake akipata tabu hatimaye. Anamtaja Fumo Liyongo kama mfano wa shujaa anayesalitiwa na kuuawa na mwanawe. Mwishowe huyu mtoto wake anaachwa katika hali ya upweke na kuangamia. Ingawa kazi hii haijamshughulikia Fumo Liyongo kwa kina, imekuwa ya muhimu kwetu hasa katika kuelewa zaidi sifa za mashujaa kwa jumla. Sifa anazozitaja Muniu zimetufaa katika uchunguzi wetu kwa kuwa zimetuelekeza katika kuwahakiki mashujaa tuliowateua kuwalinganisha.

Achieng’ (2012) ameangazia sifa za majagina Fumo Liyongo na Lwanda Magere na umuhimu wao katika jamii zao. Kazi hii pia imetusaidia katika kumwelewa Fumo Liyongo zaidi. Achieng’ naye amemtaja Sakawa kama mfano wa mashujaa wa kihistoria kwa njia ya mpito tu. Hili pia limekuwa kichochezi kwetu cha kumfanyia utafiti Sakawa, ili kumwelewa zaidi na

historiainayofungamananakuzuka kwake. Mkabala wa ulinganishi aliouchukua Achieng' umetufaa kwa kuwa uchunguzi wetu ni wa kilinganishi.

## 1.10. MBINU ZA UTAFITI

Utafiti wetu umekuwa wa maktabani. Tumesoma vitabu, tasnifu na makala mbalimbali yanayohusiana na somo letu. Lengo la kusoma ni kutafuta sifa za Fumo Liyongo na za Sakawa huku tukizilinganisha na kuzitofautisha. Tumedurusu vitabu vinavyohusu historia ya jamii ya Waswahili na Wakisii. Habari ambazo tumepata katika vitabu na makala mbalimbali zimetusaidia katika kuelezea historia ya jamii hizi mbili na mazingira yaliyochochea kuzuka kwa mashujaa hawa kwani shujaa hazuku katika ombwe tupu. Vilevile, tumesoma *Utendi wa FumoLiyongo* na *Kivuli cha Sakawa.* Katika kusoma kazi hizi, tumelenga sifa za kishujaa zinavyojitokeza katika kazi hizi.

Isitoshe, tumesoma mashairi na nyimbo za watunzi mbalimbali kuwahusu mashujaa hawa. Aidha, tumewahoji wataalam waliobobea katika masuala ya kishujaa tukitilia maanani yale yanayosemwa na watu hasa wahadhiri kuhusu mashujaa.

---

[1] Kwa maelezo zaidi kuhusu vikale tazama sura ya pili ya tasnifu hii

[2] Tumetumia dhana hii kurejelea *"collective consciousness"*.

[3] Dhana hii ya ishara imeshughulikiwa na Northrop Frye katika *Anatomy of Criticism: Four Essays* (1957) ambaye anataja viwango vitano vya uashiriaji.

# SURA YA PILI

# HISTORIA YA FUMO LIYONGO NA SAKAWA KWA KUFUNGAMANISHWA NA YA JAMII ZAO

## 2.0. Utangulizi

Katika sehemu hii, mjadala wetu unahusu vikale, mashujaa kwa jumla, historia ya Fumo Liyongo na Sakawa, pamoja na ya jamii zao ambamo mashujaa hawa walizuka. Kwa kushughulikia jamii wanamotoka tumechochewa na ukweli kwamba majagina huzuka katika mifumo na hali mbalimbali za jamii husika na wala hawajitokezi kwenye ombwe tupu. Katika sehemu hii, tumeelezea historia ya Fumo Liyongo na historia ya Waswahili na historia ya Sakawa na Wakisii. Aidha tumejadili mazingira yaliyoibua kuzuka kwao huku tukiangazia vipengele mbalimbali vya maisha yao. Kabla ya kujadili historia za jamii wanamotoka mashujaa wa uchunguzi huu pamoja na historia zao, pana haja kufafanua kuhusu shujaa ni nani kwa kusisitiza sifa anazofaa kuwa nazo mtu ili kurejelewa kama jagina.

## 2.1. Vikale

Kwa kuwa tumetumia nadharia ya uhakiki wa vikale katika uchunguzi wetu ni muhimu kutoa ufafanuzi wa dhana ya vikale hapa ili kuiweka wazi zaidi nadharia yenyewe na kuonyesha uhusiano wake na uchanganuzi wa majagina. Kwa kuwa tumekwisha kushughulikia mihimili ya nadharia yenyewe kwenye sura iliyotangulia, kwenye sehemu hii tunashughulikia aina za vikale.

Jung (1959) akinukuliwa na Landman (2006), anasema vikale ni aina-mame ya awali kabisa ya kitu, hali au dhana ambayo kwayo taswira za aina yake (wahusika, ruwaza za usimulizi na kadhalika) huibuliwa, huigwa au huumbwa. Hii ina maana kwamba kikale ni aina-mame zinazowakilisha dhana, ambazo huweza kutumiwa kuchunguza na kufasiri hali zinazojitokeza katika maisha ya kila siku ya binadamu. Kundi la kumbukumbu pamoja na fasiri mbalimbali

ambazo huhusishwa moja kwa moja na kikale mahususi hurejelewa kama ‘tato’ na hurejelewa kwa kuzingatia kikale chake kilicho kiini kwa mfano tato ya kijagina.

Kwa kawaida kuna aina tatu za vikale: taswira, motifu au ruwaza za vikale na tanzu au aina za fasihi. Taswira za vikale hujumuisha maji, jua, rangi, maumbo mbalimbali kama vile duara, nambari, wahusika wa vikale kama vile mwanamke mwenye kafara, ayari, pamoja na mandhari mbalimbali kama vile kitalu, mti fuli, mlima au pango. Ruwaza za vikale hujumuisha uumbaji wa dunia, jagina, kifo, ukombozi na mageuzi. Tanzu za vikale huwiana na majira: majira ya kuchipuka au futuhi, majira ya joto au ulimbwende, vuli kuwiana na tanzia huku masika ikiwiana na kinaya (Guerin n.w. 2010: 227 - 231). Tanzu za vikale huhusishwa na Frye ambaye anadai kwamba aina zote nne za fasihi hujitokeza kwenye tungo moja hivi kwamba anaibuka na dhana ya monomithi (Frye, 1990: 192).

### 2.1.1. Aina za vikale

Jung (1969) anataja aina zifuatazo za vikale ambavyo vinaweza kuwa ama vya kiethmografia au vya kianthropomofia:

**i. Nafsi**

Nafsi ni mojawapo ya kikale cha kiethnografia inayoashiria muungano wa akili tambuzi na akili laza. Hii ina maana kwamba nafsi huwakilisha akili katika ukamilifu wake kwa kuhusisha sehemu zote za ung’amuzi. Kwa mujibu wa Jung (ametajwa) nafsi ni zao la ujitambulishaji unaomwezesha mtu kujenga hulka yake. Jung anatumia nafsi hapa kwa maana ya jagina. Hii ni kwa sababu jamii zote huwatumia majagina kuzihifadhi zile hulka za jamii walizo nazo.

**ii. Kivuli**

Kivuli, kama mojawapo ya sehemu za akili-laza ya binadamu haifafanuliki na mara nyingi huudhi. Hata hivyo huwa na hisia za juu kuliko sehemu za akili-tambuzi. Kivuli kinaweza kuwa

ni nafsi asilia (jagina), ambaye nafasi yake imechukuliwa wakati mtoto anapokua kupitia urazini na kujirekebisha kwake kulingana na maadili ya kijamii akielekezwa na akili yake tambuzi. Kumbukumbu zile ambazo anazidumaza kutoka kwa akili tambuzi huhawilishwa hadi kwenye akili-laza ama kuwa kama kivuli cha nafsi yake na kuwa kama sehemu dhahania ya kuzihifadhi. Sehemu hii haitumii urazini kama ilivyo sehemu ya akili tambuzi. Hata hivyo, hii haina maana kwamba kivuli ni sehemu iliyojaa matendo maovu. Ingawa inaweza kujitokeza kama isiyo na huruma na yenye kujibu inapochokozwa, sehemu hii hudhihirisha huruma pale inapoguswa na hisia. Kivuli huwa muhimu kwa ung'amuzi katika kuelewa hulka, mtazamo wake na jinsi anavyoitikia maswala yanayojitokeza katika ulimwengu wa nje. Kwa jumla, kivuli hutoa habari kuhusu vigezo vinavyoisumbua hulka ya mtu na uozo wowote ule wa kijamii.

Kivuli hujitokeza kwenye ndoto na njozi katika miundo tofauti tofauti, aghalabu kama kiumbe cha kuogofya ama zimwi na huweza kuwa ama rafiki au adui. Kwa jumla, pale ambapo suala la jinsia hujitokeza, kivuli huwa jinsia sawa na ya jagina. Kwa kuwa huwakilisha akili za enzi za mababu, kujitokeza kwake si kwa kiwango sawa na ule wa jagina. Maelezo ya kina kuhusu kutokea kwa kivuli na jukumu lake na kwa kiasi kikubwa hutegemea mazoea ya kila mtu. Hii ni kwa sababu kivuli mwanzoni huibuka kwenye akili ya mtu wala si kwenye kile Jung anakirejelea kama akili-laza jumuishi.

**iii. Anima**

Hii ni aina ya kikale cha kianthropomofia cha akili laza inayorejelea sehemu ya kike iliyomo ndani ya mwanamume au ya akili laza rejelewa. Hujumuisha sifa za kike zinazojitokeza kwenye tabia ya jinsia ya kiume. Kuna baadhi ya sifa za kike zinazojidhihirisha kwa wanaume. Kikale hiki huwa ni cha kimahusiano. Kinyume na animasi inayomhusu urazini (tazama sehemu inayofuata), anima huhusu maswala ya kisaikolojia na kijinsia. Anima hudhibiti uhusiano baina

ya mwanamke na mwanamume. Huwa kielekezi cha kiakili alicho nacho mwanamume cha kukutana na mwanamke na kutangamana naye.

Kikale cha mama ni mfano maarufu wa anima, kwa kuwa hutawala uhusiano kati ya mama na mtoto wake wa kiume na hudhirika kwenye kauli kama vile Mama Afrika. Inasemekana kwamba anima hujidhihirisha kwenye ndoto na kutawala maingiliano baina na mwanamke na mwanamume.

Jung anataja hatua nne ambazo anima hupitia ili kukomaa – Eva, Hellena, Maria na Sofia. Hii ina maana kwamba kukua kwa anima ni mchakato wa mwanamume kuziachilia huru hisia zake kathiriwa. Hatua ya kwanza, Eva, huhusu kujidhihirisha kwa taama aliyonayo mwanamume. Jina hili linatokana na kisa cha Adamu na Hawa. Hellena, ni jina linalotokana na ngano za Kigiriki kumhusu Hellena wa Troy. Kwenye hatua hii, wanawake huchukuliwa kuwa wenye ufanisi mkubwa duniani, wanaojitegemea na wenye akili pevu na maoni mazuri ingawa si wema. Hatua hii hunuia kuonyesha imani kubwa kwenye vipawa vilivyo nje bila hulka ya mhusika. Maria ni hatua inayohusishwa na Bikira Maria ambayo mwanamke huonekana kuwa na wema kwa kumuona mwanamume kuwa mtu mwenye sifa hasi ambazo hangependa kuhusishwa nazo. Hatua ya mwisho ya Sofia huwa mwanamke amejaa busara kiasi cha kumpenda mwanamume ambaye huwa na mseto wa hulka hasi na chanya. Hii ndiyo hatua ya mwingiliano kamili kwani mwanamke humruhusu mwanamume wahusiane.

**iv. Animasi**

Hii ni sehemu ya kiume aliyo nayo mwanamke au mhusika wa kike kwenye akili laza. Hujumuisha sifa za kiume zinazojitokeza kwenye tabia ya jinsia ya kike. Jung alijihusisha zaidi na anima kuliko animasi kwa kwamini kwamba hizi ni sehemu mbili zinazokamilishana. Hata hivyo anasema kwamba, animasi huwa changamano zaidi kuliko anima.

### v. Shujaa

Friedrich Nietzsche katika *Thus Spoke Zarathustra* (1961:49-111) amefafanua hatua tatu muhimu ambazo jagina huzipitia ili kufikia hadhi ya "ushujaa"[1]. Hatua ya kwanza ni kuwa na hamu ya kuharibu kawaida za kijamii zilizopo ambazo huwa tu za kidhanishi. Pili, kwa kuchanganua upya na kuvunjilia mbali kawaida za zamani, jagina huikataa dini na kubuni kanuni zake za kimaadili. Tatu ni, kuushinda ukataaji wa dini ambao hujumuisha hatua tatu nazo ni; mkosa maadili, mawazo huru na shujaa.

### vi. Ajuza mwenye Hekima

Huwakilisha umuhimu wa kuzingatia maadili maishani kwa kuwa hilo humwokoa mtu kutoka kwa hatari zozote na kumpa fursa kukua kufikia umri wa uzee.

### vii. Ayari

Hurejelea jagina au roho fulani njema ambayo hupinga kanuni na matakwa ya miungu, mara nyingi kwa kijicho ingawa hatimaye huwa na athari njema kwa wanajamii. Ayari huzivunja kanuni kwa kutumia wizi au ujanja.

### viii. Uungu

Hapa tunarejelea Mungu fulani ambaye huabudiwa na binadamu. Huweza kujitokeza kwa sura mbalimbali kama vile mtu, mnyama, mti au mlima. Miungu hawafi na huchukuliwa kuwa na akili, busara, hisia, tamaa na sifa nyinginezo zinazoakisi zile za viumbe wanaowainamia.

Hadi hapa tumedhihirisha kwamba mojawapo ya kikale ni jagina. Inahalisi basi kufafanua jagina ni nani hasa kwa kuzingatia sifa za kipekee ambazo huwa nazo kinyume na binadamu wa kawaida. Hili ndilo jambo ambalo tumelishughulikia kwenye sehemu inayofuata.

## 2.2. **Jagina wa Kijamii**

Shujaa ni mhusika ambaye husawiriwa na jamii yake kuwa na sifa za kiajabu. Sifa zake aghalabu huwa zimetiliwa chumvi hivi kwamba hawawi kama binadamu wa kawaida. Wanasawiriwa kwa namna ambayo huifanya hadhira kuingiwa na hisia fulani kuwahusu mashujaa hivi kwamba wanaweza kuwahurumia kutokana na jira inayowapata, kutaka kujihusisha nao kwa sababu ya matendo yao ya kujikomboa jamii au hata kujitambulisha nao (Green, 1997). Ili kuweza kuwatambua mashujaa pana haja kuwa na majahili ambao hukinzana nao ili kuchimuza sifa zao kwa uwazi zaidi.

Vikale wa kijagina wamekuwepo tangu Griki ya kale pamoja na utamaduni wa kuwa na miungu wengi wa kuabudiwa. Kama ilivyo katika aina nyinginezo za vikale, majagina huhusishwa na miungu na mababu za wanajamii. Kadiri muda unavyopita, sifa na matendo ya hawa mababu hubadilika kutokana na ukweli kwamba ngano hizi zinapopokezwa vizazi vingine hazina budi kubadilika kwa kiwango fulani (Wood 2005).

Katika visa vya kirasimi, majagina huwa na nguvu zisizo za kawaida; walizungumza na miungu kama vile Achilles au Theseus, ambao walichukuliwa kama nusu miungu. Haiwezekani jagina kunyang'anywa cheo chake cha ujagina (Childs na Fowler 2006). Jagina huwa na uwezo usio wa kawaida. Jagina hujitokeza kupigania haki za wanyonge walio wengi. Matendo yake ya kuikomboa jamii hujumuisha kuiokoa jamii kutoka kwa maangamizi ama mambo ya kuhatarisha maisha yao, kuvumbua hazina fulani iliyofichika ama kuunganisha jamii na jaala yao (Green 1997). Majagina wengi huzaliwa na kufa kiajabu. Hujengwa kwenye mgogoro unaotokea baina yake na jahili. Yeye huwa mwema mwenye umbo lisilo la kawaida. Umbo lake huchangia kwenye nguvu zake zisizo za kawaida zitokanazo na siri fulani. Mwisho wake huwa ambapo huangaishwa ama kuangamizwa na kosa dogo hasa la kujisaliti.

Hadi hapa tumeonyesha kwamba majagina huwa na sifa na nafasi ya kipekee katika jamii. Isitoshe tumebainisha kwamba huwa wa aina mbalimbali. Kwenye sehemu inayofuata tumeshughulikia aina mbalimbali za majagina

### 2.3. Aina za Majagina wa Kijamii

Kuna aina mbalimbali za majagina kama vile majagina wa kimajaliwa, majagina wa kihistoria, majagina wa kiayari, binadamu mwenye nguvu nyingi, jagina asiyejua, kijana mrembo ajabu, mganga au mtakatifu fulani. Jagina mtendaji si sharti awe na sifa za kipekee, lakini hupigana na jahili ili kupata ushindi (Aylestock 2009). Pia kuna majagina ambao hawafuati sifa za kimapokeo za majagina. Wapo majagina wanaoiga wengine ambao kwa sababu ya kutokuwa na kipawa au kujikuta kwenye mazingira mabaya, hawafaulu kuwa mashujaa. Mara nyingi wao pia humtegemea jagina mkuu. Jagina mwigo aghalabu hufa kishujaa akijaribu kumuiga shujaa mkuu. Mfano wa jagina mwigo ni Don Quixote (Tallman 2005).

Msijagina ni jagina ambaye hana sifa kadha za majagina. Aghalabu huishia kufanya jambo linalofaa, lakini maisha yake si kamilifu na yenye mashaka. Mara nyingi huwa na upungufu wa kimaadili (Campbell, Brown, na Stuart 2003).

Hadi hapa tumeonyesha aina mbalimbali za majagina katika jamii. Kwenye sehemu inayofuatia tumeshughulikia historia ya majagina wetu wa utafiti. Maswala ya jamii wanamotoka yameangaziwa ili kuwekea msingi wa kuibuka kwao kama msingi muhimu wa utafiti wetu.

### 2.4. Historia ya Waswahili

Kwa mujibu wa Guthrie (1948) Waswahili ni Wabantu. Jamii ya Waswahili imekuwepo katika upwa wa Afrika Mashariki kwa muda mrefu ingawa upwa huu haukuwa kitovu chao. Kitovu cha Wabantu ni eneo ambalo sasa linakaliwa na nchi za Cameroon na mashariki mwa nchi ya

Nigeria. Nurse na Spear (1985:33) wanadai kuwa baadhi ya Wabantu walihamia katika janibu za kusini mwa Afrika ilhali wengine wakiwemo Waswahili, walihamia mashariki na kukalia eneo la Shungwaya katika karne ya kumi na sita na mwanzoni mwa karne ya kumi na saba. Wanadai kuwa Khoisan ndio walikuwa jamii ya awali kabisa katika maeneo ya Afrika Mashariki kabla ya Wabantu, Wakushi na Wanailoti.

Walsh (1987:21) anadai kuwa Wasabaki walitengana na Wabantu, katika eneo la kaskazini mwa nchi ya Tanzania na kuelekea katika maeneo ya kaskazini kupitia Kenya na kuingia Somalia. Walifika katika eneo hili la Shungwaya kati ya karne ya kwanza baada ya Kristo. Mwishoni mwa karne hiyo, Wasabaki walitengana katika makabila tofautitofauti kama vile Waswahili, Wapokomo, Waelwana na Wamijikenda. Baada ya muda, Waswahili walianza kuhamia sehemu za kusini mkabala wa bahari ya Hindi. Baadaye, Wapokomo na Wamijikenda waliwafuata.

Tamaduni za jamii mbalimbali za Waswahili zinadai kuwa kuhama kwao hadi katika maeneo ya pwani kulitokana na mashambulizi ya mara kwa mara na Wagalla. Stiles (1981: 858) akinukuliwa na Gichamba (2005:26) anadokeza kuwa Wabajuni katika tamaduni zao wanadai kuwa Wagalla ndio waliowafukuza kutoka eneo la Shungwaya. Maoni yaya haya yanadokezwa na Werner (1915:328) kwa kusema kuwa mashambulizi ya mara kwa mara ya Wagalla ndiyo yaliyowafanya Wasabaki kukimbilia katika sehemu za kusini. Hata hivyo, mashambulizi haya hayakusita hata baada ya kuhamia pande za kusini. Nurse (1994:48) anadai kuwa magurio ya Waswahili yalizidishwa na uvamizi wa ghafla uliowafanya kuhamia katika eneo lililoko baina ya Mto Juba ulio kusini mwa Somalia kaskazini mwa Mto Tana.

Katika maeneo ya pwani, Waswahili walijikusanya katika makundi madogo madogo kwenye visiwa na sehemu nyingine. Walitapakaa kote kuanzia Somalia hadi Msumbiji. Mazingira yao ya

bahari yaliwaelekeza katika shughuli za uvuvi kama njia yao ya kiuchumi. Mbali na uvuvi, shughuli nyingine zilikuwa ni ufugaji wa wanyama na kilimo. Shughuli za uhunzi ziliwawezesha kuunda zana za kilimo kama vile majembe, mashoka, panga na visu. Aidha, walishughulika na uundaji wa zana za kivita kama vile mishale, vitara, jambia, ngao na misu. Useremala pia uliendelezwa ili kuunda baadhi ya vifaa vya nyumbani.

Mandhari ya bahari yaliwezesha usafiri kutoka sehemu moja hadi nyingine katika shughuli mbalimbali ikiwemo biashara. Aidha, wageni wengine walifika pwani ya Afrika Mashariki kutoka maeneo mengine. Mazingira haya yalileta mabadiliko katika utamaduni wa jamii ya Waswahili kisiasa na kiuchumi. Wageni wa awali walitoka sehemu mbali mbali kama vile, Uarabuni, Ghuba ya Uajemi, Ugiriki na Ureno. Wageni hawa walifika pwani ya Afrika Mashariki kwa sababu za biashara, utalii wa kijografia, kueneza dini. Wageni hao Waingereza walifika kwa nia ya kujitwalia maeneo muhimu pamoja na kusambaza dini.

Freeman–Greenville (1955:1) anadai kuwa Afrika Mashariki ambayo kwa sasa inajumuisha pwani za Somalia, Kenya na Tanzania ilitembelewa na Muhammed bin Abdallah bin Batuta. Uhusiano wake na wenyeji na uelewa wa mandhari ya Afrika Mashariki ulisaidia pakubwa kuelewa historia ya watu wa pwani ya Afrika Mashariki. Wafanyibiashara walisaidiwa na pepo za kusini na kaskazini katika safari yao ya kuja na kuondoka pwani. Waarabu, Wahindi na Waajemi walitumia msimu wa pepo za kaskazi zilizokuwa zikianza kuvuma mwezi wa Novemba hadi mwezi wa Februari ili kufika pwani ya Afrika Mashariki. Baada ya shughuli zao za biashara kukamilika, walirudi kwao kwa usaidizi wa pepo za kusi zilizoanza baada ya pepo za kaskazi kutua. Bidhaa kama pembe za ndovu, magome ya kobe, dhahabu, watumwa, rangi za nguo na manukato zilinunuliwa na wageni waliofika pwani ya Afrika Mashariki kwa shughuli za biashara. Waswahili nao walinunua majora ya vitambaa, vyungu, shanga za vioo, vitara, vyombo

vya vioo vya nyumbani, mvinyo, shaba na ngano kutoka kwa wageni waliofika pwani ya Afrika Mashariki.

Biashara ilipozidi kushamiri, vijiji vilianza kupanuka na kuwa miji. Miji hiyo ilikuwa Mogadishu, Lamu, Mombasa, Pemba, Ugunja, Malindi, Barawa, Kilwa, Gedi, Pate kati ya mingine. Baadhi ya wageni walikuja na aila yao na kustakimu katika eneo la pwani. Allen (1993:7) anadai kuwa Waajemi na Waarabu ndio waliokuwa waasisi wa ustaarabu wa eneo hilo. Walikuwa wakitumia pepo za misimu katika Bahari Hindi kufika pwani ya Afrika Mashariki. Mbali na biashara, Waarabu waliwachukulia Waswahili kuwa marafiki kwa sababu ya imani zao asilia kama imani katika mapango, sayari za anga za juu, nyota, jua na mwezi. Kwa sababu hiyo, walisambaza dini ya Kiislamu. Dini hii ilikuja na athari zake katika sehemu hizo ambapo hadi sasa baadhi ya watu hawawezi kubainisha kati ya Uislamu na Uswahili.

Katika vipindi mbalimbali vya kihistoria, jamii ya Waswahili imekuwa na misukosuko ya kila nui pamoja na mafarakano yaliyosababisha vita kati ya jamii za Waswahili wenyewe. Vita hivi vilileta uharibifu wa mali na hata vifo. Vilevile, mashambulizi ya mara kwa mara kutoka kwa majirani zao kama vile, Wasanye, Walangulo, Wadahalo, Wagalla na Wasegeju yalikithiri. Mitafaruku hii ilitokea baina ya karne ya kumi na mbili na karne ya kumi na tano ambapo Waswahili walikuwa na taabu na maisha yao kuvurugika kiasi cha kumtaka mtu wa kuwaongoza na kuwaunganisha. Ni kutokana na hali hii basi ambapo jagina Fumo Liyongo alizuka ili kuikomboa jamii yake.

## 2.5. **Misukosuko ya Kivita iliyomzua Fumo Liyongo**

Kama tulivyodokeza hapo awali, jagina hazuki katika ombwe tupu, huzuka kwa sababu ya kutaka kuikomboa jamii kutokana ya tatizo fulani. Jamii ya Waswahili ilipitia misukosuko ya

kila nui na kusababisha kuzuka kwa Fumo Liyongo. Gichamba (2005) akirejelea Prins (1958:27-29) anasema kuwa maelezo kuhusu misukosuko hii katika vipindi mbalimbali yamefafanuliwa katika tarihi mbalimbali kama vile: Tarihi ya Pate, Tarihi ya Kilwa, Tarihi ya Lamu, Tarihi ya Mombasa na Tarihi ya Vumba.

Biashara ya watumwa iliyoendelezwa na Waarabu ilisababisha matatizo katika jamii za bara pamoja na za pwani. Biashara hii iliendelezwa kwa karne nyingi katika eneo hili. Waarabu walitumia nguvu kuwashika na kuwateka Waafrika na kuwasafirisha hadi eneo la Mashariki ya kati na sehemu nyingine ulimwenguni. Walifanya hivi kwa kushirikiana na baadhi ya Waafrika. Watumwa hawa walifungwa kwa kamba na minyororo shingoni na kusafirishwa hadi mazingira yenye hatari mno. Waliposafirishwa, walitwikwa baadhi ya bidhaa kutoka pwani. Nyumba zao ziliteketezwa na watoto wao kuuawa. Baadhi ya mateka hawa walifia njiani. Waliokuwa hawajiwezi kwa sababu ya uchovu na magonjwa walitumbukizwa baharini wakiwa wamefungwa kwa minyororo. Utekaji wa watumwa ulizua vita vya mara kwa mara baina ya Waarabu na wenyeji wa pwani ya Afrika Mashariki, wakiwemo Waswahili.

Jamii mbalimbali za Waswahili ziliendelea kupigana vita. Wafalme wa dola mbalimbali wakajizatiti kuimarisha utawala wao. Kwa mfano katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* tunaelezwa kuwa Daudi Mringwari alihofia Fumo Liyongo angenyakua utawala wake hivyo basi akapanga njama ya kumwangamiza Fumo Liyongo:

Fitina zikamngiya
mfalme miya miya
wa hila hakusudiya
kumuuwa fahamiye**(ubeti wa 49)**

Na Sulutwani niseme
alikucha mwanamume
tampoka ufalume
dhana alimdhaniya **(ubeti wa 51)**

Hali kadhalika, dola mbalimbali zilipigana vita ili kuonyesha umahiri wao katika uchezaji ngoma. Sutton (1966:18-19) akirejelewa na Achieng' (2012) anaeleza kuwa kati ya miaka 1200 na 1500 baada ya Kristo kulikuwapo na mitafaruku, ugomvi na mashambulizi baina ya dola mbalimbali. Masultani wa awali wa Kilwa walikuwa na matatizo na majirani wao. Anadai kuwa Tarihi ya Pate inaeleza kuhusu mapigano, uporaji na mapinduzi katika visiwa vya Bajuni, umwagikaji wa damu na uharibifu wa mali katika kisiwa cha Pate. Aidha, Malindi ilizozana na Mombasa hadi Wareno walipoingilia kati kwa kutumia bunduki. Inadaiwa kuwa kufifia kiuchumi na kisiasa kwa mji wa Kilwa mwanzoni mwa karne ya kumi na nne kulisadifu kuinuka kiuchumi kwa mji wa Pate. Kwa mujibu wa Tarihi ya Pate, kuinuka huku kwa mji wa Pate kulisababisha utekaji katika maeneo mbalimbali ya pwani kutoka Mogadishu hadi katika visiwa vya Kirimba vilivyo pande za kusini.

Majirani wa Waswahili vile vile walikuwa tishio kwa usalama na utangamano wa Waswahili tulivyotaja awali. Mashambulizi haya hayakutekelezwa dhidi ya Waswahili pekee ila pia kwa Wapokomo, Wasegeju na makundi mengine ya Wamijikenda. Baada ya Wagalla kuwatimua Waswahili kutoka Shungwaya, waliwafuata hadi sehemu za kusini na kuzidisha mashabulizi yao. Werner (1915:238) anatoa mfano wa Wasegeju na Wakauma waliotoroka makao yao ili kuwahepa Wagalla waliokuwa wakatili na wenye nguvu za kivita. Anasema kuwa baadhi ya Wapokomo walitekwa na Wagalla na kufanywa watumwa wao. Tamaduni za Wapokomo hata hivyo zinaeleza kuwa, Wapokomo wengine walijificha mashimoni karibu na fuo za mito kisha Wagalla waliokuja kulisha mifugo walifumwa kwa mishale ya sumu. Hatimaye, Wagalla walitorokea sehemu za chini za mito. Wapokomo nao wakawafuata usiku ulipoingia kwa kutumia mitumbwi midogomidogo na kuwaua. Baada ya mauaji, walificha mitumbwi yao chini ya mto kwenye mchanga.

Katika tamaduni za Wamijikenda na Waswahili, inadaiwa kuwa nyumba zao za awali ziliezekwa kwa nyasi kwenye paa na hata kwenye pande zake. Hali hii iliwawia rahisi Wagalla kuwafuma mikuki kutoka nje walipokuwa wamelala. Allen (1993:218) anasema kuwa kuna hadithi kuhusu *kaya* ya hapo awali ya Wagiriama kwa jina *Kaya Murikwa* iliyokuwa na nyumba za aina hiyo ambayo ilishambuliwa kikatili na Wagallla na hatimaye ikabadilishwa jina na kuitwa *Kaya Mwijo.* Wagalla walishambulia majirani zao kwa sababu ya fahari yao tu na vilevile kutwaa miguo wao.

Misukosuko hii ya kivita iliyotokea katika sehemu za pwani ilivuruga Waswahili na jamii nyingine za maeneo hayo ya pwani. Hawakuwa na mtu wa kuwaongoza ama kuwatetea didhi ya mashumbulizi hayo kutoka kwa maadui wao. Aidha, pakawa na haja ya kiongozi wa kuwaunganisha pamoja kama jamii moja. Ni katika hali hii ya misukosuko katika jamii ya Waswahili na jamii nyingine za pwani ambapo Fumo Liyongo, shujaa wa Waswahili alizuka. Fumo Liyongo hakuwa tu shujaa wa Waswahili bali Wapokomo, Wasegeju na jamii nyingine za pwani wanamtambua Fumo Liyongo kama shujaa wao hata katika tamaduni zao.

### 2.5.1. **Historia ya Fumo Liyongo**

Fumo Liyongo ni shujaa anayesifika sana katika jamii ya Waswahili na Wapokomo katika pwani ya Kenya. Kipindi alichoishi shujaa huyu hakijulikani kwa usahihi ingawa kuna madai kuwa aliishi baina ya 1160 – 1204. Hata hivyo wachunguzi wengine wanasema Fumo Liyongo aliaga dunia mnamo mwaka wa 1580. Katika fasihi simulizi ya Waswahili kuna maelezo yanaeleza kuwa Fumo Liyongo alizaliwa Siu ilhali mengine yanasema kuwa alizaliwa sehemu inayojulikana kama Shaka karibu na mji wa Kipini ulioko Pwani ya Kenya. Katika masimulizi ya Wapokomo, yanasema kwamba Liyongo alikuwa mtu wa Witu, mfalme wa Witu (Nurse 1995:42).

Masimulizi mengine yanaeleza kuwa Liyongo alizaliwa katika kasri la kifalme, akakua na kuwa kijana mwenye nguvu nyingi na akapewa kipawa cha usemi. Mamake alimpenda sana na kumtunza;[2]

Mama kamtunda sana
kimuona toa hana
sana walikipendana
wakipana farajiya

Maelezo mengine yanadai kuwa Fumo Liyongo alikuwa mtoto wa mfalme lakini mamake alikuwa suria, kwa hivyo Fumo Liyongo hakuhesabiwa kama mtoto halisi wa mfalme. Mfalme alipoaga dunia, Fumo Liyongo hakumrithi licha ya umri wake[3]. Kwa sababu hii, ulizuka mvutano mkubwa kati ya Fumo na ndugu yake anayetajwa kama Daudi Mringwari. Mvutano huu uliishia kusababisha Fumo Liyongo atoroke Pate na kuhamia bara alikoishi na Wasanye. Liyongo alipata sifa nyingi miongoni mwa watu alioishi nao. Wakati huu wote mfalme alitaka kufanya hila ya kumshika na kumfunga Fumo Liyongo. Alimwona kama tishio kwa ufalme wake. Wakati mmoja mfalme alipomwagiza kwenda Pate ili aonekane na Wagalla, Fumo Liyongo alitii. Alipofika huko Wagalla, waliokuwa watu warefu sana, walishangaa kutokana na ukubwa wake. Waliamua kufanya mpango naye ili amwoe msichana wa Kigalla. Liyongo alikubali. Lakini alipokuwa huko, alidhania kuwa mfalme alikuwa na nia mbaya naye ivyo akatorekea bara tena. Mfalme aliamua kufanya njama na Wasanye ili wamkamate au hata kumwua Fumo Liyongo.[4]

Wasanye walijaribu kila njia lakini wakashindwa. Fumo Liyongo alikuwa na uwezo mkubwa sana. Siku moja waliamua kumshirikisha kwenye kikoa – kikundi cha kula pamoja. Walipanga kuwa kila mmoja wao atakuwa akipanda mkoma na kuyatunda makoma ili wale na wengine

wafaidi. Walifanya hivi kwa zamu. Liyongo alishirikiana nao. Ilipofika zamu yake, Fumo Liyongo aliwaambia Wasanye wautafute mkoma waliotaka. Waliutafuta ule mrefu na kumwambia Liyongo, “huu hapa tumeupata!” Liyongo alipouangalia aliona ni mrefu mno, akaijua nia yao. Badala ya kuupanda ule mkoma, alitia mishale yake kwenye uta wake na kutungua ngaa nzima ya makoma, wakala wakashiba. Wasanye walishindwa la kufanya. Walimwendea mfalme na kumweleza kuwa haikuwa rahisi kupambana na Fumo Liyongo. Mfalme aliposikia hivyo aliwashauri wakamweleze Fumo Liyongo kuwa kulikuwa na mchezo wa gungu (aina ya ngoma) mjini na hapakuwa na hatari yoyote ile. Kwa kuwa Fumo Liyongo alikuwa mpenzi mkubwa wa gungu na mwao, aliamua kujiunga nao. Mfalme aliposikia hayo, alifanya mpango mzuri na baada ya Liyongo kuwasili mjini tu, akashikwa na jeshi kubwa la askari na kutiwa kizuizini[5].

Huko kifungoni alikokuwa, Fumo Liyongo alifungwa kwa pingu na minyororo na askari wakatiwa mlangoni kumzuia asitoroke. Kila siku mamake alikuwa anamtayarishia chakula na kumpa kijakazi wao aliyeitwa Saada kumpelekea. Kila mara askari hao walipokiona kile chakula kizuri walikichukua na kukila. Basi siku moja Fumo Liyongo aliamua kumtuma kijakazi Saada kwa mamake kwa ujumbe uliojaa mafumbo. Ulikuwa ujumbe wa kishairi, kwamba wampikie mkate wa wishwa na kutia tupa ndani. Alitaka aitumie tupa hiyo kuikata minyororo iliyomfunga pamoja na pingu zake na kuondoka gerezani. Utungo huo ulikwenda hivi:

> Kijakazi Saada nakutuma tumwa tumika
> Kamwambie mama ni miunga hayalimuka
> Afanye mkate pale kati tupa kaweka
> Nikereze pingu na minyoo ikinemuka
> Niparage kuta na madari kiyakiuka
> Niuwe rijali pindi wakiwana nami hateka

Ningie ondoni ninyepee ja mwana nyoka
Niingie mwituni ningurumie ja simba buka
Nali mtu pweke nimeziye katika nyika
Si nduu si mbasi nimeziye katika nyika
Nduu ali mama awasiwe kinda....

Mamake Liyongo alifanya kama alivyotaka Fumo Liyongo. Alitayarisha mikate kadha mizuri na mmoja mkubwa wa wishwa. Wale askari walipoiona ile mikate mizuri waliichukua na kuila na kumwambia kijakazi Saada aingie ndani na kumpelekea ule mkate mbaya wa wishwa. Saada alifanya hivyo alivyoagizwa. Fumo Liyongo alipouona ule mkate alifurahi sana. Mfalme na wasaidizi wake walikuwa wameamua tayari kuwa watamwua Fumo Liyongo. Naye aliomba iandaliwe sherehe ya gungu kabla ya kuuliwa kwake. Watu walikusanyika nje ya gereza alikofungwa Fumo Liyongo kwa ajili ya gungu hiyo. Huku ndani Fumo Liyongo alikuwa akiimba nyimbo nzuri za kuwatumbuiza waliokuwa huko nje. Wakati anaimba alikuwa akizikata zile pingu zilizomfunga pamoja na minyororo yake. Fumo Liyongo aliimba nyimbo za kila aina. Huu hapa ni mfano wake.

Mringwari taikha fuwanye njooni hwitwa na Fumo Liyongo
Hwitwa na Liyongo Fumo na nduguye shaha Mwengo
Mukaketi juu ya ulilye wakusanye watenzi wa ringo
Wakusanye watenzi hiari wajuao kutunga zifungo
Wajuo kufuasa zina na kucheza kwa kumia shingo
Hwitwa hima inukani mwende watukufu wana wa zitengo
Pindi sizo watu wasijakaa ukumbini kikawa kisongo.
(Kutoka *Utumbuizo wa Gungu*)

Baada ya kipindi kifupi, Fumo Liyongo alifanikiwa kuzikata zile pingu. Alitoka nje kwa kishindo kikubwa huku akiwaua wale askari waliokuwa mlangoni kwa kuvigonganisha vichwa vyao pamoja. Fumo Liyongo alitorokea bara akaenda kuishi karibu na mto Ozi sio mbali na

Shaka alikozaliwa. Aliishi huko na mkewe wa Kigalla aliyejulikana kama Kundazi. Mwanamke huyu alikuwa na mtoto wa kiume, Fumo Liyongo alimpenda na kumtunza kijana huyo.

Mfalme naye alikuwa bado na nia ya kumwua Fumo Liyongo. Aliagiza mwanawe Fumo Liyongo aje ili amtumie kujua siri ya kinachoweza kumwua babake[6]. Alimwahidi mwanawe Liyongo kuwa atamwoza binti yake ikiwa atafanikiwa kulitekeleza alilotaka. Yule "Mwana wa Kigalla" alifanikiwa kuijua siri baada ya kwenda kwa babake kumuuliza kile kinachoweza kumwua. Fumo Liyongo alitambua kuwa kijana huyo alikuwa amezainiwa au kushawishiwa vibaya na maadui zake lakini alimwelezea siri yenyewe. Alisema kuwa asingeweza kufa ila kwa sindano ya shaba ikidungwa kwenye kitovu chake. Mfalme aliposikia habari hizo alifurahi sana. Basi mfalme aliwatafuta wahunzi wazuri wakatengeneza sindano ya shaba[7]. Yule mwanawe Liyongo alipewa ile sindano ya shaba aende kumwua babake.

Siku moja Fumo Liyongo alipokuwa amelala, yule mwanawe alimwendea na kumchoma kwa nguvu zake zote kitovuni. Fumo Liyongo aliamka kwa kishindo kikubwa; alitoa ukelele mzito wa uchungu ambao ulisikika Shaka nzima (inadaiwa kuwa hata leo mwangwi wa sauti ya kilio hicho husikika usiku hasa majira ya mvua kuu). Fumo Liyongo alitimua mbio kuelekea palipokuwa kisima cha mjini na kupiga goti huku ametia mshale wake kwenye uta wake. Watu walishindwa kumwendea kwa kuogopa kuwa alikuwa amekasirika. Maji yalipoisha mjini walitaabika sana mpaka hatimaye wakashauriana kumtafuta mamake Liyongo. Mamake Liyongo alimwendea huku akimwimbia tumbuizo nzuri za kumliwaza. Lakini Fumo Liyongo alibaki katika hali ileile. Alimsogelea polepole hadi alimfikia na kumgusa naye akaanguka mfu. Huzuni kubwa iliwashika watu wote. Walimchukua Fumo Liyongo na kwenda kumzika. Yule mwanawe Liyongo hakupata ule ufalme aliokuwa ameahidiwa. Watu walimchukia sana naye kwa masikitiko makubwa akatorokea msituni alikofia.

## 2.6. **Historia ya Wakisii**

Kwenye sehemu hii tunajadili kuhusu jamii ya Abagusii anamotoka Sakawa. Maelezo kuhusu eneo wanamoishi, shughuli zao za kila siku pamoja na historia yao ni baadhi ya mambo ambayo tumeyashughulikia.

Wakisii wanaojiita Abagusii[8] ni Wabantu wanaoishi sehemu kubwa ya Kusini Magharibi mwa nyanda za juu mwa Kenya. Kati yao na ziwa Viktoria ni Wajaluo ambao ni wanailoti. Mashariki na kusini mashariki wamepakana na Wakipsigis na Wamasai. Kusini, japo wametengwa na Wajaluo, wana uhusiano wa karibu na Wakuria[9]. Hii ni jamii ya Wabantu wa Magharibi mwa Kenya waishio magatuzi ya Kisii na Nyamira. Hata hivyo hii haina maana kwamba hakuna Wakisii kwenye magatuzi mengineyo au hata kwenye mataifa mengine. Tunalosema ni kwamba hapa ndipo pahali panapohusishwa nao baada ya wao kuyafanya maskini yao na kuacha kuhama tena.

Wanakoishi sasa Wakisii wamepakana na makabila ambayo kimbari ni tofauti nao. Magharibi na kaskazini magharibi ni Wajaluo, kusini na kusini mashariki ni Wamasai na mashariki na kaskazini mashariki ni Wakipsigis ambao wote ni wanailoti. Kwa sababu ya rutuba katika sehemu wanakoishi Wakisii, wanashiriki katika ufugaji wa wanyama na ukulima. Hivi sasa ni wakulima wa kahawa, chai, pareto, mahindi na ndizi kati ya mazao mengine. Pia wanaendeleza ufugaji wa wanyama mbalimbali kama vile ng'ombe, kondoo na mbuzi.

Katika tamaduni za Wakisii, kuna madai kuwa hapo awali, walikuwa wa asili moja na Wakuria, Logoli, Wasuba, Wabukusu, Wakikuyu, Wameru, Waembu na Wakamba. Isitoshe, tamaduni hizi zinaendelea kusema kuwa wakielekea kusini kutoka nchi wanayoitambua kama 'Misiri'[10] walikuwa pamoja na Ganda na Songa. Waganda na Wasonga inasemekana walijitenga na

wenzao katika mlima Elgon wakaelekea kusini magharibi. Wakikuyu, Wameru, Waembu na Wakamba nao wakasafiri kuelekea mashariki kunakojulikana sasa kama nyanda za kati mwa Kenya na Wabukusu wakabaki mlima Elgon. Waliosalia katika kundi hili ni Wakisii, Wakuria, Wasuba na Logoli. Walielekea sehemu ya kusini na kufuata kingo za mto Nzoia wakafika fuo za mashariki mwa ziwa Victoria takriban vizazi kumi na vitano hadi kumi na sita vilivyopita, inavyochukuliwa kuwa 1560 BK.

Kuelekea mashariki walisafiri kwenye kingo za ziwa na kujenga makazi sehemu ya Goye iliyoko eneo la Yimbo[11]. Kutoka Goye, makazi yao yalienea hadi kunakojulikana sasa kama Urima, Ulowa, Sare na Ramogi. Ni katika sehemu hizi ambapo wahamiaji wa kwanza wa Wajaluo waliwapata.

Wakisii wanamtaja Mogusii kama mwanzilishi (babu) wa jamii yao na ambaye kabila lao limepata jina kutokana na jina lake. Babake Mogusii aliitwa Osogo, mwanawe Moluguhia, mwanawe Kigoma, mwanawe Rebiaka aliyekuwa mwanawe Kintu. Kintu kwa mujibu wa Ochieng (1971) ndiye aliyewaongoza kuhama kutoka Misiri hadi mlima Elgon ambapo waliishi hadi vizazi vinne kabla ya kutengana. Lakini uchunguzi wa Were na Nyamwaya (1086) unadai kwamba Kintu aliongoza magurio haya kutoka Kongo wala si Misiri. Tamaduni za jamii ya Wakisii pia zinadai kwamba Moluguhia babu yake Mogusii alikuwa na watoto ambao ndio waanzilishi wa makabila ya Waluhya. Kati yao ni Osogo na Mogikoyo. Vizazi vya Osogo ni Wakisii, Wakuria, Logoli na Wasuba na vizazi vya Mogikoyo ni pomoja na Wakikuyu, Wameru, Waembu na Wakamba.

Wakisii wanaaminiwa kuhama pamoja na makundi mengine ya Wabatu kutoka Kongo (Akama na Maxon 2006). Waliwahi kutangamana na jamii mbalimbali tangu Kongo hadi wanakoishi

sasa. Jamii walizotangamana nazo ni pamoja na: Wasudani, Wakushaiti wa Kusini na Wasaheli wa mashariki. Huenda Abagusii walichukua baadhi ya mila na tamaduni za jamii hizi. Kwa mfano, Wasaheli ni mababu wa Waswahili anamotoka Fumo Liyongo. Hii ina maana kwamba upo uhusiano wa aina fulani kati ya mashujaa wa hizi jamii mbili, jambo lililotuchochea kuwatafitia.

Babu wa Mogusii anasemekana kuwa Kintu (ama Muntu, Mundu au Wantu) aliyeongoza Wabantu kughura eneo la Kongo. Inasemekana kwamba Abagusii waliingia Kenya kutoka Uganda hadi mlima Elgon wakaelekea Kisumu miaka mia tano hamsini hivi iliyopita. Walihama kwa sababu mbalimbali kama vile kiangazi au mzozo baina yao na Wakipsigis. Kwenye safari yao wakihama, walifika kwenye kingo za ziwa Viktoria wakafanya sehemu hii kuwa makao yao kwa vizazi viwili ambako mfumo wao wa sasa wa koo ulianza kuchipukia. Koo nne zilizoanza kujitokeza ni Basi, Girango, Sweta na Wanjare (Were na Nyamwaya, 1986). Baadaye kukachipuka koo mbalimbali za Omogetutu, Omogirango (Maate na Rogoro), Omomachoge, Omonchari, Omobasi (Abaitangare na Abasansa), Omonyaribari (Chache na Masaba), Omogusero na Omosweta/ Basweta. Walipovamiwa na majirani zao Wakipsigis walihama eneo hilo hadi makao yao ya sasa.

Wajaluo na Wakisii walitengana kwa sababu ya msongamano wa watu, ukame na majanga mengine. Kutoka Yimbo, Wakisii walihamia Kisumu walikokaa kwa muda. Wakiwa Kisumu, mamake Mogusii alianga dunia. Inakisiwa kuwa Mogusii naye aliaga dunia katika eneo hili kwani walipogura kutoka Kisumu, waliogozwa na wazee wa koo mbalimbali. Ni katika sehemu hii ya Kisumu pia ambapo Wakisii walitengana na Logoli. Ukame ulipoathiri Kisumu, Wakisii walihama ili kufafuta chakula na makazi mapya. Waliosalia Kisumu ndio wanaoaminika kuwa

mababu wa kabila la Avalogoli[12]. Baadaye, Avalogoli walihamia sehemu za kaskazini na wakaweka makao yao kati ya miji ya Kisumu na Kakamega.

Katika kipindi hicho Wakisii waliweka makao yao kule Kano. Eneo hili lilikuwa na malisho ya kutosha kwa mifugo wao na huenda walikuwa wamechoka kuhamahama. Haya yaliwachochea kuishi eneo la Kano kwa miaka mia moja hivi (Ochieng 1971). Kano ni sehemu muhimu katika utamaduni wa Abagusii kwani hapa ndipo koo mbalimbali za Abagusii zilizuka. Aidha, vizimu (*totems*) vya koo hizi viliamuliwa. Kwa mfano, ukoo wa Abagirango walichagua chui, Ababasi wakachagua punda milia, Abanchari kiboko na Abasweta wakachagua nyani.

Huenda wingi wa Wajaluo na unyakuzi wa mifugo ulisababisha Wakisii kugura Kano. Aidha, walivamiwa na Wanandi kutoka sehemu ya kaskazini. Kutoka Kano, walihamia sehemu iitwaayo Kabianga iliyoko gatuzi la Kericho. Kila ukoo uliongozwa na wazee wao. Hapa, Wakisii walikumbwa na majanga ya kila nui, kama vile magonjwa, njaa, ukame uliofanya mifugo wao kufa na hata kuathiri kilimo. Haya yalisababisha kugura kwao kutoka sehemu hii. Sehemu hii (Kabianga) waliipa jina hili la kimajazi kumaanisha 'vimekataa'. Jina hili ndilo litumikalo hadi sasa. Aidha, uvamizi wa mara kwa mara kutoka kwa Wamasai na Wakipsigis uliwalazimisha Wakisii kughura Kabianga. Waliweka makazi yao Nyangarora. Wamasai waliendelea na uvamizi wao lakini Wakisii wakaamua kutohama tena. Waliweka makazi ya kudumu Nyagoe, Manga na Isecha.

Makazi haya kulingana na tamaduni zao ndiyo yalikuwa ya kwanza kwa jamii ya Wakisii kukaa katika sehemu inayokaliwa na Wakisii sasa. Ni kutoka hapa ndipo koo za Abagusii walijipanga na kutawanyika kwenda sehemu nyingine za nyanda za juu za magharibi mwa Kenya. Kuna

makundi manne makuu ya Abagusii; Abasweta ambao ni kizazi cha Mosweta, Abagirango kizazi cha Mochorwa, Ababasi kizazi cha Mobasi na Abanchari ambao ni kizazi cha Monchari.

Kwa kugundua kwamba Wakisii ni jamii iliyorahisi kuvamiwa, Wakipsigis hawakuwaacha hata baada ya kuwafurusha maeneo ya Goye na Kano. Walizidi kuwavamia kila mara wakiiiba mifugo wao na kuwaua vijana wao. Hali iliendelea hivi hadi mwaka 1892. Wasemavyo Were na Nyamwaya (1986), vita vya mwaka huo, maarufu kwa jina vita vya Saosao, ndivyo vilivyomnasua Mkisii kutoka kuvamiwa kila mara na maadui wake majirani. Anavyoeleza Ochieng (1971), Sakawa alichangia mno kuwapatia Abagusii ushindi kwenye vita hivi kwa kuwapatia maarifa ya namna ya kumwekea adui wao wa miaka mingi mtego. Waliwaacha Wakipsigis wakaenda kuivamia jamii ya Waluo ambako walijipatia mifugo wengi hata wakasahau kwamba upo uwezekano wa kuvamiwa na Wakisii. Walipokuwa wakirudi, Wakisii waliwasubiri kwenye kingo za mto Characharani ambako waliwaua wote waliokuwa wameivamia jamii ya Waluo. Tangu hapo jina la Sakawa likaenea kwenye koo zote nane za Wakisii.

Viongozi wa Wakisii walikubaliana kwamba palikuwa na haja ya kuwa na mkutano wa viongozi pamoja na vijana wa vita. Mkutano wenyewe uliongozwa na Sakawa. Mkutano ulifanyika Manga ambako walikubaliana kwamba wanafaa kuungana katika vita ili kuwashinda adui zao Wakipsigis.

Baina ya 1889 na 1892, kulijitokeza ugonjwa wa sotoka uliowaua mifugo wengi hivi kwamba Wakipsigis baada ya kupoteza mifugo waliamua kuvamia majirani wao Waluo na Wakisii kujiongezea mifugo zaidi. Kwa kuwa walikuwa mashujaa wa vita kwenye vamizi za awali, walizivamia jamii za Wakisii na Waluo bila kukisia kwamba mambo huenda yakabadilika. Kwa

kutarajia ushindi kama kawaida waliingia na kuwavamia Wakisii walikojitwalia mifugo na vyakula kochokocho wakiongozwa na Malabun arap Makiche wa Sotik. Walipofika Bureti, jeshi la Chesengeny arap Kaborok lilijiunga nao kisha wengine kutoka Belgut. Jeshi la Wakipsigis lilikuwa kubwa mno. Walipoingia kwa Wakisii walikaribishwa na kundi la tai. Hii ilikuwa ishara ya bahati mbaya. Juhudi za Chesengeny kuwashawishi kufutilia mbali uvamizi huo hazikufua dafu. Malabun na wenzake hawakusikia lolote. Waliteka mifugo sehemu za Mugirango na Kitutu. Punde tu kukaibuka mzozo baina ya viongozi wao hali iliyofanya baadhi ya wanajeshi kurudi kwao.

Wakipsigis walipokuwa wanawavamia Girango na Kitutu, Wakisii walitumiana ujumbe kukutana ili kumkabili adui wao. Baada ya kupashana habari walienda hadi mto Charachani kuwasubiri Wakipsigis kurudi kutoka kwa Waluo. Hapa ndipo waliwaua Wakipsigis wengi ambao hawakutarajia kuvamiwa kwa vyovyote na Wakisii. Mbele yao walikuwa Wakisii na nyuma ni Waluo. Hii ilikuwa na maana kwamba hawakuwa na mwanya wowote wa kujiokoa. Ushindi wa Wakisii ulisifiwa wakiimba kuhusu hivyo vita vya Saosao.

Kutokana na nafasi aliyokuwa nayo Sakawa katika maswala mengi kwa jamii ya Abagusii, ni muhimu kuishughulikia historia ya kiongozi huyu kwa kina. Kwenye sehemu inayofuatia tumemshughulikia shujaa Sakawa.

### 2.7. **Mikakati iliyomzua Sakawa**

Hadi hapa mjadala wetu kuwahusu Wakisii umeonyesha kwamba walikuwa wakisongwa na tatizo la vita na majirani zao kila mara. Isitoshe, mivutano ya kivita kati yao wenyewe lilikuwa jambo la kawaida. Wizi wa mifugo na kung’ang’ania mipaka ndizo zilikuwa sababu za vita hivi. Majirani waliowavamia ni Wajaluo, Wakipsigis na Wamasai kutoka pande zote walikojenga

makazi yao. Vita kati ya Wakisii na maadui zao vilivyokuwa vya kufa kupona ni vile vya Kenyerere. Vita hivi vilikuwa kati ya mojawapo ya ukoo wa Ababasi na Wakipsigis na vile vya Ntomocha kati ya Abagirango na Wamasai (Ochieng 1971). Japo walipata ushindi huu, matatizo yao hayakwisha na majirani wao. Hata mizozo ya wenyewe kwa wenyewe haikwisha. Hivyo walihitaji mkombozi atakayeleta amani ya kudumu. Wakati huu ndipo Sakawa alipozaliwa. Aliunganisha jamii ya Wakisii kama tutakavyoona na kusaidia katika ushindi wa vita vya Saosao.

Vita vilivyosababisha Wakipsigis kuacha kuwavamia Wakisii ni vile vya Saosao[13] vya mwaka 1892. Abagirago walivumilia uvamizi wa mara kwa mara mpaka waliposhauriwa na viongozi wao kuungana na wenzao ili kuwapiga vita Wakipsigis. Vita hivi vilisababisha vifo vingi vya Wakipsigis ambapo maji ya Mto Saosao na Charachani yalibadili rangi na kuwa mekundu kutokana na damu ya Wakipsigis waliouawa. Nyimbo zilitungwa kusifu Wakisii kwa ushindi wao na vilevile viongozi wao kwa ushauri wao.

### 2.7.1. **Historia ya Sakawa**

Sakawa, inadaiwa kwamba alizaliwa mwaka 1840, na alipotea kiajabu mwaka 1902. Alizaliwa kama mtoto wa pekee wa kiume wa Mzee Nyakembugumbugu baada ya babake kutaka kupata mtoto wa kiume atakayemrithi. Ni mzawa wa ukoo wa Abageka wanaoishi eneo la Mosocho kaunti ndogo ya Kisii ya Kati. Ajabu ni kwamba alizaliwa akiwa amemea meno tayari. Hili ndilo liliwachochea wanakijiji wengi kuja kumwona huyu mwana wa ajabu. Ilivyo katika jamii ya Abagusii, mtoto wa aina hii alifaa kuuwawa kwa kuwa hii ilikuwa ishara ya mkosi. Hata hivyo, Sakawa hakukosa watetezi wake waliodai kwamba hili liliashiria kwamba angekuwa mashuhuri katika jamii. Isitoshe, babake hangekubali kuuwawa kwake kwa kuwa alihitaji mrithi wa mali yake.

Kutokana na mapenzi aliyokuwa nayo kwa mwanake, babake alimfundisha Sakawa fani ya uganga mapema. Hili halikumpa Sakawa nafasi ya kutangamana na wanarika wenzake. Pengine ni kwa sababu babake hakutaka mahasidi wake waliotaka auwawe pindi tu alipozaliwa kwa kuwa alikuwa ameota meno alipozaliwa.

Kutokana na kuwa na akili pevu, Sakawa katika ujana wake alipewa kibali cha kushiriki vikao vya wazee, kinyume na vijana wengine wa umri wake. Sakawa alipenda kuuliza kila jambo ili kulielewa kwa kina. Kipawa chake cha kutabiri kiliwafaa mno wazee hawa. Alionya kwamba baadhi ya vijana wa umri wake, hasa baada ya kizazi chake wangeasi utamaduni wao na kuiga tamaduni za kigeni.

Sakawa alikuwa mtu mwenye hekima na aliyependa kukuli ili kulielewa jambo kwa kina kabla ya kutangamana nalo. Isitoshe alijitolea kwa bidii katika jambo lolote alilolifanya. Sifa hizi zilimfanya kuteuliwa kama mshauri mkuu wa jamii ya Abagusii. Aliwapa ushauri wanajamii wake kuhusu namna ya kukabiliana na adui zao hasa Waluo, Wamaasai na Wakipsigis katika vita sanasana vita vya Saosao ambapo walipata ushindi mkuu.

Uhasama kati ya Sakawa na wazee wa jamii yake ulizidishwa na sifa yake ya kupenda kusema ukweli. Kuna wakati jamii ya Abagusii ilikumbwa na ukame na njaa kuu. Ushauri wa Sakawa kuhusu hali hiyo ulikuwa ni kwamba hali hiyo ilisababishwa na wazee wenyewe kuuasi utamaduni wao kiasi cha kumkasirisha Mungu wao. Aliwaambia kwamba hawatoi kafara zao ilivyo desturi. Ukweli huu ndio ulizidisha uhasama uliokuwepo kiasi cha wazee hao kukodisha majambazi kumvamia Sakawa kwake. Kwa bahati nzuri hawakumpata kwa kuwa alikuwa amekwisha arifiwa kuhusu njama hiyo akatorokea kijiji jirani cha Mwamosioma kutafuta usalama.

Sakawa alikuwa na mazoea ya kukutana na wazee wengine eneo la Getembe akiwaeleza kuhusu utakavyokuwa mji wenyewe. Hapa ndipo alipotoa utabiri wake wa viyoga vya Getembe. Alieleza kwamba huko Getembe kutamea viyoga lakini atakeyevuna ni yule tu aliye na wavulana shupavu. Hapa alikuwa na maana kwamba watakaofaidi ni wale wenye watoto walio na bidii hasa masomoni. Viyoga vilikuwa jazanda ya pesa ambazo zitachumwa katika mji wa Kisii. Aliwaambia kutajengwa vituo vya polisi, hospitali, shule na kanisa. Aliwasha moto katika sehemu maalumu ili kuonyesha sehemu ambako milingoti ya umeme itakuwa. Isitoshe alitabiri kwamba jeshi lao litapokonywa silaha zao na mtu mweupe ikiwa Wakisii wangesusia kufuata maelekezo yake. Hata hivyo, mtu mweupe angekaa tu kwa muda kisha aondoke na kuwaacha kuendelea kujitawala kama walivyokuwa wakijitawala hapo awali.

Baadhi ya mambo aliyoyatabiri Sakawa ambayo yalitimia ni pamoja na kuvamiwa na nzige ambao wangekula mimea yao yote ya shambani hivyo kuwa na njaa kuu eneo lote. Kuhusu hili alishauri kwamba Abagusii waepuke vita vya mara kwa mara vya wenyewe kwa wenyewe ili watumie muda wao mwingi shambani ndipo wajaze maghala na vyakula. Kwa kuwa wengi walipuuza ushauri wake mwaka 1930 nzige walivamia eneo lote la Kisii hivyo kukatokea njaa kuu inayofahamika kama *nyangweso*[14] ilikuwa baina ya 1931 –1936 (rej. Bosire na Machogu 2013).

Pia, inasemekana kwamba Sakawa alipotabiri kuhusu mji wa Kisii, alijenga nyumba kadha huko. Ndani ya hizo nyumba kulisikika jogoo wakiwika. Watu walipoingia kuwaona hao jogoo hawakuweza kuwaona. Hapa alilolenga Sakawa ni kwamba kwa muda mrefu nchi yake itaongozwa na chama cha jogoo. Watakaoingia kwenye hicho chama kwa lengo la kutaka kuongoza hawatapata huo uongozi. Tabia ya watu kuingia tu kuwaona jogoo waliowika ndani ya nyumba, ilimkera Sakawa akaziteketeza hizo nyumba na kujenga nyumba zingine mpya mahali

kwingine. Alitaka watu watumie busara yao na washiriki katika kuijenga jamii yao wala si kutaka tu kushuhudia yanayoendelea (Ochoi 2013).

Alipenda kuwahusisha wanajamii katika mambo yote aliyoyafanya yaliyohusu mustakabali wa jamii yake. Siku moja aliwashurutisha watu wa kila eneo la Wakisii kuleta panya wawili. Panya walipoletwa, aliwatumbukiza ndani ya chungu cha maji moto. Panya waliofariki aliwatumia kutengeneza hirizi aliyoitumia katika vita vya Saosao ambavyo ndivyo vita vya kwanza Wakisii walipata ushindi mkubwa dhidi ya maadui wao wa jadi, Wakipsigis. Panya huhusishwa na udhaifu pamoja na kifo (Cirlot, 1971). Kwa kuwachoma panya, Sakawa alilenga kuwafundisha wanajamii kwamba, ili kupatikana ushindi wowote ule, pana haja kuwaadhibu waasi na maadui wa jamii yake[15].

Unavyodhihirika, utabiri wake ulijaa mafumbo ambayo yalihitaji akili pevu ili kuelewa ujumbe alikokuwa akiupitisha. Kwa mfano, aliwaeleza wanajamii kwamba kutakuja mgeni katika nchi yao, huku ameyafunga maneno kwenye jani akiyatuma nje kumwakilisha. Hapa alimaanisha kwamba mzungu ataleta mfumo wa kutuma barua iliyomo ndani ya bahasha. Isitoshe kuhusu mjo wa barabara ambao ulibadilisha mfumo wa mawasiliano, Sakawa alisema kimafumbo kwamba boga litawanda hadi kwa jirani wao Mkipsigis hivyo kurahisisha uombanaji wa moto baina ya majirani.

Inaaminiwa alifariki usiku mmoja mwezi wa Novemba 1942. Siku iliyotangulia kifo chake, Sakawa aliwaandalia jamaa zake karamu kubwa. Inasemekana kwamba hata mifugo na hayawani kama simba walihudhiria karamu hiyo. Katika hotuba aliyoitoa Sakawa siku hiyo alisema kwamba lengo la karamu lilikuwa kuwapongeza vijana wao kwa ushindi walioupata kwenye vita vya Saosao. Alisisitiza umuhimu wa umoja na ushirikiano katika mambo yote ikiwa jamii yao

ilitaka kuendelea. Katika kikao hicho hicho alitoa utabiri wake wa mwisho wa vipepeo watakaoitwaa nchi yao. Alikuwa akiwarejelea Waingereza ambao wangeingia na kuitawala nchi yao. Sakawa alionya kwamba wasipingane nao kwa kuwa utawala wao ulikuwa wa muda tu. Lakini ilivyo ni kwamba hapakosi watu ambao hawazingatii wasia. Hii ndiyo Sababu Otenyo alijaribu kupingana na Northcote hadi akauwawa. Wakisii wengi waliuwawa kwa risasi. Baada ya hotuba ya Sakawa, wageni walifumkana.

Ajabu ni kwamba punde tu walipofika kwao walisikia mayowe kutoka kwa boma la Sakawa. Usiku ulikuwa umeingia kwa hivyo wengi hawakurudi kuthibitisha yaliyojiri. Vilio viliendelea hadi alfajiri. Ikawa wazi kwamba kwa Sakawa kumetokea jambo. Ama kweli tanzia ya Sakawa ilienea kote katika janibu za Kisii na kwa majirani zao Waluo, Wakipsigis na Wamaasai. Wengi walianza kuelekea kwake kwa maombolezi. Hata mifugo na mbwa waliingiwa na huzuni. Wengi hawakuamini kwamba Sakawa angeweza kufa. Miongoni mwao alikuwa Ombati aliyekuwa rafiki yake wa karibu. Siku hiyo hakuwa karibu kwa kuwa alikuwa ameenda safari. Alipopata habari za tanzia alifika upesi kwa boma la Sakawa. Ilitukia kwamba Sakawa amekwisha kuzikwa. Aliamrisha mwili wa Sakawa ufukuliwe ili afanyiwe mazishi yanayostahili hadhi yake katika jamii. Isitoshe kaburi alimozikwa lilikuwa dogo mno. Ajabu ni kwamba hawakuupata mwili. Baada ya kuchimba kwa muda, wafukuaji walipata kiti chake alichopenda kukikalia cha miguu mitatu. Walipoendelea kuchimba zaidi waliupata mkongojo wake. Kupatikana kwa hivi viwili kuliwapa matumaini ya kuupata mwili. Wakaendelea na shughuli ya ufukuzi. Wakapata kiko chake. La kushangaza ni kwamba walipofika mwisho wa kaburi lenyewe walipata kichwa cha fahali aliyechinjwa kwenye karamu aliyowaandalia. Ombati aliwaita majirani kuja kushuhudia kioja. Hili lilizua hofu na wasiwasi mkubwa kwa wengi. Lilikuwa tukio lililozua fikira tofauti tofauti. Baadhi yao wakasema kwamba amepaa kuelekea mbinguni. Tambiko

lilifanywa kwa mujibu wa mila za Wakisii kabla ya kuliziba kaburi lenyewe. Ama kweli wanajamii wengi walisubiri kurejea kwake mwaka 1921. Hata sasa wapo wanaosubiri marejeo ya Sakawa

### 2.8. **Hitimisho**

Kwenye sura hii tumeonyesha aina za mashujaa na sifa za kijumla ambazo hujitokeza kwa majagina. Suala la vikale pia limefafanuliwa kwa kina. Kisha tumeshughulikia kuibuka kwa majagina Sakawa na Fumo Liyongo kwa kuwahusisha na jamii wanamotoka. Mikakati iliyowazua imeangaziwa pamoja na maisha yao. Lengo letu limekuwa kuweka msingi imara wa kinadharia ambao unatuwezesha kuwalinganisha majagina Sakawa na Fumo Liyongo katika sehemu ya kijarabati ya utafiti wetu. Kwenye sura inayofuata tumeshughulikia sifa zao pamoja na matendo yao kwa kuyalinganisha.

---

[1]Tunarejelea Superman

[2] Maelezo haya tumerejelea Knappert (1983:145).

[3] Kauli hii inaungwa mkono na Bitungi Matundura katika *Mkasa wa Shujaa Liyongo (*2004*).*

[4] Jan Knappert (1983:157) anaeleza kuwa Wasanye na Wadahalo walimtunza Liyongo vyema na hawakutaka kushirikiana na sultani kumwangamiza Liyongo. Ikamlazimu sultani kulipa mahasidi wa kumwangamiza. Mawazo haya pia yanarejelewa na Bitungi Matundura katika *Mkasa wa Shujaa Liyongo.*

[5]Baadhi ya wasimulizi wa kisa hiki wanadai kuwa Fumo Liyongo alishambuliwa na Wasanye alipokuwa amekwenda haja kwa mishale na kuumizwa kisha wakamshika na kumpeleka Pate kwa mfalme

[6]Masimulizi mengine yanadai kuwa mfalme alishirikiana na Wagalla kumshawishi mwanawe Liyongo kwa sababu hawakutaka kuona sifa zake zikienea kwa kasi kama ilivyokuwa

[7]Baadhi ya masimulizi yanasema kuwa haikuwa sindano ya shaba bali kilomata, aina ya kisu cha shaba kinachotumiwa kutayarisha kili au majani ya mkoma ya kusukia

[8] Pia hujiita Mwanyagetinge.

[9] Pia huitwa Watende

[10]Kulingana na S.N Bogonko (1986) Misiri ambayo tamaduni za Wakisii wanataja si ile Misiri ya Bibilia bali ni sehemu iliyoko kaskazini mwa mlima Elgon.

[11]Yimbo ni sehemu ijulikanayo hivi sasa kama Siaya

[12] Hawa ni Wamaragoli, moja ya jamii za Waluhya

[13] Wakipsigis huvirejelea kama vita vya Mogor (Taz. Ochoi 2013)

[14] Tazama Mary Omosa, "Incorporation into the Market Economy and Food Security among the Gusii: Paradise Lost or Paradise Gained?"

[15] Katika majadiliano na mzee Maguto na Atemba, wanaeleza kuwa Sakawa alishurutisha koo mbalimbali kuleta panya. Aliwasha moto katika mji wa Getembe na kila ukoo ukarusha panya wao kwenye ule moto. Panya wawili waliruka na kutoroka. Waliochomeka walitumiwa kutengeneza hirizi ambayo baadaye Moraa aliitumia kama kinga dhidi ya watu weupe.

# SURA YA TATU

# ULINGANISHI WA SIFA ZA KISHUJAA ZA FUMO LIYONGO NA SAKAWA

## 3.0. **Utangulizi**

Katika sehemu hii, tumepambanua kiulinganishi sifa za kishujaa za Fumo Liyongo na Sakawa. Tumeonyesha jinsi sifa hizi zinavyofanana na kutofautiana. Mbali na kurejelea *Utenzi wa FumoLiyongo*, tumatilia maanani yale yanayosemwa na wazee wa jamii ya Waswahili kumhusu Fumo Liyongo. Si mengi yameandikwa kuhusu Sakawa. Hata hivyo vitushi vyake alipoishi vimo akilini mwa jamii ambako alizaliwa. Kadhalika, nyimbo kumhusu pia zimetungwa zikirejelea vitushi hivi. Katika kuzisawiri sifa za Sakawa, usimulizi wa *Kivuli cha Sakawa* umetufaa. Aidha, tumejumlisha sifa zake zinavyoelezewa na wanajamii mbalimbali ambao tulizungumza nao katika kikao kisicho rasmi. Kabla ya kuzishughulikia sifa zenyewe, pana haja kueleza kwa muhtasari kuhusu *Utenzi wa Liyongo* na *Kivuli cha Sakawa.* Tumefanya hivi ili kuweka msingi wa chanzo cha data yetu ya uchunguzi.

## 3.1. **Muhtasari wa *Utenzi wa Fumo Liyongo***

Knappert (1983:142) anaeleza kuwa *Utenzi wa Fumo Liyongo* umeandikwa na Muhammad Abubakar Kijumwa aliyekuwa mwenyeji wa Lamu nchini Kenya. Alikuwa msanii mashuhuri ambaye mbali na kutunga mashairi na tendi, alikuwa mchongaji wa milango yenye nakshi, msanii-msanifu, msawidi na mnukuzi wa miswada ya zamani. Habari za maisha yake hazijulikani vizuri. Alianza kujitokeza katika utunzi miaka ya 1880, alipoanza kuwasaidia watafiti wa kizungu waliotaka kufahamu habari za Waswahili. Alifariki mwanzoni mwa miaka ya 1940. Mbali na Utendi wa Fumo Liyongo, Kijumwa alitunga mashairi kadha ambayo si mashuhuri, ukiwemo *Utendi wa Helewa*, Mulokozi (1999:1). Kijumwa aliipata hadithi hii

kutokana na mapokezi simulizi ya Waswahili wa Mwambao wa Kenya. Bila Kijumwa kufanya hivi huenda habari hizi zingepotea.

*Utenzi wa Fumo Liyongo* unahusu mgogoro kati ya Fumo Liyongo na kaka yake, sultan wa Pate ambaye hajatajwa kwa jina lake katika utenzi huu. Utenzi unaanza Liyongo akiwa kijana ambaye amebalekhe na anayesifika kote kwa kimo na nguvu. Wagalla wanafika Pate kununua chakula na kumtembelea sultani. Sultani huyo anawasifia Wagalla kuhusu Liyongo. Wagalla hawakuamini maneno yake hivyo akamwandikia Liyongo barua aje aonekane kwa Wagalla. Liyongo anatii na kufunga safari ya kuelekea Pate. Safari hii kwa mtu wa kawaida ni ya siku nne lakini Liyongo anatumia siku mbili tu. Anapokaribia Pate, anapuliza panda yake inapasuka. Anapuliza ya pili nayo vile vile inapasuka. Akapuliza ya tatu na kuingia mjini hadi barazani kwa sultani. Watu wanakusanyika kumwona, anapotua mzigo wake, anatoa vitu vya kutosha kujaza nyumba nzima. Wagalla wanakiri kuwa kweli Liyongo ni mtu mwenye nguvu.

Wagalla wanamwomba sultani awaruhusu kupata mbegu yake naye anakubali. Anaozwa mke wa Kigalla ambaye anamzalia mtoto wa kiume. Sifa za Liyongo zinavyozidi kuenea ndivyo fitina vya sultani wa Pate vinavyozidi. Mfalme anahofia kuwa Liyongo atamnyang'anya ufalme hivyo anatafuta njia ya kumuua Liyongo. Liyongo anapogundua kuwa mfalme anataka kumuua, anaondoka pate na kwenda kuishi nyikani miongoni mwa Wasanye, Wadahalo, Waboni na Watwa. Mfalme anawashawishi Wasanye na Wadahalo wamuue huko mwituni na anaahidi reale mia moja iwapo watamletea kichwa chake Liyongo. Wasanye na Wadahalo wanafanya urafiki na Liyongo kisha wanashauri wawe wakila pamoja kikoa. Wanapeana zamu ya kuangua makoma kutoka mtini ambayo ndicho chakula wanachokula pamoja. Wanatarajia kuwa zamu ya Liyongo inapofika, watamfuma kwa mishale yao wamuue akiwa mtini. Kwa bahati, Liyongo anagundua

hila yao na badala ya kupanda juu ya mti kuangua makoma, anatumia mshale wake kuangua makoma akiwa chini hivyo hawafaulu kumuua.

Wanakwenda mjini na kumweleza sultani kuwa haiwezekani kumuua Liyongo. Sultani anawaambia warudi wamweleze Liyongo kuwa mjini hakuna hatari kisha waje naye. Wanarudi na kumweleza hivyo, Liyongo anawaamini na kurudi nao mjini. Baada ya siku chache, sultani anaandaa ngoma ya gungu na mwao na kuwaalika mashaha wote wa aina hii ya ngoma Liyongo akiwa mmoja wao. Wakati wa ngoma, askari wanamshika Liyongo na kumtia gerezani. Inaamuliwa auwawe. Siku ya kuuwawa inapokaribia, anaambiwa afanye ombi lake la mwisho, anaomba apigiwe ngoma ya mwao na gungu. Ngoma inapoandaliwa, anatuma ujumbe wa kishairi kwa mama yake kupitia kwa kijakazi Saada ambaye humletea chakula kwamba siku hiyo apike mkate wa wishwa na kati yake atie tupa ya kukatia minyororo. Mama yake anafanya hivyo. Askari wanamnyang'anya Saada mikate mizuri na kuacha ule wa wishwa ampelekee Liyongo. Ngoma inapoanza kupigwa, Liyongo anatumia ile tupa kukata minyororo iliyomfunga, kisha anavunja lango la jela na kukimbilia nyikani.

Baada ya kushindwa kumuua Liyongo kwa njia hii, sultani anamshawishi mwanawe Liyongo aende amuulize baba yake kiwezacho kumuua. Anamwahidi kumpa uwaziri na kumwoza bintiye akifanikiwa. Kijana yule anakwenda hadi Shaka kwa baba yake na kumuuliza swali lile. Japo Liyongo anang'amua kuwa mtoto wake ametumwa na maadui wake, anakubali kumpa siri ile kuwa kinachoweza kumuua ni sindano ya shaba kitovuni mwake. Kijana anaporudi na kumweleza sultani alivyoambiwa, sultani anafurahi sana na kumpa zawadi nyingi. Anampa sindano ya shaba na kumwambia arudi amuue baba yake. Kijana anarudi kwa baba yake, anangoja akiwa usingizini, anamchoma na sindano ya shaba kitovuni. Liyongo anaamka kwa gadhabu, anachukua mshale wake na kwenda kisimani. Anapiga goti na kutia mshale kwenye

upinde huku kauelekeza mjini na akakata roho. Watu wanapomwona hivyo wanadhani yu hai na kagadhabika, hivyo wakaogopa kwenda kuteka maji kisimani. Siku ya tatu, walikwenda kwa mama yake Liyongo aje ambembeleze aondoke wateke maji. Mama yake anakwenda kila siku kumbembeleza kwa mashairi bila mafanikio. Mwishowe, maiti ya Liyongo inaanguka ndipo watu wanagundua alikuwa yu maiti.

Mfalme anapopata habari ya kifo cha Liyongo anafurahi sana. Anamwita mtoto wa Liyongo na kumpa habari ya kifo cha babake. Kijana yule anacheka badala ya kulia. Mfalme anakasirishwa na kitendo hicho na kumnyang'anya vitu vyote alivyokuwa amempa. Anamwambia aondoke machoni pake na asirudi mjini tena. Kwao, mamake anamchukia na hampi chakula. Siku chache baadaye akapatwa na maradhi yaliyosababisha kifo chake.

### 3.2. **Muhtasari wa *Kivuli cha Sakawa***

Kivuli cha Sakawa ni hadithi inayomhusu shujaa wa jamii ya Wakisii. Hadithi inaanza kwa kuangazia mgogoro ulioko katika familia ya mzee Ng'iti[1]. Mgogoro huu ni kati yake na mkewe wa kwanza kwa kukosa kumzalia mtoto wa kiume sababu iliyomfanya mzee huyu kuoa mke wa pili. Baada ya muda, mke wa pili naye hafanikiwi kujifungua mtoto wa kiume. Hili linamsukuma mzee Ng'iti kutoa kafara kwa miungu na mababu. Baada ya kafara hii, maombi yake yanajibiwa na mkewe wa pili anakuwa mja mzito. Ng'iti hakuwa na tashwishi yoyote kuwa mtoto ambaye angezaliwa angekuwa wa kiume. Hakukosea kwani baada ya muda kutimia, mkewe alijifungua mtoto wa kiume akapewa jina Sakawa.

Babake akawa na mapenzi mengi kwa Sakawa kwani alikuwa mtoto wa kipekee wa kiume atakayemrithi. Kwa sababu ya uzee wake, alimpa Sakawa mafunzo ya uganga ili atakapoaga dunia, Sakawa aendeleze taaluma hii ya babake. Baada ya kifo cha babake Sakawa, wazee

wanamtilia guu ili kuzima nyota yake ya uongozi. Licha ya fitina na hila za kumwangamiza, hakufa moyo kuimkomboa jamii yake. Alisifika kote kwa uwezo wake mkubwa katika uganga wa mitishamba na ushauri wake ulioweza kuwaunganisha wanajamii na kushinda vita dhidi ya maadui wao. Kabla ya kifo chake, Sakawa anatabiri kuja kwa wageni wanaofanana na vipepeo na kuonya wanajamii wasipigane nao watakaponyakua ardhi yao. kwa kawaida watoto hujulikana kukimbiza vipepeo (Ferber, 1999). Kwa mantiki hii Sakawa alikuwa akiwaonya Wakisii wasimbikize kile ambacho hawawezi kukishika. Ama hata wakikikimbiza wakakishika huenda kisiwafaidi. Vipepeo ni ishara ya mabadiliko makuu katika jamii. Wakati mwingine kipepeo huwa mtume au malaika wa aina fulani, ambaye huleta habari njema au kubadilisha roho za watu. Hivyo basi kwa kuwalinganisha wageni na vipepeo, Sakawa aliwaona kama wajumbe ambao wangeleta habari njema kwa Wakisii hata kuyabadilisha maisha yao. Utabiri huu unatimia Waingereza wanapowasili mjini Kisii. Kunatokea kundi la watu wanaojitolea mhanga kupambana na wakoloni hawa ambao wametwaa ardhi yao. Vifo vingi vinatokea na watu wanakumbuka ushauri wa Sakawa.

## 3.3. **Sifa za Mashujaa**

Kwenye sehemu hii mjadala wetu unahusu sifa mbalimbali walizo nazo mashujaa. Tunatoa maelezo kwa muhtasari kuhusu sifa zenyewe kisha tufafanue jinsi sifa zenyewe zinavyodhihirika katika maisha ya mashujaa tuliowateua kuwatafitia.

### 3.3.1. **Kuzuka kwa Mashujaa**

Kama tulivyodokeza hapo awali, mashujaa hawazuki katika ombwe tupu. Huchochewa na hali, kipindi na mazingira fulani maalum ya kijamii. Kunapotokea mgogoro fulani katika jamii, shujaa hutokea ili kuikomboa jamii yake. Hii ina maana kwamba jagina huzuka katika wakati mahususi

katika jamii yake na huishi hadi pale anapotekeleza dhima yake katika jamii. Kutokana na sababu hii, mighani ya jamii mbalimbali humtazama jagina kama zawadi kutoka kwa Mungu[2].

Katika sura ya pili, tumeonyesha mazingira yaliyochangia kuibuka kwa mashujaa hawa Sakawa na Fumo Liyongo. Fumo Liyongo alizuka kutokana na mgogoro wa kivita uliosababishwa na maadui wakiwemo Wasanye na Wagalla. Vile vile, Sakawa alizuka kuikomboa jamii ya Abagusii kutokana na mashambulizi ya majirani zao wakiwemo Wakipsigis, Wamaasai na Waluo. Alifaulu kukomesha vita hivi baada ya kutoa ushauri kwa Wakisii waungane pamoja katika vita hivi. Punde tu baada ya vita vya Saosao, inasemekana kwamba Sakawa aliaga dunia. Hii ina maana kwamba alikwisha kutekeleza jukumu lake na hakuwa na umuhimu wowote wa kuendelea kuishi.

Hivyo basi majagina hawa walizuka kwenye mazingira yanayofanana. Haja ya kupata mtu atakayewakomboa wanajamii kutoka kwa uvamizi wa majirani wao ilichochea kuzaliwa kao.

### 3.3.2. **Ubashiri wa Kuzaliwa kwa Jagina**

Mara nyingi kuzaliwa kwa majagina hubashiriwa. Mtabiri huelezea kuwa jagina ataibuka siku moja na kuiondolea jamii yake madhila ambayo yameisibu kwa muda mrefu. Aidha wanajamii hufahamishwa kuwa anayezaliwa / kuja ataasisi ufalme ambao utakuwa mkubwa ukilinganishwa na falme nyingine zilizopo au zilizowahi kuwepo. Kwa mfano, kuzaliwa kwa shujaa wa Wakristo (Yesu Kristo) kulitabiriwa na malaika Jibrili (Luka 1:26 - 37). Hata hivyo, katika historia ya Liyongo hatujaonyeshwa kutabiriwa kwa kuzaliwa kwake. Hata maisha ya ukembe wake hatujaelezewa. Kwa upande mwingine, kuzaliwa kwa Sakawa kulitarajiwa. Baada ya babake kutoa kafara kwa Mungu katika mapango ya jabali la Manga, alianza kufanya maandalizi

ya kumpokea mwana wa kiume ambaye alikuwa amemsubiri kwa miaka mingi (*Kivuli cha Sakawa* uk. 19).

Hii inaonyesha kwamba ingawa majagina huwa na sifa kadha ambazo hufanana, baadhi ya sifa hizo huweza kutofautiana. Lakini hatusemi kwamba sifa hii haimo kwenye maisha ya shujaa Liyongo bali haijatajwa popote kwenye *Utenzi wa Liyongo.*

### 3.3.3. **Shujaa kwa Kawaida huwa Mwanamume**

Suala la jinsia ya mashujaa limechunguzwa na wataalamu mbalimbali. Wengi wamedai kwamba shujaa mara nyingi huwa ni mwanamume japo wakati mwingine kunaweza tokea mwanamke akatajwa kama shujaa kwa kutenda labda jambo moja la kijasiri[3]. Pale ambapo shujaa huwa ni mwanamke huwa hasheheni sifa nyingi bia za kishujaa kama mwanamume. Hata hivyo mashujaa wengi wa kidini na wa kihistoria huwa ni wanaume. Kwa mfano, mashujaa hawa wa kidini ni wanaume kama vile Yesu Kristo, Buddha, Samsoni na mtume Muhammadi.

Mashujaa Fumo Liyongo na Sakawa ni wanaume. Katika *Utenzi wa Fumo Liyongo,* tunaambiwa:

Liyongo kitakamali
akabalighi rijali
akawa mtu wa kweli
na haiba kaongeya. **(ub. 6)**

“Ni mwanamume swahihi
kama samba una zihi
usiku na asubuhi
kutembea ni mamoya. **(ub. 13)**

Liyongo akikabili
ndiya kenenda rijali
alikwenda siku mbili
na ya pili ni kunginya. **(ub. 26)**

Kuhusu jinsia ya Sakawa katika *Kivuli cha Sakawa* mwandishi anadokeza;

> Huku maandalizi ya kukipokea na kukikaribisha kiumbe kipya… mvua kubwa ilinyesha kana kwamba ilikuwa inalowesha kurasa za kumbukumbu ya miaka mingi ya kukosekana kwa mtoto wa kiume katika familia ya Mzee Ng'iti (uk. 20).

Haya yanathibitisha jinsia ya wahusika hawa ambayo inafanana.

### 3.3.4. **Kuzaliwa na Ujana wa Jagina**

Kwa kawaida, kuzaliwa kwa shujaa huandamana na matukio ya ajabu ajabu. Wakati mwingine, mtoto ambaye ni shujaa aweza kuzaliwa akiwa na maumbile ya ajabu. Aidha, si mashujaa wote ambao tumeelezewa kuzaliwa kwao na maisha yao wakiwa watoto. Katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*, hatuelezwi kuhusu kuzaliwa wala miaka yake ya ujana. Aidha tuliozungumza nao wanadai kuwa alizaliwa kama mtoto wa kawaida tu. Vilevile, katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* hatuelezwi mazingira alimokulia Liyongo na uhusiano wake na vijana wa umri wake bali tunaelezwa kuwa alibaleghe na kuwa mwanamume mwenye haiba, kimo kirefu, mpana na maarufu.

Liyongo kitakamali
akabalighi rijali
akawa mtu wa kweli
na haiba kaongenya **(ub. 6)**

Kimo 'kawa mtukufu
mpana sana mrefu
majimboni yu marufu
watu huya kwangaliya. **(ub. 7)**

Knappert (1983:145) anaeleza kwamba kuzaliwa na ukembe wa Fumo Liyongo umeelezewa katika sehemu za masimulizi pokezi:

Liongo yuzewe jumbani
Mama yake kazalani
kayuwa yu mwenye shani
imara na shujaa

Na Liyongo akakuwa
nguvu nyingi akatiwa
na usemi akapowa
kwandika kayifundiya

Tofauti na Liyongo, tunaelezwa kuhusu kuzaliwa kwa Sakawa, maelezo yake wakati alipokuwa mtoto na hata kijana. Siku aliyozaliwa Sakawa kulikuwa na mvua ya ajabu kama tunavyodokezewa katika *Kivuli cha Sakawa*:

> Huku maandalizi ya kukipokea na kukikaribisha kiumbe kipya katika … mawingu meusi angani yalijikusanya harakaharaka. Muda si muda parakachaparakacha za radi zilianza kusikika. Mvua kubwa ikanyesha kana kwamba ilikuwa inalowesha…. Aidha mtoto huyu "Sakawa" alizaliwa akiwa ameota meno. Kitu cha ajabu kumhusu mtoto huyu kilikuwa kwamba alizaliwa akiwa ameota meno[4] (uk. 20, 21).

Mvua huashiria maisha pamoja na kitu cha kuzalisha zaidi. Isitoshe huonyesha utakazaji kutokana na umuhimu wa maji na kwamba maji haya hunyesha kutoka mbinguni. Kutokana na hali hii mvua huonyesha athari za roho ya miungu zinazoandamanishwa nayo. Hivyo basi kunyesha kwa mvua siku alipozaliwa Sakawa kunaashiria kwamba kiumbe huyu alikuwa baraka kwa wanajamii. Karibu kila jambo alilolitabiri lilikuja kutimia (taz. Ochoi, 2013). Kwa mujibu wa Ferber (2007) mvua huashiria mateso, bahati mbaya au nguvu za kurutubisha nchi zinazotoka juu. Kwa kuwa mvua ni sinekdoki ya hali mbaya ya anga, maisha aliyoyaishi Sakawa yalikuwa ya kupigana na adui wake wa ndani na nje. Wapo wazee ambao hawakutaka aishi. Pia jamii za Waluo, Wakipsigis na Wamaasai waliwaua Wakisii mara kwa mara na kuiba mifugo wao.

Vilevile, inasemekana kwamba Sakawa hakutangamana na watoto wa rika yake bali alikwenda vichakani peke yake. Pia aliandamana na babake kwenda msituni kutafuta majani, mizizi na hata maganda ya miti kutengeneza dawa za kukidhi mahitaji ya wamajamii kinyume na vijana wengine wa rika lake. Ama kweli babake Sakawa aliamini kwamba kwamba uzee utakuwa upumbavu na wa kujaa usahaulifu ikiwa utawapuuza vijana (Rawling, 2003). Hili ni jambo lisilo la kawaida kwa vijana kutotangamana na wenzao katika jamii.

### 3.3.5. **Shujaa Hutokana na Ukoo Bora/ Ukoo wa Kifalme**

Jagina hutokana na ukoo bora au ukoo wa kifalme. Otto Rank, katika Green (1997) akiwatumia Musa, Paris, Siegfried, Romulus, na Lohengrin anasema kwamba majagina huzaliwa katika familia ya kifalme na kutawa hata kuzaliwa kwao huwekwa siri kubwa. Babake shujaa aghalabu huwa mfalme au kiongozi wa jamii yake.Ukoo huu huchukuliwa na wanajamii kuwa umeteuliwa na kutengwa kando uweze kuongoza jamii. Fumo Liyongo alitokana na ukoo wa Al Bauri (Allan 1993: 121). Ukoo huu ulichukuliwa kuwa bora ulioheshimiwa na kupewa jukumu la kuongoza jamii na hususan jamii ya Waswahili wa Pate. Babake Fumo Liyongo kwa jina Mringwari alikuwa Sultan wa dola ya Pate kabla ya kifo chake.

Kwa upande mwingine Sakawa alitokana na ukoo bora uliokuwa na umaarufu na mali vilevile. Kama tunavyoelezewa katika *Kivuli cha Sakawa*:

> Hakujua ni nani angerithi mali yake nyingi iliyokuwa inaongezeka kutwa kucha kutokana na umaarufu wake katika taaluma ya uganga wa mitishamba (uk. 6).

Hii ina maana kwamba babake Sakawa alikuwa mtu maarufu katika jamii yake.

### 3.3.6. **Shujaa huwa na Maadui / Wapinzani**

Kwa kawaida, shujaa huwa hakosi wapinzani /maadui. Maadui hawa humwonea kijicho na huwa na nia ya kumwangamiza. Maadui wa shujaa huwa ni muhimu katika kuonyesha ushujaa wa shujaa. Maadui huwa ni kizingiti muhimu katika maisha ya jagina ambacho anafaa kukivuka ili kudhihirisha ujagina wake. Kwa mfano, ni kutokana na maadui hawa ambapo sifa za nguvu, sihiri na ung’amuzi zinajitokeza. Shujaa huweza kung’amua hila za maadui zake na kizikwepa.

Fumo Liyongo, kama jagina alikuwa na maadui kama vile binamuye Daudi Mringwari aliyehofia kuwa huenda Fumo Liyongo akampokonya ufalme, Wagalla na mwanawe aliyemsaliti. Daudi Mringwari alipanga njama za kumwangamiza Liyongo kwani alimwona kama tishio dhidi ya

utawala wake. Aliwatuma Wagalla ambao pia walichukuliwa kuwa wanaweza kumwangamiza lakini wakashindwa na kuishia kumwogopa kutokana na kimo chake. Aidha alimtuma mwanawe Liyongo ambaye alimuua.

Kama Fumo Liyongo, Sakawa alikuwa na maadui. Baada ya Sakawa kuzaliwa akiwa ameota meno, baadhi ya wanajamii walidai kuwa ni ishara ya mkosi ambao ungeikumba jamii ya Abagusii. Wakapendekeza kuwa aangamizwe. Aidha baada ya kifo cha Mzee Ng'iti, kutokana na mafunzo ya uganga aliyopewa Sakawa kutoka kwa babake, alitia fora na kujulikana sana katika kila pembe. Sifa hizi ziliibua maadui katika jamii yake na wakapanga mikakati ya chini kwa chini kumwangamiza (*Kivuli cha Sakawa* uk. 47). Zipo sababu tatu za Sakawa kuwa na maadui wengi. Kwanza, alikuwa kijana mdogo ambaye hakuwa na tajriba yoyote maishani. Pili, hakuwa na mvi wowote kichwani na tatu walimchukia kwa sababu daima alisema ukweli ambao uliwachoma kama mkuki (*Kivuli cha Sakawa* uk. 47). Hivyo basi kwa kuwa kijana mdogo na maarifa mengi, alikuwa na maadui ambao walikuwa na wivu. Kama tutakavyoona baadaye, uadui huu ulizidi ukasababisha Sakawa kugura kwao pamoja na aila yake.

### 3.3.7. Shujaa huwa Kipenzi cha Wanajamii

Japo shujaa huwa na maadui wengi, kwa kawaida huwa ni kipenzi cha wanajamii walio wengi. Mapenzi haya ya wanajamii kwa jagina ndio huwa chanzo cha uadui wanapoona jinsi watu wanaajabia na kusifu ushujaa wake. Basi wao hukirihika na kumwonea wivu kwa sababu ya ufanisi wake. Kutokana na dhima ya jagina ya kukomboa jamii yake kutoka hali ngumu, wanajamii humsifu jagina wao wanayemtarajia kuwaletea mabadiliko. Umaarufu wa shujaa huenea katika jamii nzima na kila wakati wanajamii hutarajia mambo makubwa kutoka kwake.

Fumo Liyongo anarejelewa kama mtu maarufu aliyependwa na kuajabiwa na wanajamii wa Uswahilini. Katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* (ub. 88), Liyongo alipokamatwa na kutiwa gerezani, Sultan aliomba ushauri kutoka kwa wanajamii kuhusu kuuawa kwake.Wanajamii walimtetea kwa kila njia kwa sababu walimwona kama mtetezi wao dhidi ya maadui wao kama tunavyoelezwa katika beti mbili zifuatazo za *Utenzi wa Fumo Liyongo:*

Kukifanywa mashauri
"Auwawe" madhukuri
"tulepuwe lake shari
Liyongo namcheleya." **(ub. 88)**

Wenginewe wakanena
"Kumuuwa siyo sana
huyu nda mui zana
ni mwenye kukuteteya. **(ub. 89)**

Vile vile, kifo cha Fumo Liyongo kiliwasikitisha wanajamii sana. Beti zifuatazo zinaonyesha kiwango cha huzuni waliokuwa nao wanajamii.

Make Liyongo hakika
matanga aliyaweka
watu wakasikitika
kwa Liyongo kuifiya.**(ub. 224)**

"Liyongo Silaha yetu
kwa wut'e khasimu zetu
alikuwa ngao yetu!"
wut'e wakinena haya.**(ub. 225)**

Mui walisikitika
hakuna wa kutosheka
kwa Liyongo kutoweka
imeanguka paziya. **(ub. 226)**

Sana wakahuzunika
na matanga wakaweka
kisa mamake kutoka
kana ada katembeya. **(ub. 227)**

Katika beti hizi, wanajamii wanamrejelea Liyongo kama silaha na ngao yao. Sasa ameliacha pengo, aidha mtunzi ametumia fumbo "imeanguka paziya" kwa maana ya kuwa jamii imeachwa bila mtu wa kuwaongoza na kuwatetea hivyo wanaweza kuvamiwa na maadui.

Umaarufu wa Liyongo vile vile unajitokeza katika sherehe za gungu na mwao zilizofanywa kabla ya kuuawa kwake ilivyotarajiwa na Sultani Daudi Mringwari. Watu walipotangaziwa kuhusu sherehe hizi, walijitokeza kwa wingi. Liyongo alisifika sana kuwa bingwa wa gungu na mwao na wengi walimpenda na kujihusisha naye. Tunaambiwa katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*;

Liyongo nikwambiao
Shaha wa gungu na mwao
tena ni mkuu wao
huwashinda wut'e piya. **(ub. 79)**

Na ngoma na nyingi kusi
kusisalie unasi
ikawa kama harusi
watu wakiangaliya. **(ub. 112)**

Kwa upande mwingine, Sakawa kama shujaa naye alikuwa kipenzi cha wanajamii. Japo alikuwa na maadui ambao kwa kiasi kikubwa walikuwa wazee, alikuwa kipenzi cha wengi. Mapenzi haya yalitokana na umaarufu wake katika uganga wa mitishamba na vilevile ushauri wake mzuri wa kila mara ambao uliwasaidia wanajamii kuepuka madhila ya mara kwa mara. Mapenzi haya yanaonekana pale ambapo taarifa kuhusu kifo chake ziliposikika, wengi walihuzunika.Watu wengi hata kutoka makabila mengine walifika kuomboleza kifo chake (uk. 79) "Hata Isiria Maasai na Wakipsigis … walifika kushuhudia mkosi uliomkumba tabibu waliyemthamini na kumheshimu kwa dawa na ushauri wake."

### 3.3.8. **Safari ya Shujaa**

Safari huwa jazanda mwafaka kwa kuwa inaweza kusimamia dhana mbalimbali zinazohusu nyanja mbalimbali za maisha. Inaweza kuwakilisha mchakato, usafiri wenyewe au shughuli yoyote itekelezwayo kufikia lengo fulani. Safari huwa motifu inayojitokeza katika tungo za kale

kuwahusu mashujaa hivi kwamba huakisi uvikale ndani yake. Shujaa hufunga safari kwa sababu mbalimbali kama vile kutafuta utambulisho wake, kutafuta nchi nzuri jamii yake imeahidiwa, kutafutata mbinu za kulipiza kisasi, kuwaokoa wanajamii wake, kutafuta mpenzi (kama kumwokoa mwana wa mfalme aliye taabani ndipo apatiwe msichana), kusaka hekima, kuiokoa nchi yake kutokana na majanga kama ukame ama kuusaka ukamilifu wa binadamu. Safari ya jagina huwa na sifa zifuatazo: Huwa hana tajiriba au uzoefu wowote. Hii ina maana kwamba huwa na usungo mwingi. Awapo njiani anakumbana na mazimwi au binadamu waovu kimo cha mazimwi. Hata hivyo, jagina huwa na mwelekezi wake mwenye busara kuu kama kielelezo kwake kama vile msichana mrembo ambaye humpa moyo kuendelea kujisaka. Huzaliwa mashambani, mbali na watu wengi wa mjini. Huvuka maji. Hupoteza wazazi wake akiwa mkembe hivi kwamba analelewa na wanyama au viumbe wa ajabu. Hatima ya safari humpevusha akili na kumwezesha kuuelewa ulimwengu kwa undani.

Katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* safari inajibainisha kama mchakato unaompitikia mhusika mkuu Fumo Liyongo. Kwa mujibu wa Voytilla (1999) safari aifungayo jagina huwa na hatua kumi na mbili. Hatua muhimu zaidi ni tano.

Ama kweli jagina hufunga safari halisi katika juhudi zake za kutatua shida fulani. Hata hivyo, safari hii huwa na umuhimu mkubwa wa kisaikolojia, jinsi ilivyo muhimu katika uhalisia. Matendo na maamuzi anayoyafanya humkuza kama mhusika. Ujasiri wa Sakawa na Fumo Liyongo unadhihirishwa hivi kwamba hata wanajamii wenzake wanamwamini hadi wanamchukulia kama zawadi waliyotumiwa na miungu wao kuwakomboa jinsi tutakavyoona baadaye kwenye tasnifu hii. Inahalisi kutaja kwamba kuna sehemu mbili za safari hii – safari ya ulimwengu halisi na ile ya ulimwengu wa kidhanaishi ama wa miungu. Baada ya kifo cha Sakawa, waombolezaji walipokuwa wakifukua mabaki yake hawakupata mwili wake. Asemavyo

mwandishi wa *Kivuli cha Sakawa* wanajamii bado wanamsubiri kurudi. Hii ina maana kwamba yumo safarini bado. Safari hii ndiyo tunayoirejelea kama ya ulimwengu dhanifu. Safari aliyoifunga hadi mapango ya mlima Manga tunaweza kuirejelea kama ya ulimwengu halisi kama ilivyo safari aliyoifunga Fumo Liyongo hadi kwa Wagalla. Ajabu ya safari hii ni kwamba badala ya kutumia siku nne, Liyongo anatumia siku mbili hivyo kuifanya kuwa safari ya kipekee. Hivyo basi, sharti jagina afunge safari ya kipekee itakayomwezesha kutekeleza jukumu lake kwa wanajamii. Hii ni safari ambayo humpeleka kwenye ulimwengu maalumu kama njia ya kumtayarisha kutekeleza jukumu lake.

Safarini, jagina hukumbana na vikwazo, vizuizi na changamoto za kila aina ambazo hufaa kuziepuka ili mwishowe afanikiwe. Hii huwa njia ya kumtayarisha kutekeleza jukumu lake (taz. Voytilla 1999; Vogler 2007). Mara nyingi, shujaa hutoka au hutoroka nyumbani kwao na kwenda kuishi katika sehemu zilizo mbali na nyumbani. Sababu ya kutoroka kwa shujaa ni kutokana na tishio la kuangamizwa na maadui wake. Kama tulivyotaja hapo awali, maadui wa mashujaa kwa kiasi kikubwa huwa ni viongozi wanaohofia shujaa huenda akawapokonya ufalme. Safari hii ya jagina mara nyingi huwa ni muhimu kwani humtayarisha shujaa kutekeleza wajibu wake katika jamii. Ni katika safari ambapo shujaa hujifunza mbinu za kukabiliana na maadui wake. Katika safari ya kishujaa, shujaa anaweza kurejea kwao au asirudi. Kulingana na Mutiso (1999: 31), safari ya shujaa inaweza kuwa ya kiwakati, kimahali, kifikira au kisaikolojia. Katika safari ya kisaikolojia, jagina huzindukana kutokana na mawazo mapya anayopata. Baadaye yeye huwafunza wafuasi wake mambo wanayostahili kutenda na hivyo kuubadili mfumo wa jamii. Mutiso anasisitiza kuwa, safari ya aina yoyote ile, huhusu kule kutoka kwenye mazingira au hata ukawaida na kuingia kwenye hali au mazingira mengine tofauti. Hili humfanya jagina kutazama mambo yaliyomo kwenye jamii yake kwa jicho tofauti kabisa.

Fumo Liyongo aligura kutoka nyumbani kwao na kuishi porini. Hii ni kwa sababu ya tishio la Sultani wa Pate Daudi Mringwari la kutaka kumwangamiza. Kutokana na maelezo ya Mutiso (khj) tunaweza kusema hii ni safari ya kimahali. Kule porini waliishi pamoja na Wasanye na Wadahalo. Hawa wanamhadaa Liyongo kutokana na njama waliyokuwa wameipanga na Mringwari kwa kumwambia amebadili nia ya kumwua, si mbaya tena. Walipanga kumfuma kwa mshale atakapopanda kwenye mkoma kuangua makoma zamu yake itakapofika lakini Liyongo akaangua makoma kwa kutumia mshale bila kuupanda mkoma. Jambo lililowashangaza na hata kuishia kumwogopa Liyongo. Kwenye *Utenzi wa Fumo Liyongo* tunaambiwa:

Mfalume changaliya
mwituni mekimbiliya
Wasanye kawazengeya
na Wadahalo pamoya (**ub. 52**)

Na wao maana yao
siku yeye apandao
wamfume wut'e hao
zembe kwa wao umoya **(ub. 59)**

Kama Fumo Liyongo, Sakawa naye aligura kwao kwa sababu ya kutaka kusalimisha maisha yake. Tumesema kwamba wazee na maadui wa Sakawa walimchukia. Uadui huu haukuisha bali ulichukua sura nyingine. Uhasama kati ya Sakawa na maadui zake ukawa maradufu na wakataka wamwangamize. Walikodisha majambazi wamshambulie Sakawa katika makazi yake wakati wa usiku. Sakawa alipata fununu kuhusu njama hiyo. Aliipasha habari familia yake na wote wakatorokea kijiji jirani cha Mwamosioma ili kutoa maisha yao hatarini, (*Kivuli cha Sakawa* uk. 48). Hata hivyo hakukata tamaa ya kuikosoa jamii na vilevile kuikomboa.

### 3.3.9. **Mashujaa huwa na Akili Pevu/ Uwezo wa Kung'amua au Kutabiri**

Mashujaa kote ulimwenguni huwa wenye akili pevu au wenye uwezo wa kung'amua mambo yaliyofichika. Akili pevu huwasidia kukwepa hila za maadui wao na hivyo kuishi hadi pale wanapotimiza wajibu wao katika jamii yao. Aidha shujaa huweza kuyatabiri ya kutokea baadaye. Fumo Liyongo anasawiriwa kama mtu aliye na akili pevu na pia mwenye uwezo wa kutabiri mambo. Uwezo wake wa ung'amuzi ndio ulimwezesha kukwepa hila za Sultan wa Pate alipotaka kumwangamiza, kwa mfano, katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* tunaelezwa:

Fitina zikamngiya
Mfalume miya miya
kwa hila kakusudiya
kumuuwa fahamiya (**ub. 49**)

Liyongo akatambuwa
huzengea kuuwawa
pale Pate kayepuwa
Barani akitembeya (**ub. 50**)

Aidha Wasanye na Wadahalo walipoambiwa wamuue Liyongo kwa kuahidiwa riale mia moja, walimtafutia mkoma mrefu zaidi ili atakapoupanda, wamfume kwa mishale. Liyongo aling'amua na akaangua makoma mengi zaidi kwa kutumia mshale bila kuupanda mkoma. Maelezo haya tunayapata katika beti zifuatazo za *Utenzi wa Fumo Liyongo*: 62 – 65. Alipotiwa kizuizini, alitumia akili yake pevu kujinasua kutoka gerezani. Alitumia ushairi ambao ni mama yake tu angeweza kung'amua ujumbe uliokuwemo. Tunaelezwa katika Utenzi wa Fumo Liyongo:

Kamba "Sada nakutuma
enda kamwambie mama
afanye mkate mwema
kati tupa aitiya. (**ub. 104**)

Vile vile, mwanawe Liyongo alipomuuliza kitu kinachoweza kumuua, Liyongo anang'amua kuwa ametumwa na maadui wake kumwangamiza. Aidha Liyongo anamfunulia kuwa amehadaiwa jambo ambalo linakuja kutokea. Baada ya kumuua babake, zile ahadi zote alizokuwa ameahidiwa hazikutimizwa. Katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* tunaambiwa:

Babake akamwambiya
"wewe kuuliza haya
dhana nimekudhaniya
kuniuwa huzengeya." (**ub. 136**)

Akamwambia "Nayuwa
kijana umefundiwa
na wewe utahadawa
hayo yamezokwambiya. (**ub.140**)

Tunaambiwa Sakawa alikuwa mwerevu na aliyependa kujifunza mambo mengi. Licha ya kuwa kijana mdogo, alipenda kuulizauliza maswali kwa lengo la kuelewa kila jambo kwa kina. Isitoshe, tunafahamishwa kwamba sababu ya wazee kumchukia ni kuwa alikuwa amekirimiwa hekima ingawa alikuwa kijani. Aidha, alikuwa na uwezo wa kutabiri mambo ambayo hapo baadaye yangekuja kutokea. Kwa mfano, alitabiri kuwa wanajamii wangekumbwa na janga la njaa endapo hawangetii ushauri wake. Alibashiri kuwa nchi yao ingeshambuliwa na wingu la nzige ambao wangeharibu mimea yote na hivyo basi kuzuka kwa baa kuu la njaa. Katika *Kivuli cha Sakawa* (uk.49). Haya yalitimia tunavyoelezwa, "ilipotokea kuwa utabiri wa Sakawa ulikuwa umetimia…" (uk. 51). Vilevile alitabiri kuwa watakuja wageni wanaofanana na vipepeo nao watatwaa ardhi yetu (uk. 75). Utabiri huu pia ulitimia kwa kuja kwa wazungu wakoloni.

### 3.3.10. **Maisha ya Mashujaa huwa ya Dhiki Tupu**

Mara nyingi, maisha ya majagina huwa ni ya dhiki tupu. Baadhi ya dhiki wanazozipitia majagina ni kama tishio la kuuwawa, kugura kwao na kuteseka katika nchi tofauti, maisha ya upweke, kusalitiwa na kadhalika. Kama tulivyosema hapo awali ni kuwa dhima ya jagina ni kuikomboa jamii yake kutokana na mgogoro unaoikumba. Hali ikiwa ni hii, jagina hatulii hadi pale anapotekeleza lengo lake. Anapofanya hivi lazima atateswa, alaumiwe, ashutumiwe, asingiziwe na hata auwawe. Kwa mfano shujaa wa Wakristo (Yesu Kristo) aliishi maisha ya dhiki tupu. Alizaliwa kwenye zizi la ng'ombe, akakataliwa na jamii yake, akasingiziwa na mwishowe akauwawa.

Vile vile Fumo Liyongo aliishi maisha yaliyojaa rundo la dhiki. Hakutulia kutokana na vitisho vya binamuye Daudi Mringwari. Alitoroka kwao na hata mjini kwenda kuishi porini. Pale porini, maisha yake yakawa hatarini baada ya Wasanye na Wadahalo kula njama na Daudi Mringwari kumwua Fumo Liyongo. Aidha, alikamatwa na kutiwa kizuizini hadi alipotumia akili yake pevu kujinasua.

Sakawa kama shujaa wa jamii ya Wakisii naye maisha yake yalijaa rundo la dhiki tangu kuzaliwa kwake. Kwa sababu alizaliwa kama ameota meno, baadhi ya watu walisema hiyo ni ishara ya mkosi katika jamii hivyo basi wakahiari kuuwawa kwake. Hawa wapinzani wake wanaongeza dhiki maishani mwake. Uadui na wivu ulizidi hadi ikamlazimu kugura kwao baada ya kutishiwa kuuawa na wazee waliomwonea gere. Maadui waliwatuma majambazi kumuua, lakini walipomkosa walichoma makazi yake yote. Hata hivyo, ushauri aliokuwa akiwapa wanajamii mara nyingi haukutiliwa maanani kwa sababu ulitolewa na kijana wa umri mdogo kama yeye. Hivi ni kusema kwamba, maisha yake kama shujaa yalijaa dhiki tele kwa sababu ya umri wake mdogo na kutenda mambo ya ajabu.

### 3.3.11. **Maisha na Matendo ya Mashujaa huwa ya Kimiujiza**

Mashujaa hutofautiana na wagina yaani watu wa kawaida kutokana na uwezo wao wa kutenda mambo yasiyo ya kawaida. Kwa mfano, Yesu Kristo ambaye ni shujaa wa Wakristo, alitenda miujiza mingi iliyowafanya watu kumfuata kwa wingi na kumstahajabikia. Hii ni pamoja na kufufua wafu, kuponya wagonjwa na hata kutembea juu ya maji.

Fumo Liyongo kwa upande wake alitenda vitendo visivyo vya kawaida. Kwa mfano alitembea kutoka Shaka hadi Pate kwa siku mbili tu. Hii ni safari ambayo kwa mtu wa kawaida huchukua siku nne kwa mwendo wa haraka (ub 24, 25) huku akiwa amebeba mkoba ambao ndani yake vitu

vingejaa nyumba nzima (ub 36). Alipofika Pate alipuliza na kupasua punda tatu (ub. 27, 30, 31). Vilevile aliweza kuikereza minyororo kwa kutumia tupa jambo ambalo si la kawaida na vile vile kuangusha makoma mengi mno kwa kutumia mshale bila kuupanda mkoma.

Kama Fumo Liyongo, maisha ya Sakawa nayo yalijaa miujiza. Kwanza kabisa, alizaliwa akiwa na maumbile ya ajabu. Wakati wa kuzaliwa kwake pia mvua kubwa ilinyesha ambayo haikuwa ya kawaida. Alivyoendelea kukua, mambo aliyoyatenda yalikuwa ni kinyume na ya watoto wa umri wake. Aliweza kwenda msituni peke yake ili kuwa na muda wa kufikiria. Aidha, aliweza kujua miti mbalimbali ya kutibu kwa haraka. Hili linadhihirisha kwamba alikuwa na akili pevu.

### 3.3.12. **Mashujaa huwa na Kimo Kikubwa na Nguvu Nyingi**

Majagina hasa wa kihistoria huwa na vimo vya majitu na nguvu nyingi zisizo za kawaida. Sifa hii ni mojawapo ya sifa muhimu za mashujaa ambazo huwafanya wanajamii wastaajabie shujaa wao. Vimo hivi vya majitu na nguvu nyingi pia husaidia shujaa katika vita dhidi ya kuikomboa jamii yake kutoka kwa adui. Katika utenzi wa *Fumo Liyongo*, Liyongo anasawiriwa kama mtu mkubwa na mwenye nguvu nyingi na ambaye anatisha. Katika kuwaeleza Wagalla kuhusu Liyongo, Sultani Daudi Mringwari anasema:

Ghafula kikutokeya
mkoyo hukupoteya
tapo likakuwiliya
ukatapa na kuliya. (**ub. 14**)

Mato kikukodoleya
ghafula utazimiya
kufa kutakurubiya
kwa khaufu kukungiya. (**ub.15**)

Isitoshe, Wagalla ambao walikuwa ni mashujaa wa mwituni wanapolinganishwa na Fumo Liyongo, inasemekana walimfika magotini. Ulinganishi huu unaonyesha Liyongo alivyokuwa jitu la mtu.  Katika beti 34 na 35 tunaambiwa;

| | |
|---|---|
| "Napite" akamwambiya<br>kipita akatokeya<br>Wagala wakashuhudiya<br>khaufu ziliwangiya (**ub. 34**) | Ruhu zikenda kishindo<br>zimo zao hukoma ondo<br>huyo ni bwana wa kondo<br>ashindaye jeshi niya (**ub. 35**) |

Nguvu zake nyingi za kimwili zinadhihirika pale ambapo anapuliza na kupasua panda tatu punde tu anapozipuliza. Katika masimulizi pokezi ya Waswahili, wanamtaja Liyongo kuwa simba wa Uswahilini kwa sababu ya maumbili na kimo chake. Ndposa watu wakamwita mfalme wa Uswahilini. Tunaelezwa[5]:

Liyongo simba wa miji
Azegele ja siraji
watu wamveze taji
ya nchi Sawahiliya.

Sakawa kwa upande mwingine hakuwa na kimo cha jitu au cha kustaajabiwa wala hakuwa na nguvu nyingi. Hakuna popote pale tumeelezwa kwa umbo lake halikuwa la kawaida. Hii inaonyesha kwamba baadhi ya mashujaa huwa na umbo la binadamu wa kawaida.

### 3.3.13. **Ndoa**

Mara nyingi, ili shujaa aweze kutimiza dhima yake katika jamii, ni sharti awe huria. Wengi hawatilii maanani swala la ndoa. Kwa kawaida, ndoa huwa na majukumu mengi na kwa hivyo huenda ikamfunga shujaa na kuwa kikwazo kwa shujaa kutimiza dhima yake. Hata hivyo, hatuwezi kusema kuwa majagina wote hawaoi. Katika utenzi wa *Fumo Liyongo*, tunafahamishwa kuwa Fumo Liyongo alioa (bt. 45, 46). Wagalla walimpa mke kwa sababu walitaka mbegu yake. Alipata mtoto wa kiume ambaye alimsaliti na kumwua baadaye.

Sakawa kama Liyongo, alioa. Tunavyoelezwa na Ochoi (2013), Sakawa alipata mtoto wa kiume anayeitwa Nyamacharara. Okombe, Openda na Nyataige wanatajwa kuwa wajukuu wa Sakawa.

Katika *Kivuli cha Sakawa*, mwandishi anamsawiri Sakawa kuwa hakuoa. Maisha yake yote alitia bidii kukosoa na kushauri jamii pale ilipobidi. Isitoshe, alijihusisha sana na safari za mwituni kutafuta mitishamba kwa ajili ya mahitaji ya wateja wake waliotoka kila sehemu ya Gusii pamoja na majirani wao kama Wakipsigis na Wajaluo. Aidha, huenda ikawa sababu ya kutooa pia ni kuwa na umri mdogo ambapo hakuwa amekomaa kuanzisha familia yake mwenyewe.

### 3.3.14. **Shujaa Uhusishwa na zaidi ya Jamii Moja**

Japo shujaa hutokana na jamii fulani, yeye hachukuliwi kuwa tu wa jamii hiyo bali watu kutoka jamii nyingine hujihusisha naye. Fumo Liyongo tunayemtambua kama shujaa wa Waswahili, kuna jamii ambazo hujihusisha naye zikiwemo Wasegeju, Wabajuni na Wapokomo kama anavyoeleza Nurse (1994:69) akirejelewa na Gichamba (2005:70). Katika mahojiano yake na mmojawapo wa Wabajuni, alielezwa kuwa Fumo Liyongo alikuwa Mbajuni. Mjadala wao ulikuwa kama ifwatavyo:

**Swali**: Fumo Liongwe alizaliwa wapi?
**Jibu:** Fumo Liongwe alikuwa huko Shungwaya. Fumo Liongwe ni Mbajuni. Alizaliwa na kulelewa huko Shungwaya.

Werner (1915:333) vile vile akirejelewa na Gichamba (2005:108) anaeleza kuwa alifahamishwa na mmojawapo wa mjumbe mmoja mtoa habari kuwa Fumo Liyongo alikuwa Msegeju. Hii inadhihirisha Wasegeju na Wabajuni walitaka kujinasibisha na Liyongo. Pia Wapokomo (khj) wanajihusisha naye kwa kudai kuwa Fumo Liyongo alikuwa mtu wa Witu na mfalme wa Witu Nurse (1995:42).

Kwa upande mwingine, japo Sakawa alitokana na ukoo wa Abagusii, makabila mengine ambao walikuwa majirani wa Abagusii wanajihusisha naye. Kwa sababu ya taaluma yake ya uganga wa mitishamba, sifa zake zilienea kote na watu kutoka makabila mengine walikuja kutafuta msaada

kutoka kwake. Haya yanathibitika katika *Kivuli cha Sakawa* tunapoambiwa; "jamii ya Waluo kutoka sehemu za Gem, Mumbo na Nyakach walifika nyumbani kwa Sakawa kwa wingi …jamii hii bila shaka ilikuja kutoa heshima zake za mwisho kwa mtabiri na tabibu ambaye huduma zake hazikujua mipaka wala kabila". (*Kivuli cha Sakawa* uk. 79). Isitoshe Wakipsigis waliwasili kuhudhuria mazishi yake ingawa walipata kwamba tayari keshazikwa. Kuja kwao kunadhihirisha kwamba alikuwa ametambuliwa hata nje ya jamii yake.

### 3.3.15. **Usaliti wa Jagina**

Majagina mara nyingi husalitiwa na watu walio karibu nao jambo ambalo husababisha kufa kwao au mwisho wao. Usaliti hutokana na jagina kufichua siri yake kwa mtu ambaye yuko karibu naye na ambaye mara nyingi huwa ametumwa na mahasidi wa jagina. Kwa mfano, tukirejelea majagina wa kidini, kama vile Yesu Kristo alisalitiwa na mmoja wa wanafunzi wake na akauwawa. Samsoni, shujaa wa Waisraeli kwenye Biblia, naye alisalitiwa na mkewe akatobolewa macho na Wafilisti kutokana na usaliti huu. Kwa kuhisi kwamba amesumbuka mno mikononi mwa Wafilisiti, Samsoni anatikisa mihimili ya nyumba walimokuwa hadi paa likaanguka na kuwauwa wote waliokuwemo pamoja naye. Katika majagina wa kihistoria, Lwanda Magere alisalitiwa na mkewe baada ya kumfichulia siri kuwa uhai wake ulikuwa kwenye kivuli chake. Siri hii mkewe aliwafichulia mahasidi wake ambao waliuchoma mkuki kwenye kivuli chake na kumuua.

Tukirejelea mashujaa wa somo letu, kuna usaliti vilevile. Baada ya kujaribu kila mbinu kumuua Fumo Liyongo na zote kuambulia patupu, Sultani wa Pate aliamua kumtumia mtoto wake Liyongo kujua kimuuacho. Katika Utenzi wa *Fumo Liyongo* tunaambiwa;

Kwa baba enda sikhini
umuulize yakini
kimuuwacho ni n’ni
nakuomba hili moya. (**ub. 126**)

Mtoto wa Liyongo alikwenda kwa babake na kumuuliza kitu ambacho kinaweza kumuua. Japo Fumo Liyongo alinga’amua kuwa ametumwa na anataka kumuua, alimwambia siri hii aliyoitaka. Mtoto huyu alifululiza hadi kwa Sultani wa Pate na kumpa siri hii. Sultani alimpa mtoto sindano ya shaba akamuue babake baada ya kumpa ahadi chungu nzima. Haya tunaelezewa katika beti zifuatazo:

“Kikuuwacho ni n’ni
nami niyuwe yakini
nina hamu ya moyoni
atakuweka Jaliya. (**ub. 135**)

Babake akamwambiya
“Wewe kuuliza haya
dhana nimekudhaniya
kuniuwa huzengeya. (**ub. 136**)

“Kitu kiuwacho baba
ni msumari wa shaba
menambiya ni akiba
ya hatari kucheleya.” (**ub. 152**)

Aidha, tunaweza kusema pia kule kutaka kuuawa na binamuye Daudi Mringwari ni usaliti. Katika hali halisi, tunatarajia watu wenye uhusiano wa karibu kushirikiana kwa karibu na kusaidiana. Hivi ni kusema kwamba, kumtafutia ila jamaa wa karibu inakuwa ni usaliti na kinyume na maadili ya jamii kwa jumla.

Kwa upande mwingine Sakawa hakusalitiwa na aila yake japo alisalitiwa kwa namna fulani. Usaliti wenyewe hausababishi kifo chake kama ule wa Fumo Liyongo. Usaliti tunaouona katika *Kivuli cha Sakawa* ni kuwa, japo aliwashauri wazee jambo la kufanya alipotabiri kuhusu kuja kwa wageni wanaofanana na vipepeo, ushauri huu haukutekelezwa baada ya kifo chake. Baada ya kuja kwa wageni hao alivyosema Sakawa, kikao kilifanywa kujadiliana watakavyokabiliana na wageni hao. Jambo hili lilikuwa kinyume na alivyoshauri Sakawa, (uk 83) "Sakawa alituonya tusithubutu kuwachokoza…" "Sakawa hayuko nasi kwa sasa…asiyekuwepo na lake halipo". Huu ulikuwa ni usaliti kwa kwenda kinyume na matakwa ya jagina. Kama tutakavyoona hapo baadaye, wasaliti wa majagina hukumbwa na matatizo hata vifo kutokana na usaliti wao.

### 3.3.16. **Wasaliti wa Majagina Hawaishi kwa Muda Mrefu/ Hutaabika**

Tumekwishataja kuwa mara nyingi shujaa husalitiwa jambo ambalo husababisha kifo chake[6]. Msaliti na jagina ni pande mbili ambazo daima hukinzana. Penye ujagina usaliti huchipuza. Baada ya kifo cha jagina, wanaomsaliti huishia kufa au hata kukumbwa na matatizo ya kila nui kama vile kutotekelezwa kwa ahadi walizopewa na mahasidi wa jagina, kuwa katika hali ya upweke na vile vile kupatwa na majanga kama vile njaa au kupoteza ukoo wao. Tukirejelea Fumo Liyongo baada ya kumsaliti na kumuua babake, mwanaye Liyongo aliishi katika hali ya upweke:

Kangiya mayutoni
katindikia nyumbani
hata wenzi hawaoni
hamu imezomngiya (**ub. 220**)

Linalojitokeza hapa ni kwamba ahadi zote alizokua za Sultani hazikutimizwa. Badala yake alifukuzwa kutoka mjini (bt. 213, 214 na 216). Mamake pia hakumpenda tena (ub. 221), alikosa kumpa chakula na kijana akawa na majonzi tele. Baada ya siku chache, alipatwa na maradhi

yasiyomwondokea na akafa baadaye.  Katika *Kivuli cha Sakawa*, baada ya wazee kwenda kinyume na mashauri yake, kulitokea vifo vingi katika jamii. Vijana waliojitokeza kupigana na wazungu waliuwawa kwa wingi hadi vijana waliokuwa wa umri mdogo wakaagizwa kuoa ili kizazi chao kisipotee.

### 3.3.17. **Kifo cha Jagina / Siri ya Kifo cha Jagina**

Mashujaa hawafi vivi hivi tu.Vifo vyao huwa vya ajabu. Hawafi kwa ugonjwa au maradhi bali wengi hufa kwa kufanyiwa tendo ndogo tu. Tendo hili linalosababisha kifo chao huwa ndiyo siri ya kufa kwao. Hii siri ya kifo chao huwazuia kufa hadi pale wanapokamilisha dhima yao. Wanapoifichua hivi tu, basi husalitiwa na kuuwawa. Kwa mantiki hii kifo huchukuliwa kama ni ishara ya mwisho wa kipindi fulani hasa kinapokuwa kifo cha kikafara. Kifo cha shujaa huchukuliwa kuwa kama ni kafara ya mwisho ambayo hutolewa ili kuleta ukombozi kamili kwa jamii yake (taz. Cirlot 1971). Kwa mfano, Samsoni katika Bibilia Takatifu, anakufa baada ya kunyolewa nywele zake ambapo nguvu zake zilikuwa. Naye Lwanda Magere anakufa kwa kufumwa mkuki kwenye kivuli chake na kusababisha kifo chake.

Waaidha, shujaa wa somo letu Fumo Liyongo anakufa baada ya kudungwa sindano ya shaba kwenye kitovu chake. Tumeeleza awali kuwa Sultani alikuwa amejaribu mbinu zote za kumuua akashindwa. Liyongo alipoifichua siri hii kuwa kimuuwacho ni sindano ya shaba kwenye kitovu chake, basi anakufa anapochomwa ile sindano ya shaba kwneye kitovu chake. Jagina hafi kikawaida tu, kifo chake huwa cha ajabu au huandamana na matukio ya ajabu. Fumo Liyongo anapotiwa ile sindano ya shaba kitovuni, hakufa pale kitandani. Aliamka akashika mshale akaenda kisimani. Akapiga goti na kutia mshale kwenye uta. Akawa katika hali hiyo kwa siku kadhaa. Ilikuwa vigumu kwa watu kuchota maji kisimani kwa kuhofia huenda Liyongo

amekasirika. Walisubiri kwa siku kadha hadi mwili wake ulipoanguka ndipo wakatambua kwamba alikuwa amekufa. Tunaambiwa katika *Utenzi wa Fumo Liyongo:*

Babake akishutuka
chembe uta akashika
kwa haraka akatoka
nde mi kayendeya. (**ub. 180**)

Akapija ondo lake
katambika chembe chake
kama hai ada yake
Chembe utani katiya. (**ub. 181**)

Watu mai wasiteke
waume na wanawake
kwa pot'e khabari yake
majimbo ikaeneya. (**ub. 183**)

Kipata siku katiti
kaanguka ni maiti
wakatambua umati
Liyongo ameifiya. (**ub. 202**)

Kama Liyongo, kifo cha Sakawa kilikuwa cha ajabu. Kabla ya kutoweka kwake, aliandaa karamu kubwa bomani mwake. Baada ya karamu, kila mmoja aliyehudhuria alijiondokea akiwa na furaha ghaya. Sakawa aliachwa akiwa mzima kama kigogo. Siku iliyofuata, kulisikika vilio kutoka boma la Sakawa. Watu walipofika, walipata habari kuwa Sakawa ameaga dunia na tayari amekwisha kuzikwa. Hili likawa la ajabu kwamba mtu aliyeheshimika anaweza kufa na kuzikwa bila kuzingatia mila na tamaduni za jamii ya Abagusii. Jambo lingine lilokuwa la kushangaza ni kuwa kaburi lililodaiwa kuwa alizikwa Sakawa lilionekana dogo kama la mtoto. Baada ya mashauriano kufanywa, wazee waliamua kuchimbua mwili wake ili uzikwe kulingana na tamaduni. La kushangaza ni kuwa mwili wake haukupatikana ila kiti chake, kiko na fimbo yake na vilevile mwishoni mwa kaburi kulikuwa na kichwa cha fahali aliyechinjwa siku ya karamu (*Kivuli cha Sakawa*, 82). Haya yalikuwa matukio ya ajabu yaliyoandamana na kifo cha Sakawa.

### 3.3.18. **Utabiri wa Majagina Hutimia**

Sifa mojawapo ya mashujaa ni kuwa huwa na uwezo wa kutabiri. Mara nyingi wanayoyatabiri kwa hakika hutimia mwishowe. Mwanawe Fumo Liyongo alipomwuliza kimuuwacho naye

akang'amua kuwa anakusudia kumuua, alitabibiri kwamba yale yote alikuwa ameambiwa amedanganywa. Ukweli ni kwamba baada ya kumuua babake, zile ahadi zote hazikutekelezwa, alikuwa amedanganya.

Yote aliyoyatabiri Sakawa pia yalitimia (Ochoi 2013: 104). Inavyojitokeza kwenye *Kivuli cha Sakawa* (uk. 48), utabiri wake kuwa jamii ingekumbwa na janga la njaa kutokana na nzige ambao wangeharibu mimea yote ulitimia. Tunaambiwa katika *Kivuli cha Sakawa* "miaka mitatu ilipita kabla ya utabiri wa Sakawa kutokea kuwa kweli. Wingu kubwa la nzige lilishambulia ardhi yao na kula mimea yote mashambani. Mwaka uliofuata kiangazi kikaandamana" (uk 51). Pia alitabiri kuwa kutakuja wageni wanaofanana na vipepeo katika ardhi yao na kuitwaa, utabiri huu unatimia na majilio ya wakoloni Waingereza kwenye makao ya jamii ya Wakisii.

### 3.3.19. **Jagina Huwa Gwiji katika Vita**

Mashujaa wengi hasa wa kijamii huzuka ili kukomboa jamii zao kutokana na mashambulizi kutoka kwa maadui wao. Hivyo basi, shujaa sharti awe na uwezo wa kupigana vita na kuikomboa jamii yake. Tzu (1910) anasema uelewa wa kina wa fani ya vita una umuhimu mkubwa kwa jamii inayohusika kwa kuwa huhusu uzima na mauti, usalama na maangamizi. Kwa mantiki hii, uchunguzi kuhusu vita una umuhimu usioweza kupuuzwa na yeyote yule. Kati ya vipengele muhimu anavyovitaja Tzu, kile cha muhimu kwetu ni kumhusu amri jeshi wa vita. Anasema kwamba amri jeshi huwakilisha busara, ukali, ujasiri, uthabiti na ukarimu. Vipengele hivi anavyovitaja Tzu vinajitokeza kwenye majagina Sakawa na Fumo Liyongo.

Mashujaa tunaowashughulikia hawaogopi chochote na huwa na nguvu nyingi. Fumo Liyongo alizuka katika kipindi kilichojaa misukosuko ya kivita katika janibu za Afrika Mashariki. Utenzi

wa Fumo Liyongo unamsawiri kama gwiji wa kivita aliyeweza kuwakabili watu wengi kwa wakati mmoja. Tunaelezwa:

Mfalume kawambiya
Wagala kiwasifiya
"Huwegema watu miya
wasiweze hukimbiya. (**ub. 12**)

Ruhu zikenda kishindo
zimo zao hukoma ondo
huyo ni bwana wa kondo
ashindaye jeshi niya (**ub. 35**)

"Na tumfanye amiri
zikiya zita ni kheri
atakufa kwa uzuri
maana hatokimbiya. (**ub. 90**)

Kadhalika, Liyongo anasawiriwa kuwa hodari kwa kutumia mshale. Haya yanadhihirika anapoangua makoma mengi ajabu kwa kutumia mshale jambo linalowafanya Wasanye na Wadahalo kmwogopa zaidi. Isitoshe, Liyongo anakufa akiwa ameshika mshale uliotiwa kwenye uta akiwa amepiga goti moja chini tayari kufuma. Haya yanadhihirishwa katika beti zifuatazo kwenye *Utenzi wa Fumo Liyongo*:

Akawambia "Ngojani"
akatowa mkobani
chembe katia ngweni
makoma kuwanguliya (**ub. 65**)

Achangusha ngaa ndima
ni mangi mno makoma
awa wut'e wakaatama
ajabu zikawangiya. (**ub. 66**)

Babake akishutuka
chembe uta akashika
kwa haraka akatoka
nde mi kayendeya. (**ub. 180**)

Akapija ondo lake
katambika chembe chake
kama hai ada yake
chembe utani katiya. (**ub. 181**)

Tofauti na Fumo Liyongo, Sakawa hajasawiriwa kama gwiji vitani. Japo alizuka wakati kulikuwa na msukosuko wa kivita kati ya jamii ya Wakisii na majirani wao, mwenyewe hakuhusika vitani. Ila tunaambiwa kwamba ushauri aliowapa wazee wa koo zote sita za jamii

yake ndio uliosababisha kusitishwa kwa mgogoro huo. Aliwashauri wote waungane katika mapambano dhidi ya maadui wao. Kulingana na Ochoi (2013), hirizi aliyotengeneza kutokana na panya waliokufa ndiyo iliyotumiwa kuwaletea ufanisi mkubwa kwenye vita vya Saosao. Tunaweza kusema kwamba Sakawa alikuwa shujaa kiuwakilishi.

### 3.3.20. **Shujaa "Hafi" na Hukumbukwa Milele**

Ama kweli kifo si jambo linalochangamkiwa na yeyote kwa kuwa huwakilisha mwisho wa enzi fulani (Ferber, 1999;Cirlot, 1971). Kwa sababu hii wanajamii "hawawaui" mashujaa wao ama kukubali kifo chao. Tofauti na mashujaa, watu wa kawaida wanapokufa, hasahaulika baada ya muda fulani kupita. Shujaa anapokufa, wanajamii hawaamini kuwa shujaa wao amekufa, huchukulia kuwa ameenda safari na aterejea kuwakomboa. Wengine huwa na matarajio kuwa akija atawaletea zawadi. Kwa hivyo matumaini katika nyoyo za wanajamii huwa hai wakimsubiri shujaa wao kurejea na zawadi.

Mashujaa wa somo letu Sakawa na Fumo Liyongo wanakumbukwa bado na jamii zao na watu wa jamii nyingine kutokana na matendo yao ya kishujaa. Katika *Kivuli cha Sakawa* (uk. 91) tunaelezwa; "Sakawa ambaye alitoweka kwa njia isiyoeleweka angerejea siku moja kuwaokoa watu wa jamii yake kutoka kwa utawala dhalimu wa Waingereza". Haya yalikuwa matumaini ya wanajamii kwa kuamini kuwa shujaa wao hajafa. Vile vile tunaelezwa; "hadi wa leo, Sakawa yungali katika vinywa vya Abagusii". Hii ni kusema kwamba shujaa hasahauliki.

### 3.3.21. **Jina la Jagina**

Majina ni kipengele muhimu katika fasihi kinachowezesha uumbaji na utambulishaji wa wahusika au mahali. Katika tamaduni nyingi kote ulimwenguni, majina huwa na maana fulani muhimu kwa kuwa yanaashiria tabia au sifa fulani. Wakati mwingine, shujaa hapewi jina vivi

hivi tu, jina lake huashiria sifa fulani aliyonayo shujaa. Jina hutumiwa kumtambulisha mtu. Katika isimu, majina hujitokeza kwenye kategoria ya nomino za pekee. Taaluma ya onomastiki[7] inaelekea kuepuka kutumia vigezo vya ndani ya lugha na kuzingatia vile vya kimuktadha (Piller na Chapman 2009). Kutokana na jina, tunaweza tukaelezea tabia ya shujaa. Hivi ni kusema kwamba, shujaa hupewa jina na wanajamii kutokana na hulka yake au wakati mwingine kutokana na maumbile au hata matendo yake. Anaweza akapewa majina mengi yakiwemo hata ya lakabu inapobidi.

Fumo Liyongo kama shujaa wa Waswahili amepewa jina kulingana na sifa yake. Katika hali hii tunaweza kusema kwamba hili ni jina la kimajazi. Majazi ni mbinu ya kutumia majina yanayofumbata tabia, sifa au matendo ya wahusika, mahali au mandhari katika kazi za kifasihi. Majazi humwezesha mtunzi kuchimuza mtazamo wake kuwahusu wahusika fulani na mwelekeo wa hadithi nzima (Wamitila 2004: 197). Majazi ni aina ya upenyezi wa mwandishi kwa kumwelekeza msomaji kwenye tathmini au uelewaji maalum (Wamitila 2008:378). Jina 'Fumo' ni jina linalotumiwa na Waswahili kurejelea mkuki wenye chembe pana mno na ambao hutumika katika vita kuangamiza maadui. Matumizi ya majazi huweza kufungamanishwa na ushabihikweli[8] wa kazi zinazohusika hasa kwa jamii ambazo majina huwa na maana. Utoaji wa majina katika hali halisi una misingi ya kimajazi. Fumo Liyongo ni shujaa wa kivita na ana uwezo wa kuangamiza watu wengi kama ilivyo fumo tulivyoeleza hapo awali (ub. 12, 35). Hivyo amepewa jina hili kutokana na ushujaa wake vitani na uwezo wa kuwaangamiza watu wengi. Gichamba (2005:82) akimrejelea Allen (1993:228) anasema kuwa, nembo ya mkuki wenye chembe kipana (fumo) hupamba mojawapo wa msikiti wa Gedi na pia hujitokeza kwenye maeneo ya juu ya mashubaka ya misikiti mingi ya kaskazini. Anadai kuwa neno 'fumo' lilifasiriwa kama 'mwana mfalme' na lilitumiwa na familia ya kifalme ya Pate kwa jina

Nabahani, kama neno la heshima. Huenda walilitoa jina hilo kutokana na jina la Fumo Liyongo baada ya ushindi wao dhidi yake katika karne ya kumi na tano. Liyongo mwenyewe alikuwa mwana wa mfalme na kisha akawa mfalme wa dola ya Ozi. Waaidha, *Utenzi wa Fumo Liyongo* unatueleza kuwa Fumo Liyongo alikuwa mwenye heshima na adabu, hasa pale anapoombwa na sultani wa pate afike mjini pate ili Wagalla wapate kumtazama. Tunaelezwa;

Tumi kenda kwa haraka
kwa Liyongo akafika
kampa kaumunika
akasoma yot'e piya. (**ub. 20**)

Na Liyongo akajibu
kwa hishima na adabu
"Nitakuja kwa karibu
nitwiiye Maulana." (**ub. 21**)

Kwa upande mwingine, tofauti na Fumo Liyongo, jina Sakawa ni jina tu la kawaida alilopewa kulingana na tamaduni za jamii ya Wakisii.

### 3.3.22. **Jagina huchukuliwa na Jamii kama Hidaya**

Majagina huchukuliwa kama hidaya kwa jamii kutoka kwa Mola. Hii ndio sababu mashujaa huhusishwa na jambo lolote jema na huchukuliwa kuwa watu wema katika jamii. Mashujaa huwa watetezi wa haki za wanajamii. Mara nyingi hawalipizi kisasi hata wanapowajua mahasidi wao. Majagina huwa na heshima na adabu. Katika *Utenzi wa Fumo Liyongo,* Liyongo anasawiriwa kama zawadi kwa jamii hata Wagalla wakataka mbegu yake:

Mfalume kawambiya
ni huyo amezokuya
sasa hiyau tangiya
mutaona ni hidaya (**ub. 32**)

"Twaitaka mbeu yake
nasi kwetu tuipeke
kwa furaha tumuweke
apate kutuzaliya". (**ub. 90**)

Liyongo pia anasawiriwa kama mwenye adabu na heshima inavyodhibitishwa katika ubeti ufuatao:

Na Liyongo akajibu
kwa hishima na adabu
"Nitakuja kwa karibu
nitwiiye Maulana." (**ubeti wa 21**)

Isitoshe, japo Liyongo alijua sultani alikuwa na nia ya kumuua, hakujaribu kulipiza kisasi japo alikuwa na uwezo wa kufanya hivyo.

Kama Liyongo, Sakawa naye anachukuliwa kama zawadi kwa jamii. Wanajamii walimwona kama aliyetumwa kwao kuwakomboa ndiposa hata baada ya "kifo" chake, waliendelea kungoja kwamba angerudi kuwaokoa kutokana na udhalimu wa Waingereza.

## 3.4. **Hitimisho**

Ni wazi kwamba mashujaa wawe wa kidini au wa kuhistoria / kijamii huwa na sifa bia kadhaa zinazofanana. Ubia wenyewe unadhihirishwa kutokana na kuwepo kwa sifa kadha ambazo zinafanana jinsi tumedhihirisha kwenye uchunguzi huu. Sifa za Fumo Liyongo na za Sakawa kwa kiasi kikubwa zinafanana. Tofauti baina yao ni chache mno. Tofauti hizi ni pamoja na utabiri wa kuzaliwa ambapo hatukupata data katika maadishi inayozungumzia utabiri wa kuzaliwa kwa Liyongo. Vilevile hatukupata historia ya ukembe na ujana wake. Kuhusu umbo, Sakawa ana umbo la kawaida ilhali Liyongo ni jitu. Isitoshe, Sakawa hasheheni sifa ya ugwiji katika vita kwa kuwa hajajitokeza kuenda kwenye uwanja wa vita kushiriki mapigano. Hata hivyo mchango wake kwenye ushindi wa vita vya Saosao ni mkubwa. Isitoshe, sifa ya jina la shujaa inatofautiana kwani Sakawa anapewa jina la kawaida tu kulingana na utamaduni wa Wakisii kinyume na Fumo Liyongo ambaye alipewa jina la kimajazi.

[1] Hili jina limetumiwa na mwandishi kumrejelea babake Sakawa ambaye kwingineko tumesema kwamba anaitwa Nyakembugumbugu. Hili pia linadhihirisha ubunifu wa mwandishi.
[2] Tazama sehemu ya majagina huwa hidaya kwa wanajamii (3.3.22)

[3] Mifano ya wanawake mashujaa ni pamoja na Wangu wa Makeri na Mekatilili wa Medza. Katika jamii ya Wakisii, Moraa, anachukuliwa kama shujaa kwa kumpa Otenyo hirizi itakayomkinga anapoenda kukabiliana na Mwingereza.

[4]Katika mazungumzo na mzee Maguto na Atemba, sifa hii ya kuzaliwa akiwa ameota meno haikujitokeza. Katika hali kama hii, tunasema kwamba huo ni ubunifu wa mwandishi (ikiwa Sakawa hakuwa amezaliwa akiwa na meno) ambao huifanya kazi hii kuwa ya kisanaa kinyume na madai ya baadhi ya wataalamu kwamba huu si utungo wa sanaa bali ni masimulizi.

[5] Knappert (1983:146)

[6] Sehemu ya 3.3.15

[7] Taaluma inayochunguza, kuchambua na kuchanganua chimbuko, maana, matumizi na uteuzi wa majina ya pekee.

[8] Hii ni hali ya mwandishi kuteua na kuwasilisha malighafi yake kwa namna inayokaribiana na ukweli ulivyo katika maisha halisi. Rejelea Wamitila (2003) *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia*

# SURA YA NNE

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 4.0. **Utangulizi**

Kwenye sura hii matokeo ya utafiti wetu yameshughulikiwa kulingana na madhumuni ya uuchunguzi wetu. Tumejadili pia upimaji wa nadharia tete pamoja na mapendekezo yetu katika tasnifu hii.

## 4.1. **Muhtasari wa Utafiti**

Utafiti huu umehusu kuwalinganisha majagina Fumo Liyongo na Sakawa kwa lengo la kuchunguza ikiwa wanajitokeza kuwa na sifa bia za majagina kama walivyo majagina wengi. Katika kufikia lengo hili madhumuni ya utafiti wetu yalikuwa ni kwanza, kuzipambanua sifa za kishujaa za Sakawa na Fumo Liyongo zinavyosawiriwa katika *Kivuli cha Sakawa* na *Utenzi wa Fumo Liyongo.* Pili tulilenga kuchunguza sifa za mashujaa zinazofanana na zinazotofautiana. Tatu tulidhamiria kuelezea historia ya Fumo Liyongo na Sakawa kwa kuifungamanisha na ile ya jamii zao ili kuonyesha yale mambo yaliyochangia kuzuka kwao katika jamii zao. Umuhimu wa utafiti huu ulikuwa ni kuchangia maandishi ya kitaaluma katika uwanja wa fasihi simulizi hasa tungo za visasili na tendi pamoja na historia na maendeleo ya lugha ya Kiswahili na vilevile kwenye uwanja wa Isimu Linganishi ambapo lugha mbili za Kibantu zimejitokeza. Ni utafiti wa maktabani na ambapo mtafiti alisoma *Utenzi wa Fumo Liyongo* na masimulizi ya *Kivuli cha Sakawa* ili kupata data ya kuchanganuliwa. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uhakiki wa vikale iliyoasisiwa na Carl G. Jung (1959) katika kuchanganua vipengele muhimu vya sifa za majagina. Utafiti huu una sura nne.

Katika sura ya kwanza, masuala muhimu ya kijumla katika utafiti yameshugulikiwa. Haya ni pamoja na maswali ya utafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia tete, msingi wa kinadharia

yaliyoandikwa kuhusiana na mada yetu ya utafiti na mengine ambayo yametanguliza utafiti wetu pamoja na kutuongoza katika mchakato mzima wa utafiti.

Katika sura ya pili, dhana muhimu kuwahusu majagina kama vile sifa na aina za majagina zimeangaziwa. Isitoshe tumeieleza historia ya mashujaa Sakawa na Fumo Liyongo sambamba na ile ya jamii zao. Tumeangalia mazingira yaliyowazua mashujaa hawa. Migogoro ya kivita iliyowazua Fumo Liyongo na Sakawa imebainishwa. Nafasi ya historia ya jamii zao katika kuwaelewa mashujaa imebainishwa.

Katika sura ya tatu, sifa za kishujaa Fumo Liyongo na Sakawa zimelinganishwa. Hii ndiyo sura iliyokuwa kiini cha utafiti wetu. Katika kuzipambanua sifa hizi, tulipata kuwa mashujaa hawa wanadhihirisha kuwa na sifa za kishujaa ambazo zinadhihirika katika mashujaa wengine kote ulimwenguni. Mashujaa hawa wana sifa nyingi zinazoshabihiana na tofauti kati yao ni ndogo mno. Matokeo ya utafiti wetu yameshughulikiwa kwenye sehemu inayofuata.

## 4.2. **Matokeo ya Utafiti**

Kwenye sehemu hii tunahusisha madhumuni yetu ya utafiti katika kuchunguza yale yanayojitokeza katika utafiti wetu. Tumejaribu kuonyesha ulinganifu uliopo baina ya Sakawa na Fumo Liyongo. Utafiti huu ulidhamiria kujibu maswali yafuatayo ya utafiti (i) Ni sifa zipi za kishujaa zinazojitokeza katika *Kivuli cha Sakawa* na *Utenzi wa Fumo Liyongo?* (ii) Je, ni sifa zipi zinazofanana na zipi zinazozotofautiana za majagina hawa wawili? (iii) Je, mazingira yaliyochangia kuzuka kwa majagina hawa wawili ni sawa ama mambo yaliyochangia kuzuka kwao katika jamii zao ni tofauti? Matokeo yafuatayo yaliafikiwa:

Katika uchunguzi wa swali la kwanza, vigezo vya hulka, historia na matendo ya Sakawa na Fumo Liyongo vilikuwa nguzo muhimu katika uchunguzi wa ulinganifu wa sifa za majagina

hawa. Hii ni kwa sababu vipengele hivi hutuwezesha kubainisha sifa kila mmoja wao alizo nazo maishani. Kwa kuzingatia vigezo hivi uchunguzi wetu umedhihirisha kwamba sifa za mashujaa hawa zinalingana kwa kiasi kikubwa na tofauti kati yao ni ndogo. Sifa zinazofanana ni kama wote ni wanaume waliotoka kwenye ukoo maarufu katika jamii zao, walikuwa watu maarufu waliopendwa na wengi hata nje ya jamii wanamotoka, maisha yao yamezingitwa na dhiki tupu ambazo husababishwa na pingamizi walizozipata kutoka kwa adui wao, walifunga safari kujiokoa na kuyaokoa maisha ya wanajamii walio wengi na walisalitiwa na hatimaye kufa kiajabu.

Katika kuchunguza namna walivyofanana na kutofautiana, uchunguzi umebainisha kwamba tofauti zao ni ndogo tu hivyo kubainisha kauli kwamba majagina huwa na sifa bia zinazofanana kwa kiasi kikubwa. Tofauti zilizojitokeza baina ya Sakawa na Fumo Liyongo ni pamoja na utabiri kuhusu kuzaliwa kwao, ambapo hatujaelezwa lolote kuhusu kutabiriwa kwa kuzaliwa kwa Fumo Liyongo kama ilivyo katika kuzaliwa kwa Sakawa. Isitoshe, kuhusu umbo, imejitokeza kwamba Sakawa alikuwa na umbo la kawaida ilhali Fumo Liyongo alikuwa mkubwa. Pia jina analopewa Sakawa lilikuwa la kawaida ambalo halina maanda ya ndani au ya kimajazi kama lile alilopewa Fumo Liyongo. Inadhihirika kwamba majagina hawa walikuwa hodari kwenye fani ya vita ingawa hatuelezwi kwamba Sakawa alishiriki vita moja kwa moja bali alichangia upatikanaji wa ushindi kwenye vita vya Saosao.

Mwisho tulichukulia kuwa kuzuka kwa mashujaa hawa ni kutaka kutetea kabila lao dhidi ya adui na ndiko kuliwajenga kama mashujaa. Katika sura ya pili, tumeeleza msukosuko wa kivita uliowazua mashujaa hawa. Hivyo ni wazi kwamba mashujaa hawazuki katika ombwe tupu.

## 4.3. **Mapendekezo**

Utafiti huu ulishughulikia ulinganishi wa majagina Sakawa na Fumo Liyongo. Kwa kuwa tungo za fasihi simulizi huweza kuwa na tofauti za hapa na pale kutokana na ufaraguzi kwenye uwasilishi, mtafiti anapendekeza utafiti ufanyiwe katika majagina ili kubainisha baadhi ya sifa ambazo hazijajitokeza kikamilifu kwenye tungo tulizozitumia kukusanya data yetu. Ingawa maisha ya ujana wa Sakawa yameshughulikiwa kwa kiasi, yale ya Fumo Liyongo hayajatajwa popote hivi kwamba ni vigumu kufikia uamuzi kuhusu maisha yake ya kipindi hiki. Ilivyo ni kwamba Fumo Liyongo katika wakati fulani alikuwa kijani lakini hili halijitokezi kwenye *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Hivyo basi pengo hili linafaa kushughulikiwa ili kuyaelewa maisha yake tangu kuzaliwa hadi kifo chake.

Kuna mambo mengi yanayoweza kushughulikiwa kuhusiana na taasisi ya ushujaa. Utafiti huu ni mojawapo tu ya masuala haya. Kwa sababu hatuwezi kuyashughulikia mambo haya yote, tumejikita katika ulinganishi wa sifa za mashujaa wawili wa Kiafrika wote wakiwa ni wa Kibantu. Huenda hatujataja sifa zote katika utafiti wetu, hivyo basi, utafiti huu huenda ukawa msingi bora kwa watafiti wengine ambao wanaweza kutalii sifa zaidi na kuwalinganisha mashujaa kutoka jamii nyingine au hata wa kidini.

Tunapendekeza pia uhakiki wa kimtindo ufanywe katika tungo zinazohusu majagina hawa wawili, Fumo Liyongo na Sakawa au hata ulinganishi.

## 4.4. **Hitimisho**

Kwenye uchunguzi huu tumebainisha kwamba majagina huwa na sifa kadha ambazo hufanana. Hali hii inadhihirisha vikale vilivyomo akilini mwa jamii mbalimbali ambazo zimedumishwa kwenye akili laza jumuishi zao. Kwa kuwatumia Fumo Liyongo na Sakawa, imedhihirika

kwamba sifa hizi huwa na ubia fulani, hali ambayo hudhihirisha kwamba binadamu wote wana kitovu kimoja. Hivyo basi tunaweza kusema kwamba vikale huvuka mipaka ya kihistoria, kijografia na hata kitanzu. Hii inadhihirika kwenye tungo mbili tulizoteua kutumia ambazo ziliandikwa kwenye vipindi tofauti vya kihistoria, kwenye maeneo tofauti na kutumia tanzu mbili tofauti za kihistoria.

## MAREJELEO


Abrams, M. H. (1999). *A Glossary of Literary Terms* (7th Ed.). Massachusetts: Heinle& Heinle.

Achieng', O. B. (2012). "Sifa za Mashujaa na Umuhimu wao katika Jamii Zao: Ulinganifu wa Fumo Liyongo na Lwanda Magere". Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi: Haijachapishwa.

Akama, J. S. na Maxon, R. (2006). *Ethnography of the Gusii of Western Kenya: A Vanishing Cultural Heritage.* New York: The Edwin Mellen Press.

Aylestock, N. (2009). *Supreme Heroes.* S.I.: Iuniverse Inc.

Bitugi, E. M. (2010). *Kivuli Cha Sakawa*. Canada: Nsemia Inc. Publishers.

___________ (2004). *Mkasa wa Shujaa Liyongo*. Nairobi: Phoenix Publishers.S

Bressler, C. E. (2011). *Literary Criticism: An Introduction to Theory and Practice.* Boston: Longman.

Brooks, C.A (1970). "The Conquest of the Abagusii 1900 – 1914". Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi: Haijachapishwa.

Burton, B. A. (1968). "Prolegomena to Archetypal Criticism". Tasnifu ya Uzamili , Chuo Kikuu cha Texas Technological College.

Butler, B. (1979). *The Myth of a Hero*. London, Rider & Company.

Campbell, C. J., Brown, P., na Stuart, L. (2003). *The Hero Journey: Joseph Campbell on his Life and Work.* Novato, Calif: New World Library.

Campbell, J. (1970). *Myths, Dreams, and Religion.* New York: E. P. Dutton.

Carlyle, T. (1924). *On Heroes, Hero Worship na the Heroic History.* London: Macmillan & Co. Ltd.

Childs, P. na Fowler R., (Wah) (2006). *The Routledge Dictionary of Literary Terms*. London: Routledge.

Cirlot, J. E. (1971). *A Dictionary of Symbols.* (J. Sage, Trans.) London: Routledge.

Derek, N. (1995). *Historical Texts from the Swahili Coast.* Part III.

Ferber, M. (2007). *Dictionary of Literary Symbols*. New York: Cambridge University Press

Frye, N. (1990). *Anatomy of Criticism.* Princeton: Princeton University Press.

Guerin, W. L., Labor, E., Morgan, L., Reesman, J. C., na Willingham, J. R. (Eds.). (2010). *A Handbook of Critical Approaches to Literature* (6th ed.). Oxforp: OUP.

Gichamba, J. M. (2005). "Sifa za Mashujaa na Umuhimu wao katika Jamii Zao: Ulinganifu wa Fumo Liyongo na Shaka Zulu". Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi: Haijachapishwa.

Green, T. A. (Mha) (1997). *Folklore: An Encyclopedia of Beliefs, Customs, Tales, Music and Art.* California: ABC~CLIO.

Guthrie, M. (1948). *The Classfication of the Bantu Languages.* London: Oxford University Press.

Halpé, A. (2010). "Between Myth and Meaning: The Function of Myth in Four Post Colonial Novels". Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Toronto.

Harries, L. (1962). *Swahili Poetry*. Oxford: Claire don Press

Jung, C. G. (Ed.). (1964). *Man and His Symbols.* New York: Dell Publishing Co. Inc.

__________ (1990). *The Archetypes and the Collective Unconscious* (2nd ed.). Princeton: Bollingen and Princeton University Press.

__________(1996). *Psychology and Literature In 20th Century Literary Criticism.* Singapore: Longman et Singapore Publishers.

Kahler, E. (1961). The Nature of the Symbol. (R. May, Ed.) *Symbolism in Religion and Literature*, 53 - 70.

Kijumwa, M. (1973). *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Dar es Salaam. TUKI.

Knappert, J. (1970). *Myths and Legends of the Swahili*. Nairobi: Heinemann Educational Books.

_________ (1983). *Epic Poetry in Swahili and Other African Languages*. Netherlands: E.J. Brill, Leiden. (Volume Twelve)

Landman, M. (2006). "Dream of a Thousand Heroes: The Archtypal Hero in Contemporary Mythology, with reference to the Sanman by Neil Gainman." Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha South Africa (UNISA): Haijachapishwa.

Longhorn (2011). *Kamusi ya Karne ya 21.* Nairobi: Longhorn Publishers (K) Ltd.

Mbele, J. L. (1986). "The Liongo Fumo Epic & The Scholars". *Kiswahili, 53*(1), 128 – 145.

Mulokozi, M.M. (1999). *Tenzi Tatu za Kale*. Dar es Salaam. TUKI.

Muniu, G. G., (2011). "Ujagina wa Mwanamke Katika Pango". Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Mutiso, Kineene (1985). "Hurafa na Uyakinifu katika Hamziyya". Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

_____________ (1999). "Sira ya Majagina: Buddha na Muhammadi".

Nurse, D. na Spear, T. (1985). *The Swahili. Reconstructing the History and Language of an African Society, 800-1500.*

Ochieng', W.R. (1974). *A Pre-Colonial History of the Gusii of Western Kenya C.A.D. 1500 – 1914.* Nairobi: East African Literature Bureau.

Ochoi, J. A. (2013). *The History and Traditions of Abagusii People of Kenya*. Canada:

Rawling, J. K. (2003). *Harry Potter and the order of the Phoenix.* New York: Scholastic Inc.

Robert, M. M. (1971). "British Rule in Gusiiland, 1907 – 1963". Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Syracuse.

Steere, E. (1870). *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar*. London: Bell & Davy.

Sugg, R. P. (1992). *Jungian Literary Criticism.* Evanston: Northwestern University Press.

Tallman, B. (2005). *Archetypes for Spiritual Direction: Discovering the Spiritual Heroes Within.* New York: Paulist Press.

TATAKI (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la Tatu). Nairobi: Oxford University Press.

Tzu, S. (1910). *The Art of War.* (L. Giles, Trans.) England: The Puppet Press. Retrieved Sept 2nd, 2015, from http://www.puppetpress.com/classics/ArtofWarbySunTzu.pdf

Vogler, C. (2007). *The Writers Journey.* Laurel Canyon Blvd: Michael Wiese Productions.

Voytilla, S. (1999). *Myth and the Movies: Discovering the Mythic Structure of 50 Unforgettable Films.* Michael Wiese Productions.

Werner, A. (1968). *Myths and Legends of the Bantu*. London; Frank Cass & Company Limited.

Wood, M. (2005). *In Search of Myths and Heroes: Exploring Four Epic Legends of the World.* Berkley: University of California Press.

Zhugang. (1997). *Western Literary Criticism.* Dalian: Dalian Foreign Language Institute Publication.